

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 17 Juni, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita mwuliza swal wa kwanza, nataka niwashukuru sana Wenyeviti wa Bunge wote, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid na Mheshimiwa Job Ndugai, kwa muda kama wa siku nzima jana na juzi nusu siku, wamekaa katika kiti hiki kuongoza shughuli na nyote nadhani mnakiri kwamba wameongoza kwa hali ya umadhubuti mkubwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, jambo la pili Mheshimiwa Naibu Spika anatuwakilisha katika Mkutano wa Maspika wa Bonde la mto Nile kule Cairo na tunamtarajia kurejea siku ya Jumamosi, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Na. 52

**Kuigawa Wilaya ya Kondo ya Wilaya Mbili**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE (K.n.y. MHE. PASCHAL C. DEGERA)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Kondo ni kubwa sana na ina wakazi takribani laki tano (500,000); na kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilitoa mapendekezo ya kugawa Wilaya hiyo katika Wilaya mbili ili kusogea huduma karibu na wananchi.

Je, Serikali imefikia hatua gani katika mchakato wa kuigawa Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Degera kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kuchukua nafasi hii kumpa pole sana kwa kufiwa na mama yake mzazi, tunatambua kwamba isingekuwa ni hili tatizo angekuwepo hapa ili aulize swali lake. Sisi sote tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kumpitisha katika hali hii ngumu na aweze kumzika mama yake kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa ni moja kati ya Wilaya 56 ambazo ziliwasilisha maombi ya kutaka kugawanywa. Baada ya kupokea maombi hayo, ofisi yangu imefanya zoezi la uchambuzi ili kuona ni Wilaya zipi ambazo zinakidhi vigezo vilivyopo. Hatua inayofuata ni kuwasilisha maoni na mapendekezo ya kitaalamu kwa Mheshimiwa Rais ambaye ndiye mwenye mamlaka ya kisheria ya kuigawa Nchi katika Mikoa na Wilaya.

Mhehsimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maeneo ya utawala yanagawanywa kulingana na vigezo vilivyowekwa kisheria, na uwezo wa kifedha wa Serikali.

Pia tukumbuke kwamba Wilaya 10 zilizogawanywa kipindi cha awamu ya tatu bado hazijamalizika kujengwa miundombinu. Pindi itakapokamilika katika Wilaya hizo Mheshimiwa Rais kama ataona inafaa atatangaza Wilaya mpya. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kwamba kuna Wilaya zaidi ya 58 ambazo zimetimiza vigezo, na mmepeleka maombi ya kugawanywa kuwa Wilaya mbili, na kwa kuwa kuna Wilaya ambazo zina idadi ya watu zaidi ya laki saba kwa mfano Kondoa, Kilosa, Geita na Kahama.

(a)Je, Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba pamoja na kwamba wanasubiri hizo Wilaya 54 zigawanywe. Je, zoezi hili haliwezi kufanywa kwa awamu badala ya kungoja kuja kugawa Wilaya zote hizo na gharama itakuwa kubwa kwa Serikali?

(b)Kwa kuwa hivi sasa Serikali inajiandaa kutangaza vijiji vipya na Kata mpya. Je, ni lini Serikali itatangaza vilevile Tarafa mpya ikiwemo tarafa ya Mima Wilayani Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Lubeleje kwa namna anavyofuutilia masuala haya, mimi nakumbuka mara nyingi sana amekuja ofisini, natambua kwamba pia amekutana na

Waziri wa Nchi kuzungumzia masuala haya pamoja na Waziri Mkuu mwenyewe, amesema hizi Wilaya 58 ambazo zimeleta maombi tunaonaje kama tungeweza kuanza kwa awamu.

Mimi sioni tatizo kwa hili analolizungumza kwa sababu wakati wa kumshauri Mheshimiwa Rais unachofanya ni kushauri kama anavyoshauri hapa, kwamba tutatoka tutamwambia kuna mawazo.

Je, unaonaje kama tutakwenda awamu kwa awamu, lakini bado tutabakia pale pale ambapo tunazungumzia kuona kwamba Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa zinakamilika kimiundombinu kwa maana ya kwamba Serikali haiendi tu moja kwa moja inaangalia kwanza zile ambazo imezianzisha zinaweka mazingira ambayo yatawezesha huduma kuwa karibu na wananchi kama ilivyotarajiwa kwa maana ya kuunda Wilaya yenye.

Mheshimiwa Spika, kimsingi mimi sioni kama kuna kuna tatizo lolote katika hili analolizungumzia hapa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la vijiji pamoja na Kata na Tarafa, la Vijiji Mheshimiwa Waziri wa Nchi alishajibu hapa na hata Waziri Mkuu alishajibu kwamba zoezi lile limekamilika, tupende tusipende ni lazima majina yale na vijiji vile ni lazima yatolewe kwa sababu huko mbele tunakokwenda, tunakwenda kwenye uchaguzi ambao utakuwa unahusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hiyo ni suala la kutangaza tu na mimi huwa nakaa katika vikao hivyo, siyo kwamba najibu tu maswali huwa nakaa katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, inaonekana kwamba vijiji vingi vinakidhi vigezo vilivyowekwa, suala litakuwa ni mamlaka ambayo inaamua na kufanya maamuzi ya mwisho ndiyo itakayosema kwamba sasa ni kipi au kipi lakini kimsingi mimi naona hamna kiongozi yejote ambaye anaonekana kwamba ana tatizo na hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tarafa ambayo ameizungumzia hapa, tarafa inaingia katika eneo ambalo linatamkwa na Mheshimiwa Rais mwenyewe, na Tarafa hii ambayo anaizungumzia hapa Mheshimiwa Lubeleje imeletwa katika maombi kwa hiyo tutaiangalia kwa sura hiyo kwa maana ya kupeleka mapendekezo ili Mheshimiwa Rais aone uwezekano wa kuianzisha Tarafa hiyo.

Na. 53

### **Ujenzi wa Kijiji cha Millenia Micheweni**

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna mradi wa kujenga kijiji cha Milenia katika Jimbo la Micheweni kupidia mradi wa *UNDP*:-

- (a) Je, Serikali inaweza kutupa maelezo ya kina kuhusu mradi huo umefikia hatua gani na ni fedha kiasi gani kimeshatumika katika mradi huo?
- (b) Je, kwa nini mradi huo unasuasua?
- (c) Je, ni miradi ipi midogo imeshatekelezwa katika mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Jimbo la Micheweni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi mradi wa ujenzi wa Kijiji cha Millennia huko Micheweni, Pemba utekelezaji wake bado haujaanza. Hali hii imetokana na kuchelewa kupatikana kwa fedha kutoka kwa Mkurugenzi wa Mradi wa Vijiji vya Millenia Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mnamo mwezi wa Septemba, 2008 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejulishwa rasmi kukubaliwa kwa ombi na kuahidiwa kupatiwa dola za kimarekani milioni 1.5 kwa ajili ya kusaidia uanzishwaji wa Kijiji cha Milenia huko Micheweni Pemba. Fedha hizo zitasaidiana na zile za Serikali ya Zanzibar zitakazotolewa kupidia Bajeti zake na zitatumika kwa kipindi cha miaka mitano(5). Vile vile, Afisi ya Mkurugenzi wa Mradi wa Vijiji ya Milenia imeiarifu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwa Mtaalam mshauri atawasili Zanzibar Mwezi Juni, 2009 na atakuwepo Zanzibar kwa kipindi cha miezi (3) kwa lengo la kufanya maandalizi ya uanzishwaji wa kijiji hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo napenda kumjulisha rasmi Mheshimiwa Shoka kuwa hadi sasa hakuna fedha ya mradi iliyotumika na hakuna miradi midogo midogo iliyokwishatekelezwa chini ya mradi huu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kabla sijafanya hivyo nashukuru kupata fursa hii katika Jimbo langu ya kuweza kujengewa hicho Kijiji. Vilevile nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

- (i) kuna miradi ambayo imeanzishwa kule Micheweni, kuna mradi wa ufugaji wa nyuki pamoja na mradi mwengine wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa, Mheshimiwa Naibu Waziri unasema mradi huu bado haujaanza miradi hii imetokea wapi?

(ii) Hivi karibuni alikuja Afisa kutoka *UN* katika Jimbo la Micheweni na bahati nzuri nilimtembeza mimi katika Jimbo zima la Micheweni, na tulipopita katika vijiji wananchi aliwapa ruhusa ya kuibua miradi ambayo wanaipenda wao wenyewe. Je, itakapofika kuanza kwa miradi, ile miradi waliyoichagua wananchi ndiyo itakayopewa kipaumbele?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwanza mradi wa ufugaji nyuki na mbuzi wa maziwa, kama sote tunavyofahamu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Wizara ya Kilimo Maliasili wanashughulika na miradi mbalimbali ya wananchi, ametaka kujua miradi hii imetoka wapi, nataka nimwaambie kwamba miradi hii imeanzishwa na wananchi chini ya Wizara ya Kilimo kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pili wananchi kuibua miradi yao, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la miradi ya milleniam siyo kuanzisha miradi mipyä, itaendeleza miradi ambayo wananchi wenyewe wameibua kwa maana hiyo hii miradi ambayo wananchi wameibua kwa lengo la kujipatia mapato itaendelezwa chini ya mradi huu wa millennia pamoja na kuanzisha miradi mingine ambayo itaonekana ina tija zaidi kwa wananchi wa Micheweni, mimi Micheweni ni kwetu nakufahamu.(*Makofi*)

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika ahsante sana, mimi nilitaka kujua tu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Je, miradi hii itakuwa kwa ajili ya Jimbo la Micheweni au Wilaya nzima ya Micheweni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kulingana na hali ya fedha zilizopo kwanza tutaanzia na Jimbo la Micheweni na baadaye tukiona kwamba mafanikio yamepatikana vizuri basi Serikali itatafuta fedha kupitia vyanzo vingine au kupitia fedha za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kuweza kutanua, kama mtakumbuka mkiangalia takwimu za viashiria Micheweni kama Wilaya kwa kweli wapo katika hali duni zaidi kuliko Wilaya zingine za Zanzibar.

Na. 54

#### **Ulipaji wa Kifuta Machozi na Udhibiti wa Wanyama Wakali**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mnamo tarehe 1/12/2008 Tembo mmoja kwa nyakati tofauti aliua watatu katika Kata ya Sengenya na Nangoma, Wilayani Nanyumbu tukio ambalo lilileta mtafaruku mkubwa na majonzi kwa wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, ndugu na jamaa za watu waliouawa katika tukio hilo watalipwa lini kifuta machozi na kwa kiasi gani?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti Tembo hao wanaotoka katika misitu ya uwindaji wa Msanjesi na Lukwika wasiendelee kuua wananchi na kuharibu mazao yao?

## **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka utaratibu wa kutoa kifuta machozi kwa mwananchi aliyeuawa na wanyamapori kiasi cha shilingi 200,00 kwa kila familia ya marehemu.

Malipo hayo hufanyika baada ya kuwepo uthibitisho wa taarifa za kifo kutoka katika uongozi wa Kijiji, Polisi, Mganga Mkuu wa Wilaya na Uongozi wa Halmashauri husika.

Aidha Wizara hutoa kifuta jasho kiasi cha shilingi laki moja kwa mazao katika shamba lenye ukubwa unaozidi ekari moja. Utaratibu wa kifuta jasho kwa mazao unahusisha uhakiki na uthibitisho wa uharibifu unaofanywa na Afisa Kilimo Wilaya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kijibu maswali ya Mheshimiwa Mkapa kama ifuatavyo:-

(a) Wizara yangu katika kutekeleza azma yake ya kulipa kifuta machozi kwa wafiwa ambao katika swali liloulizwa ni ndugu watatu waliouawa na tembo katika tukio la tarehe 1Desemba, 2008 katika Kata ya Sengenya na Nangomba, Wilaya ya Nanyumbu. Jumla ya shilingi 600,000 zilipelekwa tarehe 8 Januari, 2009 kwa Meneja wa mapori ya Akiba Lukwika/Lumesule na Msanjesi na zikalipwa kwa warithi wa marehemu kama ifuatavyo:-

(i) Jina la Marehemu ni Awetu Bilali Jina la Mrithi ni Shabihu Milanzi kiasi alicholipwa ni Sh. 200,000.

(ii) Jina la Marehemu ni Grace Sijale, Jina la Mrithi Pancras Sowani shilingi 200,000.

(iii) Jina la Marehemu ni Said Omary Mapemba, Jina la Mrithi ni Fatuma Hussein shilingi 200,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo ya Wilaya ya Nanyumbu wakiwepo Tembo, Serikali ina mipango ifuatayo:-

(1) Kuendelea kuimarisha doria za msako wa kudhibiti wanyamapori wahariburu. Aidha Wizara itaendelea kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kuajiri askari wanyamapori wa kutosha na pia kujenga kituo cha doria eneo la Lumesule kwa ajili ya kudhibiti wanyamapori waharibifu hususani tembo katika maeneo hayo yaliyo nje ya ya mapori ya Lukwika na Lumesule na Msanjesi.

(2) Kujumuisha wanyamapori waharibifu kwenye *quota* ya wanyamapor wanaowindwa kwa matumizi mbalimbali, kama vile uwindaji wa kitalii, leseni za nyara na uwindaji wa wananchi.

(3) Kushauri Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu kuchukua hatua za haraka za kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi katika viji ya vilivyopo katika eneo la Ushoroba wa wanyamaporili kuruhusu wanyamaporikupita bila kuziba katika Ushoroba huo kutoka eneo moja kwenda maeneo mengine. (*Makof*)

(4) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya na wafadhili wa WWF Serikali imeanzisha mradi wa kuwashirikisha wananchi katika uhifadhi na kutoa elimu stahili ya kupambana na wanyamapor waharibifu hususani tembo kwa kutumia mbinu mbadala za kuadhibiti ambazo zimethibitika kupunguza tatizo hilo.

(5) Serikali kupitia Idara ya Wanyamapor imetoa gari jipya ya *Landrover 110 (TDi)* Namba STK 1050 kwa Wilaya ya Nanyumbu kwa ajili ya kuongeza nguvu za kupambana na wanyamapor waharibifu hususani tembo.

**MHE. DUSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika ahsante sana. Kwanza napenda kuishukuru Serikali kwa kuitikia kilio changu cha kutupatia gari, lakini jambo la pili niishukuru tena Serikali kwa kutoa pole kwa wafiwa kwa kiasi hicho kilichotajwa.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi tarehe 2 Machi, 2009 mpiga kura wangu mwingine aliuawa na tembo katika kijiji cha Mkwahiya, lakini pamoja na matukio yote haya sijaona Mkurugenzi wa wanyampori, Naibu Waziri au Waziri mwenyewe angalau kuja kutembelea pale na kuona hali halisi. Safari zao utaona ni Seronera, Ngorongoro na huko kwingineko ambako kuna starehe.

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu hili? (*Makof*)

(b) Pamoja na wanyama hawa waharibifu kuna wanyama aina ya nyani, ngedere, na nguruwe pori ambao wanansumbua sana kule kwetu.

Je, Serikali haiwezi kutuletea nyavu hasa katika viji ya Chirigit, Makongondera na Mwamba ili waweze kudhibiti wanyama waharibifu hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kupokea shukrani za Mheshimiwa Mbunge na sisi kama Wizara tunafarijika pale ambapo kidogo tunachokifanya kutokana na uwezo wetu kinapokelewa na kutambulika. Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pole sana kwa Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Nanyumbu kwa tukio la tarehe 2 Machi, 2009 la mwananchi kuuawa na wanyama wakali. Matukio ya namna hii yameongezeka sana katika miaka ya karibuni na ndiyo maana mwezi Februari mwaka huu 2009 tulipitisha sheria Namba tano 2009 ya kudhibiti au kuboresha uhifadhi kwa maana ya kudhibiti wanyamapor.

Mheshimiwa Spika, hili suala la kutembelewa kwa kweli ni la kibinadamu na kwa bahati mbaya sana tukio hilo lilivyotokea sikumbuki vizuri mimi mwenyewe nilikuwa wapi na Waziri alikuwa wapi lakini kwa hakika ni jambo ambalo linastahili kuwapa pole na tulifanya hivyo. Kuwatemeblea kwa ajili ya kuwapa pole *physically* ni jambo ambalo mimi naomba nilichukue na kwa sababu msiba ulishatokea basi uungwana ni vizuri kuwaona na niseme kwamba tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kudhibiti wanyama wadogo wadogo kama nyani niseme nimelichukua tatizo mara nyingi inapotokea tunahitaji mawasiliano ya haraka katika Wizara ili tuweze kuchukua hatua ambazo zinazostahili. Kwa hivyo tutawasiliana na wenzenetu wa pori la akiba la Lumesule ili waweze kuangalia idadi au ukubwa wa tatizo halafu tuweze kuona ni njia gani inaweza kufaa, kupeleka nyavu ni njia mojawapo lakini hakika tunaweza kutumia njia zingine ambazo zinaweza kuwa *effective* zaidi. Hili nimelichukua na tutawaelekeza watu wetu waweze kuchukua hatua hiyo.(*Makofî*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo la wanyama waharibifu lipo nchi nzima na mahali pengi watu wameuawa nikitoa mifano michach ni kwamba katika pori la Ugara, Tutuo Sikonge, Ikinga –Peramiho, Ikolo na Mwangeza Iramba Mashariki na kwa kuwa lengo letu ni kuhakikisha kwamba wananchi na mali zao hawauwawi, na kwa vile tatizo kubwa ni uhaba wa askari na vitendea kazi.

Je, Serikali itakuwa tayari Bajeti hii kuhakikisha Halmashauri nyingi zinapewa vibali vya kuajiri Askri wa kutosha na nyenzo za kufanyia kazi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tatizo la migongano kati ya binadamu na wanyama hasa wanyama kuharibu mazao na hata kuua binadamu imeongezeka sana miaka ya hivi karibuni na ndiyo maana tumeanzisha sheria mpya ambayo inazingatia mazingira ya sasa na ku-*address* changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, katika sheria hii tulioipitisha Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kwamba tumependekeza kuwepo kwa mamlaka ya wanyamapori ambayo itakuwa na uwezo mkubwa zaidi ili kuweza kuajiri kiasi kikubwa cha askari wanaohitajika na kuweza kudhibiti tatizo hili. Lakini pia katika sheria hiyo tumependekeza kwamba tutabainisha upya maeneo ya mipaka ya wanyamapori. Kubainisha upya Shoroba na *dispersal areas* ili kupunguza mwingiliano kati ya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuruhusu Halmashauri ziweze kuajiri Askari wengi iwezekanavyo, niseme hili ni wazo zuri na changamoto itakuwa katika kila Halmashauri. Sisi kama Wizara haturuhusu au kutoruhusu Halmashauri kuajiri. Kila wakati tumekuwa tukiwasihii waajiri askari ili sisi tuweze kushirikiana nao kuweza ku-*complement effort* zao tuweze kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, hiyo itakuwa ni hatua njema na ninapenda kuwasih  
Halmashauri kufanya hivyo.

**MHE. DR. WILBROAD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa  
nafasi niulize swali dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo ya wanyama hawa waharibifu yapo mengi hususani pia  
katika vijiji vyangu vya Shakamo, Kitete, Endamagang na kadhalika, na kwa kuwa  
tulipitisha sheria hapa Bungeni Mwezi Februari, 2009 kama alivyosema Mheshimiwa  
Waziri na kwa kuwa Sheria yetu ya fidia hajifanyiwa marekebisho muda mrefu na  
inazungumzia fidia ya shilingi laki moja.

Je, Waziri atatuambia sasa ni lini sheria ile tuliyopitisha Februari mwaka huu iweze  
kufanya kazi wataleta marekebisho ya sheria hapa Bungeni ili watu wetu aidha kwa  
binadamu kuuliwa au kwa mali zao kuharibiwa waweze kupata fidia inayolingana kidogo  
na hali hiyo pamoja na kwamba binadamu huwa hafidiwi? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tatizo la  
uharibifu limeongezeka kama tulivyosema, kwenye sheria tuliyopitisha tulikuwa  
tumeazimia kwamba mapema iwezekanvyo sheria ile ianze kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwenye sheria tuliyopitisha tuli-debate sana kuhusu kutumia  
neno fidia na tulikubaliana kwamba neno kifuta machozi kwa binadamu na kifuta jasho  
kwa mazao liendelee kutumika kwa kuzingatia kwamba hakuna fidia inayoweza  
ikapatikana ya kuweza kufikia thamani ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa na sheria imeshapitishwa sasa hivi tupo  
kwenye hatua ya kutengeneza Kanuni, tunategemea ifikapo mwezi Oktoba, 2009 Kanuni  
nne za msingi zitakuwa zimekamilika na kwa sababu tunategemea kutengeneza Kanuni  
nane zikiwemo tatu ambazo zipo sasa hivi na zingine tano za nyongeza ili sheria iweze  
kutumika, kwa hiyo tunafikiri kuanzia mwezi Oktoba Kanuni nne za msingi zitakuwa  
zimekamilika na hapo tunaweza kwamba sheria inaweza ikaanza kutumika. Tunategemea  
mwaka huu tunaweza tukaanza kutumia sheria hiyo.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa  
kuniona.

Kwa kuwa wanyamapor hawa waliozungumziwa katika swali la msingi huko  
katika Kata ya Sengenya na Nangoma ni sawa na wale wanaosumbua katika Wilaya ya  
Rombo na Siha, Mkoani Kilimanjaro na kwa kuwa ni muda mrefu sasa tumekuwa  
tukielezwa hapa Bungeni kwamba askari wa wanyama pori watawekewa vituo katika  
maeneo hayo ili kunusuru hali hiyo.

Je, Naibu Waziri anaweza kutueleza sasa ni lini zoezi hilo litakamilika ili  
wananchi wa maeneo hayo waweze kufanya kilimo chao bila usumbufu wa wanyama  
hawa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shally Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeanza kujenga vituo kwenye maeneo mbalimbali ili askari wetu waweze kukaa jirani na hifadhi na hivyo kuweza kutoa msaada wa haraka unapohitajika. Kwa mwaka huu wa fedha unaoisha tayari tunaendelea na ujenzi kituo cha Rombo, lakini katika mwaka ujao wa fedha tunategemea kujenga vituo vingine kwenye maeneo ya Longido, Simanjiro, Karagwe, Kahama na Nanyumbu. Kwa hivyo tutaendelea kufanya hivyo na ninaamini azma hii itaweza kufikiwa kama ambavyo tumepanga.

Na. 55

### **Kuongeza Ulinzi wa Maliasili**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni dhahiri kuwa hivi sasa Serikali imeelewa katika ulinzi wa maliasili kama vile wanyamapori, miti ya mbao, miti ya dawa, magogo na hata misitu ya kupandwa ambayo uhujumiwa na majangili:-

(a)Je, si wakati muafaka Wizara ya husika ikapewa kibali cha kuongeza maofisa wa kuhifadhi maliasili yetu iliyobaki ili isiteketee?

(b)Je, kwa nini Serikali isifanye *surveillance* kwa familia na watu wote wanaojulikana na jamii kujihusisha na uwindaji haramu unaomaliza wanyama?

(c)Je, kwa nini Serikali isiwawajibishe maafisa Maliasili katika Wilaya zetu wasiowajibika ipasavyo na kushirikiana na majangili?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) (b) na ( c ), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli Wizara yangu inakabiliwa na changamoto nyingi Katika ulinzi, uhifadhi na matumizi endelevu ya raslimali ya misitu na wanyamapori zinazotishia uwepo wa raslimali hii muhimu nchini. Baadhi ya changamoto hizo, ni pamoa na upungufu wa watumishi, hasa walinzi wa misitu, maafisa wanyapori, pamoa na wahifadhi wanyama pori.

Aidha changamoto nyingine ni uwepo wa watumishi wenye umri mkubwa (karibu kustaafu) hasa katika sekta ya Misitu na wanyamapori, uhaba wa vitendea kazi,

miundombinu hafifu na kukiukwa kwa maadili ya kitaaluma (*Code of Ethics*) ambayo ni msingi wa kusimamia Maliasili hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa watumishi, Serikali imeajiri watumishi 299 katika sekta ndogo za wanyamapori na misitu katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Aidha, Serikali iko kwenye mchakato wa kuangalia uwezekano wa kuajiri na kukidhi mahitaji kwa masharti nafuu bila kuathiri matarajio ya Serikali ya kuwa na watumishi wenye sifa zitakazotakiwa katika utumishi wa umma kwa kupendekeza ajira ifanyike kwa wananchi wenye elimu ya darasa la saba ambao wamepitia mafunzo ya JKT. (*Makofii*)

Ndiyo maana sisi kama Wizara tumefurahi, kwamba wazo la kuanzisha JKT sasa linandelea vizuri. Sanjari na mkakati huu Wizara itaendelea kuzishauri Halmashauri kuajiri wahifadhi wanyamapori ili kusaidia kuimarisha ulinzi wa maliasili katika maeneo yenye raslimali za misitu na wanyamapori wengi.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya *Surveillance* ya kiintelijensia katika maeneo yanayozunguka hifadhi za wanyamapori na kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu watu wanaofanya uhalifu dhidi ya wanyamapori na mazingira. Taarifa hizo za kiintelijensia hutumika kuwanasa majangili kupitia doria za kawaida na operesheni mbalimbali zinazofanywa ndani na nje ya maeneo yaaliyohifadhiwa.

Naomba kuchukua fursa hii kuwahamasisha wananchi kuendelea na kusaidia Serikali kwa kutoa taarifa za uhalifu wa maliasili zetu. Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano kwao. Aidha katika kuboresha utendaji kazi za intelejensia Wizara imekuwa inawagharamia watumishi wa ngazi mbalimbali kujifunza mafunzo ya intelejensia katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

(c) Mheshimiwa Spika, Watumishi wasio waaminifu, Wilayani hushughulikiwa na mamlaka zilizowaajiri kwa kufuata taratibu na Kanuni za ajira zao. Aidha, katika kukabiliana na tatizo la watumishi wasio waaminifu, Wizara yangu inakusudia kuanzisha Baraza la Maadili la kitaaluma katika sekta ya misitu na wanyamapori ambalo pamoja na taratibu za kiutumishi, watumishi ambao si waaminifu watashughulikiwa na baraza kwa mujibu wa taaluma zao.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursahii ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kwanza niwashukuru Wizara, baada ya kwenda kueleza matatizo ya maliasili katika Wilaya yangu, wametumwa maafisa kutoka Wizarani wakaja wakatembelea. Nashukuru kwa hilo, lakini sidhani kama waliyaona yote. Sasa, swali langu la kwanza:-

(i) Mheshimiwa Spika, katika pori la akiba la Lwafi, ambalo liko katika Wilaya ya Ikasi na Jimbo langu la Kalambo, pamoja na pori la misitu la Kalambo. Wanyama waliokuwemo, wamemalizika. Kwa sababu ya uwindaji haramu, pamoja na uharibifu wa

msitu. Lakini pia lipo pori la akiba katika bonde la ziwa Rukwa, hili lenyewe limekwisha. Kwa sababu watu wamewinda wamemaliza wanyama na wafugaji wamehamia katika pori hilo, kwa sababu afisa wanyamapori ndiye anayeruhusu mambo haya yafanyike na tumelalamika lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Je, Serikali itachukua hatua gani ili kuhakikisha hayo hayatokei?

(ii) Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri, watumishi ni wachache na mapori haya kwetu yameharibika kwa sababu ya urasimu ya kuwachukulia hatua hawa maafisa ambao wanahusika na uharibifu zinachukua urasimu mkubwa sana kiasi ambacho hakuna hatua yeote zinazofanyika, na wananchi wanaamua na wao kuingia katika, kuharibu kwa sababu wanaolinda wanaharibu.

Je, Serikali itachukua hatua gani za haraka kuwachukulia hatua kali, au kuwafukuza, au kuwahamisha wale maafisa ambao wameshiriki katika kuharibu maliasili katika Mkoa wetu wa Rukwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya mheshimiwa Ludovick Mwanzila, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Mwananzila, kwa kweli, kwa kuonyesha uchungu mkubwa katika uharibifu na utoroshaji au ujangili unaofanywa kwenye rasilimali zetu.

Ni kweli tatizo ni kubwa, na ndio maana dhamira ya Serikali, kupitia Wizara yangu ni kufanya mapinduzi makubwa, kwenye tasnia ya wanyamapori na misitu. Ni kweli tatizo la uhaba wa watumishi ni kubwa sana. Kwa mfano, idara ya wanyamapori, kwa mapori tuliyonayo, tunaitaji wafanyakazi wanaofikia 4199. Tulionao sasa hivi ni 1199.

Kwa hiyo, tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 3000. ndio maana tukasema tukianzisha mamlaka ya wanyamapori, pengine itakuwa ni rahisi zaidi kuweza kuajiri na kwa maana hiyo tutaweza kuyalinda mapori yetu kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Spika, kadhalika kwa upande wa misitu nako tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi, tunahitaji maafisa angalau 500 zaidi ya wale tuliyonao. Lakini pia hatuna afisa, au tuseme askari wa ulinzi wa misitu au tuseme *Forest Guards* hata mmoja na kwa misitu yetu na kwa mazingira tuliyo nayo na changamoto, tunahitaji angalau askari wa misitu yaani *Forest Guards* 2600. Kwa hiyo, tunafanya mazungumzo katika Serikali, kuweza kupata namna ya kupata askari hawa. Mazungumzo yanaendelea vizuri na ninaamini kwamba tutafikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swala la uadilifu ambalo linahusisha pia swali la pili alilouliza. Hili ni tatizo la kawaida la kitumishi na hatua zimekuwa zikichukuliwa kila tunapokuwa tumebani watu wenye matatizo.

Katika miaka mitatu iliyopita, kuna watumishi zaidi ya 24 ambaao idara ya misitu na idara ya wanyama pori zimewachukulia hatua, wakiwemo watatu walioachishwa kazi kutokana na matendo ya utovu wa uadilifu.

Kwa hiyo, tutaendelea kuchukua hatua kila tunapoona kuna matatizo ya namna hiyo. (*Makofî*)

Na. 56

### **Kupeleka Umeme - Vijiji vya Kwimba**

**MHE. BUJIKU P. SAKILA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali kupitia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, mwaka 2008/2009 iliahidi kupeleka umeme kwenye vijiji vya Hungumalwa, Ilala, Kawekamo, Bupamwa, Sangu, Kikubiji Shilima, Nyamilama na jineri mbili za pamba za Mwalujo na Sangu kwenye Jimbo la Kwimba; na kwa kuwa zoezi la kusambaza umeme kwenye vijiji hivyo ilikuwa litanguliwe na ujenzi wa kituo cha kupoozea umeme katika kijiji cha Mabuki wilayani Misungwi:-

- (a) Je, miradi hiyo miwili, yaani ujenzi wa kituo cha Mabuki na ile ya kusambaza umeme kwenye vijiji vilivyotajwa hapo juu imefikia hatua gani ya utekelezaji?
- (b) Pindi kituo cha kupoozea umeme cha Mabuki kikikamilika kitawezza kuunganishwa na njia ya umeme iendayo Ndugu ili kuongeza na kuimarisha umeme katika mji huo ambaao ndiyo Makao Makuu Kwimba?
- (c) Kama fedha kwa ajili ya mradi huo umeshapatikana.Je, ni hatua zipi zinazochelewesha utekelezaji wa miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bujiku Philip sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakati tukijibu swala hapa Bungeni tarehe 31 julai, 2007, na katika hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2008/2009, Serikali iliahidi kupeleka umeme katika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge.

Maeneo aliyyoyataja Mheshimiwa Mbunge yanatarajiwa kupatiwa umeme kwenye mradi ujulikanao kama *Electricity V unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB)*. *Africa Development Bank (ADB)* watafadhilli ujenzi wa njia ya umeme wakati ujenzi wa kituo cha kusambaza umeme cha Mabuki utagharamiwa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, zabuni ya ujenzi wa kituo kikuu cha kupozea umeme cha Mabuki katika Wilaya ya Misungwi chenye ukubwa wa *15MVA* kwa msongo wa *220/33KV* ilitangazwa tangu tarehe 13 machi 2009 na wakandarasi kadhaa walioonyesha nia ya kushiriki kwenye zabuni hiyo. Walitembelea eneo hilo tangu mwezi Machi, 2009 kwa lengo la kuhakiki gharama na hivyo kutoa makadiriko ya ujenzi ya wakati huu.

Mheshimiwa Spika, mkandarasi anatarajiwa kupatikana kipindi cha Mwezi juni, 2009 ambapo idadi kamili ya wakandarasi walioonyesha nia ya kushiriki itafahamika baada ya zabuni kufunguliwa tarehe 19 Juni, 2009, hapo awali zabuni ilipangwa kufunguliwa tarehe 8 Juni, 2009. Kituo hicho kinajengwa kwa Bajeti ya *TANESCO*. Awamu ya kwanza, kiasi cha shilingi bilioni tatu (Tsh 3 bn.) kimetengwa katika Bajeti ya ujenzi ya mwaka 2009 ya Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kazi hii. Kazi ya ujenzi, inajumuisha uletaji wa vifaa, ikiwa ni pamoja na *transforma*, ujenzi, usimamizi hadi kukabidhi kazi iliyokamilika. Kazi hii inatarajiwa kuchukua muda usiopungua miezi 16 tangu Mkandarasi kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa njia za umeme (*feeders*) kutokea kituo hicho kwa ajili ya kusambazia umeme, itafanywa na mkandarasi wa mradi atakayepatikana chini ya ufadhiliwa *African Development Bank*. Zoezi linaloendelea kwa sasa ni mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi wa mradi, ambaye ye ye atafanya maandalizi na taratibu za kumpata mkandarasi wa mradi. Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bijiku Philip Sakila, Mbunge wa Kwimba, lenye sehemu (a) ,(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa kituo cha kupoozea umeme cha Mabuki, upo katika hatua za ununuzi na urejeshaji wa zabuni (*bidding process*) ya kumpata mkandarasi, wakati mradi wa kusambaza umeme upo katika hatua ya kumpata mshauri mwelekezi.

(b) Mheshimiwa Spika, pindi kituo cha kupoozea umeme cha Mabuki kikikamilika marekebisho/mabadiliko kadhaaa yatafanyika ili kuongeza na kuimarisha nguvu ya umeme katika maeneo yenye umeme hafifu, yanayotarajiwa kufikiwa na umeme kutoka kwenye kituo hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wowote ule, hauna budi kuitia michakato mbalimbali kulingana na taratibu za manunuzi (*Procurement Regulations*). Michakato hiyo ni pamoja na kuandaa zabuni, kutangaza zabuni, ununuzi na urejeshwaji wa zabuni na kadhalika. Hivyo, michakato ya utekelezaji wa hatua hizi ichukuliwe kuwa ni sehemu ya utekelezaji wa mradi. Mara nyingi wakati wa kufanya kazi hizi, kutegemeana na ukubwa wa mradi hukuchukua muda mrefu na nyakati zingine kwa kuwa sio kazi zinazojidhihirisha kwenye eneo la kazi, hazichukuliwi kama ni sehemu ya lazima ya utekelezaji wa mradi. (*Makofi*)

**MHE. BUJIIKA P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mrefu sana na mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ambayo yanajitahidi kupiga chenga hoja msingi, naomba kuuliza maswali mawili. (*Makofi*)

(i) Mategemeo ya wananchi katika vijiji nilivyovitaja, ni kupata umeme. Na kila mradi, una mpango kazi. Kwa mujibu wa mpango kazi wa mradi huu, mradi huu ulitakiwa kuanza lini na kumalizika lini?

(ii) Nilanza kuomba umeme tangu 1996, mwaka jana, kauli ya Serikali ikatolewa kwamba vijiji hivi, vingeanza kupatiwa umeme. Kuna kipindi niliomba, Waziri wa Nishati na Madini aje afanye ziara katika Jimbo langu usiku. Hakuja usiku akaja mchana. Sasa naomba kuuliza. Sasa hivi atakuwa tayari kuja usiku afanye mkutano Hungumarwa, Ilula, Mwamashinba na Shirimba ili haya maelezo aliyoyatoa hapa, aweze kuwaeleza wananchi, aone kama wataweza kumwelewa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bujiku Sakila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakati wa majibu yangu, katika swal la msingi, nimesema kwamba, kuna hatua zilizokwisha kufikiwa kwenye mradi wa *Electricity Five*, chini ya ufadhili wa *African Development Bank (ADB)*. Utakaohusisha miradi ya ujenzi wa kilovoti 33 na 11.

Wakati Serikali imetoa ahadi tarehe 31 Julai, 2007 mradi huu ulikuwa unatarajiwa ufanyike chini ya ufadhili wa Serikali ya Hispania. Nadhani kwa bahati mbaya, ufadhili huu haukuja.

Kwa hiyo mwaka jana wakati Serikali inawasilisha utekelezaji wa mradi huu, tukawa tena tumeomba ufadhili huo upitie *African Development Bank (ADB)*, kwa awamu ya usambazaji umeme. Lakini kwa kituo cha Mabuki, ambacho ndicho kitapokea umeme kutoka kituo cha Nyakato Mwanza kuja pale.

Mheshimiwa Spika, kituo hicho kitajengwa na *TANESCO* na tayari *TANESCO* wameshatenga milioni 3 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Ameuliza mradi utaanza lini. Mradi huo ni mkubwa, una gharimu bilioni 9 na utekelezaji wake utachukua miezi karibu 16 hadi 18. Kwa hi, matarajio ni kwamba baadhi ya utekelezaji wa mradi huu, utafanyika mwaka huu wa fedha na utakao kamilisha mradi huo, utafanyika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swal la nyongeza la kufanya ziara usiku au mchana. Mimi naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tu kwamba, mwaka jana tulifanya ziara. Mimi mwenyewe binafsi nilikwenda Wilaya ya Kwimba. Kwa bahati mbaya sikufika kwenye maeneo yake, nilifika kwenye maeneo ya Jimbo la Sumve. Lakini naomba nimwahidi kwamba tutafanya ziara sio tu ya usiku au mchana, tutafanya ziara ya usiku na mchana. (*Makofii*)

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa vile Naibu Waziri mwenyewe amesema kwamba alitembelea Jimbo la Sumve, hasa katika kijiji cha Mallya, tukafanya mkutano mkubwa sana pale na

akaahidi kwamba ndani ya miezi mitatu, kijiji cha Mallya kitakuwa kimepata umeme. Je, ahadi hiyo sasa iko wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Richard Ndassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulipokwenda Mallya, katikati ya mwezi wa kumi, kwa sababu mradi pale wa umeme wa kufikisha mradi Mallya, umeishia kijiji kinachoitwa Lyoma. Na pale si mbali. Tulikuwa tumetarajia kwamba mradi mzima ule, unakadiria kutumia kama milioni 700. Sasa tulikuwa tumesema kwamba, kama tungepata *allocation* hiyo ya Bajeti, kwa kiwango kidogo, tungeweza kutoa umeme ule kutoka Lyoma mpaka Mallya ambako nadhani ni kama kilomita 10 hivi. Halafu baadaye kikaja kile kipande cha kusambaza umeme Mallya, ambapo pana gereza, Chuo cha Michezo Mallya, Chuo cha Ustawi wa Jamii pamoja na Reli ya Kati inapita hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo yote hayo yanakadiria kufikiwa na umeme. Lakini tukasema, hatua ya kwanza, tufikishe umeme Mallya. Kwa bahati mbaya, upatikanaji wa fedha umekuwa umechelewa kidogo. Kwa hiyo na sisi tunatarajia tutakapo pata *allocation* hiyo kama ilivyopangwa na sisi katika utaratibu wa utekelezaji wa huo mradi utaendelea japo kwa awamu hivyo kama tulivyo ahidi tulipokuwa kwenye ziara hapo Mallya. (*Makofi*)

**SPIKA:** Bado Wizara hiyo hiyo, Swal ambalo lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Benson Mpesa.

Na. 57

### Kupeleka Umeme Tarafa ya Isangati

**MHE. BENSON M. MPESYA (K.n.y. MHE. MCHUNGAJI LUCKSON MWANJALE)** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa ni takriban miaka kumi (10) imepita, Serikali haijapeleka umeme Tarafa ya Isangati – Mbeya Vijijini, ingawa nguzo zimewekwa:-

Je, ni lini umeme utapelekwa Santilya, Jojo, Ilembo, Isuto na maeneo mengine kwenye Tarafa hiyo?

### WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa spika, mradi wa usambazaji umeme Mbeya Vijijini ulianza mapema mwaka 2000 na ulijumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 kuitia Mbalizi, Izumbwe, Horongo, Santilya, Illembu na Iwinji yenyе urefu wa kilometra 44.

Hata hivyo, kutokana na ukosefu wa fedha mradi huo ulisimama mwaka 2003. Kazi zilizokuwa zimefanyika kabla ya kusimama mradi huo ni:-

- (i) Ujenzi wa njia ya umeme ya Mbalizi ahadi Izumbwe yenyе urefu wa kilomita tano na ufungaji wa *transforma* katika kijiji cha Izumbwe.
- (ii) Usimikaji wa nguzo kutoka Izumbwe hadi Santilya ukiwa na urefu wa kilomita 34.
- (iii) Usimikaji wa nguzo kutoka Izumbwe hadi Horongo, umbala wa kilomita 6.

Mheshimiwa Spika, mradi huo umejumuishwa katika miradi itakayotekelezwa chini ya ufadhili wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*).

Utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge umekwishaanza kwa kuandaliwa zabuni ya kumpata mkandarasi wa mradi, ambapo maandalizi yanatarajiwa kufanyika tarehe 29 Mei, 2009, na kikao cha Bodi ya Zabuni hiyo inatarajiwa kufanyika tarehe 25 Juni, 2009, na kikao cha Bodi ya Zabuni hiyo kinatarajiwa kufanyika tarehe 25 Juni, 2009. Aidha, kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Novemba, 2009. (*Makofî*)

Mheshimiwa spika, kwa maeleo yangu ya hapo awali, ni dhahiri mradi huu ni mradi ambao utekelezaji wake umechukua muda mrefu.

Kwa bahati mbaya miradi mingi katika kipindi hiki ilikumbwa na ucheleweshaji na kukosa ufanisi kwa sababu mbali mbali ikiwemo ile ya kusimama kwa maamuzi ya kubinafsisha shirika kwa muda mrefu, migogoro ya utaratibu wa uendeshaji na kadhalika.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu kwa kushirikiana na *REA*, na uongozi wa Wilaya ya Mbeya, tutafanya kila linalowezekana ili ukamilishaji wa mradi huu ulionza muda mrefu sana, uanze kupata utekelezaji mwaka huu wa fedha kama tulivyoahidi.

**MHE. BENSON M. MPESSYA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

- (i) Kwa kuwa, kama tulivyosema kwamba swali hili ni nyeti sana na ni takriban miaka kumi hajatekelezwa, na kwasababu nguzo zimeishia Izumbwe, lakini umbali wa

kutoka Izumbwe kwenda Isangati ni mkubwa zaidi kuliko Igogwe ambako kuna umeme wa gridi. Igogwe kwenda Isangati ingekuwa ni jirani zaidi. Je, Serikali itakuwa tayari kuiangalia na hii *option* ya pili, ili kupunguza gharama za kuchukua umeme kutoka maeneo ya Igogwe kuteta Isangati, halafu iendele kwenda Iwinji. Serikali itakuwa tayari na kuangalia *option* hii ya pili?

(ii) Swali la pili, kwa kuwa wananchi wa Ilungu na Tembela, kwa muda mrefu wamesuka nyaya nyumba zao kwa maadalizi ya umeme.

Je, ni lini watafikishiwa umeme huo watu wa Ilungu na Tembela? (*Makofit*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, Swali la Mchungaji linaulizwa na Askofu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Benson Mpesa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwenye maelezo yangu ya msingi nimekiri kwamba mradi huu umeanza mwaka 2000 na hii ni 2009 na utekelezaji wake umesuasua na matatizo yaliyokuwa yanachelewesha utekelezaji wa mradi huo nimeyaainisha. Mradi huu utatekelezwa na *REA* kama ulivyokuwa umechorwa mwaka huo wa 2000 kwa maana ya utaratibu huu nilioueleza.

Lakini huu ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge, wa kuchukua umeme wa gridi kuupeleka Igogwe, halafu kutoka Igogwe utokee Isangati, Iwinji na kadhalika, uende kwenye maeneo hayo. Mimi nadhani huu ni ushauri ambaa unafaa kutazamwa, na hivyo namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nitawapelekea wataalamu wa *TANESCO* na wataalam wengine, wao waangalie na waangalie kwa kulinganisha na utekelezaji wa mradi kama ulivyopangwa awali kuona kama kuna unaifuu sio tu wa gharama lakini pia wa haraka kwa sababu mradi huu tayari umeshachelewa sana.

Mheshimiwa Spika, mradi huu kwa sasa hivi kama ulivyopangwa kutekelezwa, tayari *REA* wameshakadiria pesa kisasi cha shilingi milioni 250, kwa ajili ya kuanza kazi ya *design* ya mradi huo na kadhalika. Kwa hiyo, utekelezaji wa mradi kwa vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge, utategemeana na utekelezaji wa awali kwa jinsi kazi walivyozipanga *REA*. Lakini mimi naamini kwamba tutaanza utekelezaji wa mradi huo kwa mwaka huu na nitakuwa nawasiliana naye na kushauriana naye na kumpa *up to date information* ya mradi huo unatekelezwaje na unaendaje, ili apate kuwaeleza wananchi wake.

**MHE. NURU AWADHI BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika ahsante, kwa kuwa tatizo lililopo Tarafa ya Isangati Mbeya Vijijini, ni sawasawa na tatizo lililopo katika kitongoji cha Kipumbwi Mtoni, kijiji cha Kipumbwi, Wilaya ya Pangani.

Wakati Mheshimiwa Waziri akijibu swal la Mheshimiwa Riziki Omar Juma Mwaka 2007 na Mwaka 2008, aliahidi kwamba angewapelekeea umeme wananchi hawa ambao tayari walikwischachangia kuleta nguzo mpaka kwenye kituo cha afya. Waziri atuambie ni lini atawapelekeea *transforma* watu hawa ili wanufaika na umeme huo? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Nishati na Madini, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Nuru Bafadhili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, amesema tatizo la Wilaya ya Pangani linafanana na Wilaya ya Mbeya Vijijini. Kusema ukweli hazifanani. Kwa sababu tatizo la Wilaya ya Pangani ni kwamba wao wanapata umeme kutoka vituo vya Hale na kituo cha Hale sasa hivi kinakumbwa na matatizo ya *hydrology* kwa maana ya upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, umeme unaopatikana kituo cha Hale kidogo ni mdogo.

Lakini hata hivyo, kwa kuwa ahadi ilikuwa ni ahadi ya *transforma*, Mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha tumeainisha kupata utekelezaji wa maeneo yale ambayo *transforma* zikienda sio tu kwamba tunapeleka huduma ya umeme lakini huduma hiyo pia inaboresha shughuli za kiuchumi. Kwa hiyo ni maeneo ambayo tunayafikiria na mimi nakupa ahadi kwamba tutalifanya kazi na tutakupa taarifa. (*Makofii*)

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Mbeya vijijini linafanana na tatizo la Wilaya ya Uyui, katika Kata ya Bukumbi, Isikizya, Igalula, Goweko. Je, Serikali inasema nini kupeleka umeme katika Wilaya ya Uyui ili kuarakisha maendeleo ya Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Mchemba, Mbungewa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kutofautiana tena na Mheshimiwa Mwanne, kwa sababu kupeleka umeme Uyui si sawa na kupeleka umeme Mbeya Vijijini, Matatizo yanafanana kwa sababu umeme unakuwa haujaenda lakini namna ya utekelezaji ya hiyo ahadi, inakuwa kidogo tofauti.

Lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mwanne Mchemba, kwamba Serikali imeshatoa ahadi ya kupeleka umeme Uyui. Kwanza kwa kuanzia kwenye Makao Makuu ya Wilaya, halafu kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo lililotukumba mwaka huu kusema ukweli ni tatizo la upatikanaji wa fedha na namna ambavyo fedha hizo zilikuwa zikipatikana.

Lakini utekelezaji wa mradi huo bado unaendelea, haswa kwa kuzingatia kwamba tayari mradi huo umepasishwa kwa kuzingatia umuhimu kwa shughuli za uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. (*Makofit*)

Na. 58

### **Uzalishaji wa Mboga za Asili Nchini**

**MHE JANET B. KAHAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mboga za majani ni chakula bora katika mwili wa binaadamu na wanyama na kwamba kuna mboga nyingi zinazolimwa hapa nchini ikiwa ni pamoja na mchicha, *spinach* za Kichina na mboga za kizungu kama vile *carrot*:-

- (a) Je, Serikali itahamasisha lini wananchi ili watumie zaidi mboga za asili kama vile mboga za mgagani, magimbi, mlenda, mnafu, kisamvu na kadhalika?
- (b) Je, Serikali haioni kuwa, kuna umuhimu wa kuzalisha mbegu hizi zaidi na kuzitawanya nchi nzima ili hatimaye ziweze kuuzwa hata nchi za nje kama vile nchi ya China inavyouza mboga zake Barani Amerika na kwingineko?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inahamasisha matumiza ya mboga za asili kwa kufanya utafiti wa mboga za asili na kuzalisha mbegu za mboga hizo.

Aidha wakulima wanashirikiswa katika kuzalisha mbegu kwa ajili ya kuwauzia wakulima wengine. Ili kuendeleza utafiti wa aina za mboga za asili, kituo cha Taifa cha kutunza Vinasaba (*Tanzania Plant Genetic Resource Centre (TPGRC)*) kilichopo Arusha, kinakusanya vinasaba vyta aina mbalimbali za mboga za asili wakati kituo cha Utafiti wa mazao ya bustani cha Tengeru na Kituo cha Utafiti cha *World Vegetable Centre* vinashirikiana katika, utafiti wa mbegu za mboga za asili kama vile mnnavu, ngogwe (nyanya chungu), tege na mgagani.

Aidha vituo hivyo hutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam wa kilimo kutoka Halmashauri mbalimbali za Wilaya kuhusu namna ya kuongeza tija, uzalishaji na matumizi ya mboga za asili.

- (b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuhusu umuhimu wa kuzalisha mbegu bora za mboga za asili kwa ajili ya matumizi ya humu nchini na kuuza nje ya nchi.

Kwa sasa wakala wa mbegu za kilimo, yaani *Agriculturals Seed Agency (ASA)*, kwa kushirikiana na makampuni binafsi kama vile *Alfa Seed* wanaendelea kuzalisha mbegu mbalimbali zikiwemo mbegu za mboga za asili katika kituo cha Tengeru Arusha ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa mboga hizo unakuwepo.

Aidha kati ya mwaka 2002 hadi 2008 Serikali ilitekeleza mpango wa kuimarisha sekta ya kilimo uliofahamika kama *Agricultural Sector Program Support, ASPS*, ambao umewajengea wakulima wadogo uwezo wa kuzalisha mbegu za daraja la kuazimiwa, yaani *QDS* za aina mbalimbali. Mpango huo pia umetoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu bora yaliyotolewa kwa wataalamu wa ugani na wakulima kwa kutumia mbinu shirikishi na mashamba ya mfano. Jumla ya wilaya 18 zilitekeleza programu hii.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa, nina maswali mawili ya nyongeza. Vipo vitengo vya biashara katika maofisi yetu ya ubalozi katika nchi mbalimbali. Je, ofisi hizo zimeshafanya au zina utaratibu gani wa kutafuta masoko kwa ajili ya mazao yanayozalishwa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, la pili ni ningelitaka kujua. Je, kuna mazao ya aina gani yanayouzwa katika nchi ambazo wanunu mazao kama vile matunda na mboga kutoka katika nchi yetu ya Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Janet Kahama, kama ifuatavyo. Swali la kwanza ni kwamba vituo vyetu ambavyo viko nje, kwa mfano kilichopo Uingereza na Dubai, vituo hivi ukifika kwenye ofisi zao unakuta mazao mbalimbali ama kwa picha ama kwa mfano kwa kahawa unakuta kahawa za aina mbalimbali wamezi-*display* pale na wanatumia *sample* hizo kwa ajili yak *u-advertise* mazao yetu tuliyonayo hapa Tanzania. Na ni balozi zote, ukienda nchi mbalimbali kwenye balozi zetu utakuta mazao yetu ambayo tunayalima wameyaweka ama kwenye picha ama mazao kamili yako pale na nchi mbalimbali zikifika pale zinayaona.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ni mazao gani ambayo yanauzwa nje ni kwamba sasa hivi kuna ndege ambayo inakuja nadhani ni mara moja au mara mbili kwa wiki kutoka Kilimanjaro na inakwenda mpaka Nairobi kuchukua mazao ya bustani, ya mboga mboga, yanapelekwa nchi za ulaya na Uarabuni.

Kwa hiyo, zoezi hilo limeanza, ila kwa sasa hivi tunahamasisha uzalishaji zaidi kwasababu kama uzalishaji utaongezeka na hivi tunavyojenga uwanja wa ndege wa Songwe kuna uwezekano mkubwa wa ndege hiyo ikachukua mboga mboga hizo kutoka Mbeya na Nyanda za Juu Kusini ikamalizia Kilimanjaro. Kwa hiyo ndege ile ikawa imeja kwa mboga za Tanzania peke yake badala ya kwenda Kenya.

Na. 59

**Kuendeleza Kilimo cha Zao la Mkonge**

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la Mkonge hulimwa sana na wakulima wadogo na wa kati katika mkoa wa Tanga hususan wilayani Korogwe na kwamba lipo lengo thabiti la kukuza zao hilo:-

- (a) Je, Serikali inasemaje kuhusu kuanzisha mfuko maalum wa mikopo ya zana na pembejeo kwa ajili ya wakulima hawa?
- (b) Je, ni lini wakulima hawa watapatiwa hati ndogo ya kumiliki ardhi (*sub-lease*) kutoka Bodi ya Mkonge (*Tanzania Sisal Board*) kama wanavyoahidi kila mara ili waweze kutumia kuombea mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa *Eng.* Laus Omar Mhina, Mbunge wa Korogwe Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika mchakato wa kuanziasha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kuhudumia wadau wote wa kilimo. Benki hii itawahudumia wakulima wa aina zote, wakiwemo wakulima wadogo wa mkonge kwa kuwapa mikopo ya pembejeo kama vile mbolea, dawa za wadudu, magugu na mbegu bora na zana za kilimo kama matrekta, vipandio, na kadhalika. Aidha Bodi ya Mkonge kwa kushirikiana na wadau wa Mkonge inakamilisha mchakato wa kuanzisha *Sisal Industry Trust Fund* ambayo itawahudumia wakulima wote katika kuendeleza zao la mkonge ikiwa ni pamoja na kushughulikia upatikanaji wa mbolea na pembejeo zitakazohitajika.

(b)Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa hati miliki, Bodi ya Mkonge Tanzania iliomba fedha kupitia iliyokuwa *PSRC* na baadaye *Consolidated Holding Corporation* ili kupima mashamba na kuweza kutengeneza Hati Miliki, lakini bado fedha hizo hazijapatikana. Kutokana na hali hiyo Bodi ya Monge Tanzania itatenga shilingi milioni 50 kutoka fedha za bajeti ya 2009/2010 ili kazi hii ifanyike. Pamoja na fedha hizo za Serikali, Bodi ya Mkonge inawahamasisha baadhi ya wakulima wanaoweza kugharamia kazi hii kufanya hivyo, ili Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi iweze kutoa *sub-lease*.

**MHE. ENG. LAUS O. MHINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuzingatia ushauri wa Bodi ya Mkonge kushughulikia hati hizi miliki.

Je, Bodi hii haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwapatia japokuwa barua wakulima hawa wadogo wadogo ili waweze kuzitumia katika ku-*process* hati hizi miliki?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Eng. Laus Omari Mhina, Injinia Mbunge wa Korogwe vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wazo lake ni zuri kama kuna uwezekano tutawasiliana na Bodi ya Mkonge. Kisheria kama kuna uwezekano basi watapatiwa barua ili waweze kuanza ku-process hati miliki hizo.

Na. 60

### **Chombo cha Kuhakiki Hukumu Zinazotolewa Na Majaji/Mahakama**

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mahakama na Majaji ni wanadamu kama wengine na katika kutoa hukumu ya kesi wanaweza pia wakakosea kwa namna moja au nyingine:-

(c)Je, ni chombo gani kilichowekwa kisheria/kiutaratibu ambacho kinapitia kesi mbalimbali kuona kama hukumu zinazotolewa na Mahakimu hao ni sahihi?

(d)Kama chombo hicho kipo. Je, inapotokea mshtakiwa amehukumiwa isivyo haki, ni sheria gani inayombana Jaji/Hakimu aliyeamua kesi hiyo. Je, mshatakiwa anafidiwaje?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Kheri Khatibu Ameir, Mbunge wa Matembwe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(c)Mheshimiwa Spika, utaratibu umewekwa na sheria mbalimbali ili kuona kwamba hukumu zinazotolewa na Mahakama kupitia Majaji na Mahakimu ni sahihi. Hukumu zinazotolewa huweza kusahihishwa na Mahakama ya Juu ili kuhakikisha kwamba hukumu na mwenendo mzima wa kesi ni sahihi, halali na umefuata taratibu zilizowekwa na sheria.

Njia zinazotumika ni kama vile kuomba Rufani ya kesi, yaani *Appeal* kwa Mahakama ya Juu na pili ni kuomba hukumu kufanyiwa masahihisho, *Revision* na tatu ni kwa kuomba hukumu kufanyiwa mapitio, yaani *Review*. Hii ni njia ambayo Mahakama husika imepewa mamlaka ya kupitia baadhi ya maamuzi yake yenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya kuchukua hatua hizo yametolewa chini ya vifungu vya 20, 21 na 43 vya Sheria ya Mahakama za Mahakimu, yaani *The magistrates' Courts Act, Chapter 11 Revised Edition 2002*. Aidha kiutawala Mahakama za juu na Mahakimu na majaji Wafawidhi, wana uwezo wa kuitisha majalada ya kesi ili

kujiridhisha na kuona kwamba mwenendo mzima wa mashauri na hukumu ni sahihi, halali na taratibu za kisheria zilizingatiwa.

(d)Mheshimiwa Spika, Majaji na Mahakimu wana kinga ya kisheria kutoshitakiwa kwa matendo wanayoyafanya katika kutekeleza majukumu yao ya kutekeleza sheria katika nyadhifa zao, iwapo wanapofanya hivyo, wanafanya kwa kufuata na kuzingatia misingi iliyowekwa katika kutekeleza majukumu yao. Kinga hii imetolewa na kifungu cha 66 cha Sheria ya Mahakama za Mahakimu (*The Magistrates' Courts Act*), sura ya 11.

Mheshimiwa Spika, Jaji au Hakimu huweza kuchukuliwa hatua pale inapobainika kwamba alitumia nafasi yake vibaya na kukiuka maadili ya kazi yake, pale maamuzi yake yanapokuwa hayakuzingatia miiko ya kazi na kuathiri kazi zake za Kimahakama. Mahakimu na Majaji ni lazima wazingatie maadili ya kazi zao, yaani *The Code of Conduct for Judicial Officers*.

**MHE. KHERI KHATIBU AMEIR:** Mheshimiwa Spika, Mahakama ni moja kati ya Mihimili Mitatu ya Utawala hapa nchini. Yaani kuna Bunge ukiongoza wewe, *Executive akiongoza Mheshimiwa Rais na Mahakama ikiongozwa na Jaji Mkuu*.

Mheshimiwa Spika, ni nini *role* ya Waziri wa Sheria pale ambapo Mahakama ikiwa imekiuka Katiba au Sheria ya nchi. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ameir kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kulingana na Katiba yetu Ibara ya 107 (a) Ibara ndogo ya kwanza, Mahakama ndio chombo pekee na cha mwisho cha kutoa haki katika nchi yetu. Kwa hiyo Waziri wa Katiba na Sheria hana mamlaka juu ya Mahakama ya nchi hii. (*Makofi*)

Na. 61

### **Muswada wa Sheria ya Vidhibiti Mwendo**

**MHE. IBRAHIM MUHAMAD SANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya 90 Serikali ililetta Sheria ya Vidhibiti Mwendo kwa mabasi ya abiria yanayofanya safari zake hapa nchini; na kwa kuwa, imeonekana kwamba mbali na kuitishwa Muswada wa Sheria hiyo lakini bado kiwango cha ajali kimeongezeka nchini.

Je, ni lini Serikali italeta tena Muswada wa Sheria hiyo hapa Bungeni ili ifanyiwe marekebisho au kufutwa kabisa kwa vile haujaleta mafanikio au kupunguza ajali za barabarani?

## **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 51 kifungu kidogo cha 5 cha Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya Mwaka 1973 R.E 2002 inaagiza kwamba magari yote ya abiria yanapaswa kufungwa kifaa cha kudhibiti mwendo kabla ya kuidhinishwa kufanya shughuli ya biashara ya kusafirisha abiria. Sheria hii haiyahu magari madogo ya abiria (*Taxi Cab*). Aidha kuitia Gazeti la Serikali Na. 263 la mwaka 1990 (G. N. No. 263 of 1990) la tarehe 27 Julai, 1990 Serikali pia iliagiza wamiliki wa Magari kufunga vidhibiti mwendo kwenye magari.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa Sheria na Kanuni hiyo, nikiri kwamba kumekuwa na udhaifu wa kufuatiilia utekelezaji wa sheria hiyo, nikiri kumekuwa na udhaifu wa kufuatiilia utekelezaji wa sheria hiyo hivyo kutoa mwanya kwa baadhi ya wamiliki wa mabasi au madereva wao kuviharibu vifaa hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuitia mkutano wake wa wadau wa biashara ya usafirishaji wa abiria chini ya usimamiaji wa *SUMATRA* ulifanyika mwezi Februari mwaka 2009 katika ukumbi wa *Karimjee* Serikali imeagiza magari yote ya abiria ifikapo mwaka 2009 yawe yamefungwa kifaa cha *takography* ambacho kitakuwa kinarekodi mwendo kasi wa gari kwa kipindi chote cha safari.

Kifaa hicho mara baada ya kukaguliwa kitaonesha mwendo wa mwenendo kasi wa gari kwa kipindi chote cha safari na pale itakapobainika kuwa mwendo kasi aliokuwa anakwenda dereva na kampuni husika itachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

**MHE. IBRAHIM MUHAMAD SANYA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kujibiwa vizuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, ajali za barabarani husababishwa na mambo mengi yakiwemo ya uzembe wa madereva, magari chakavu yasiyokidhi hali ya kuchukua abiria na mwendo wa kasi. Je, serikali kuitia Wizara hii, itahakikishaje kwamba inakifanyia ukaguzi kifaa hicho kipyaa cha *tekography* kila baada ya muda gani ili kujua mwenendo mzima wa mwendo wa gari husika?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Katika kipindi cha Januari – Aprili 2009, ajali za barabarani zilizotokea ni 1597 na kati ya ajali hizo watu 219 wamepoteza maisha yao. Je, kifaa hicho hakitakuwa kinachezewa tena na madereva kama ilivyofanyika katika vidhibiti mwendo ili tuweze kujua hali halisi ya utumiaji wa vifaa hivyo na kupunguza ajali nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Ibrahim Muhamad Sanya, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba hizo takwimu ambazo amezitoa kuhusu ajali na kuhusu vifo ni kweli na nilizitoa hata jana katika swali la msingi lililoulizwa. Lakini ninaomba niseme kwamba ajali inapotokea ni kweli inapata *publicity*, inatangazwa kwenye magazeti, inatangazwa kwenye luninga na kadhalika. Lakini kuna mambo ambayo hayatangazwi ambayo ni hatua zinazochukuliwa.

Kwa mfano, katika kipindi cha Januari – Machi mwaka huu, madereva 114 wamepigwa faini kwa kutoweka *reflector* zile za barabarani. Madereva 91 wamefungiwa leseni zao, katika kipindi hiki cha miezi mitatu ya mwaka huu, kwa kipindi cha miezi sita au mpaka mwaka mmoja kwamba hawawezi wakaendesha magari. Lakini pia niseme kwamba askari 30 katika jeshi letu ambao kwa kweli imebainika kwamba wamekwenda kinyume na utekelezaji wa sheria wameweza kuhamishwa na wengine wameweza kufukuzwa katika kazi. Kwa hiyo hizo shughuli zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi hichohicho kumekuwa na muongezeko wa magari. Watu wamekuwa wanunu magari mengi na kumekuwa kuna muongezeko wa pikipiki za miguu miwili, kumekuwa na muongezeko sasa wa bajaji – pikipiki na barabara ni zilezile. Kwa hiyo bado unakuta kwamba ongezeko la magari limekuwepo lakini *services* kama barabara zimekuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hiki kifaa tumesema kwamba itakuwa ni *mandatory* kuanzia Septemba mwaka huu. Itakuwa *kila gari linakuwa inspected* na tunaweka utaratibu kwamba kila mwaka kuna *mandatory inspection* ya kuhakikisha kwamba tunatizama hivi vifaa viro.

Lakini sasa zinapotokea ajali nafikiri itakuwa ni utaratibu wa kuwekwa kwamba wale ma-*traffic officers* watakuwa wanacheki yale magari barabarani wala bila kuwa na muda maalum lakini kila wanapokuwa barabarani ili kuhakikisha kwamba ule mwendo wa spidi ya lile gari unakwenda viro. Nafikiri tunajitahidi lakini maaskari pia tulionao ni wachache lakini idadi ya *service* imekuwa ni kubwa kuhusu magari na kadhalika. Lakini jitihada tunafanya na *concerns* ambazo umezitoa Mheshimiwa Mbunge, tutazizingatia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa muda umepita, maswali yamekwisha. Sasa ni matangazo; Waheshimiwa Wabunge, nawaarifu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, hayupo leo hapa Dodoma amesafiri kwenda Dar-es-Salaam kwa shughuli za kikazi na amemwachia shughuli za kuongoza shughuli za Bunge hapa kama Kiongozi wa shughuli hizo Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Waziri wa Nchi. Ingawa kama kawaida Mheshimiwa Muhammed, hapendi kukalia kitie cha Waziri Mkuu, kwahiyo amekalia kitie kile cha pili kile. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni wageni. Wapo wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustapha Mkullo, ambao ningetarajia wakae kwenye *Speaker's Gallary* lakini sijui wako wapi sasa? Bwana Juma Reli, Naibu Gavana wa

Benki Kuu, hayupo. Na Naibu mwingine Dokta Bukuku, pia hayupo. Wapo wageni 50 wa Mheshimiwa Felister Bura, ni wanafunzi wa Chuo Kikuu Cha Dodoma ambao ni Wanachama wa Umoja wa CCM, naomba wasimame.

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa, kutoka Chuo Kikuu cha Mtakatifu Johns, Dodoma ambao ni Wanachama wa *CHADEMA*, naomba wasimame. Kama kawaida hao ni wachache kuliko wale wa kwanza. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa nimearifiwa na Mheshimiwa waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005; ni marufuku kuunda matawi ya Vyama vya Siasa katika Vyuo Vikuu. Ndio maana nawatambulisha kama wanachama, nikishasema hivyo sasa wazingatie kwamba wasiunde matawi, ndio. Kwa hiyo hilo ndilo sahihisho ni wanachama wanaweza kuwa na matawi yao mjini lakini, ehee!! (*Makofi*)

Mheshimiwa Suleiman Murad Saddiq, Mbunge wa Mvomero, anaye mgeni wake Ndugu David Mwaibula. Ndugu David Mwaibula ni mtu maarufu sana huyu, yule pale. Naona amesimama na mama mmoja sijui ndio mkewe? Hapana! Karibu sana David, tunakumbuka sana mchango wako katika mambo ya *SUMATRA*, ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Matangazo ya kazi, tunalo tangazo moja tu. Kwa idhini ya Mheshimiwa Spika, nimeruhusu Kamati ya Fedha na Uchumi wafanye kikao saa 4.30. Kawaida vikao vya Kamati vinaanza saa 7.00. Lakini wenzetu hawa Kamati ya Fedha na Uchumi, wanakwenda kuuzingatia Muswada wa Fedha wa Mwaka 2009 ambao tutaufanya kazi Ijumaa siku ya kesho kutwa. Kwa hiyo nimewaruhusu wakafanye kikao. Hayo ndio matangazo. Katibu endelea na *Order Paper*.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika, Kanuni ya 68.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issa Yahya.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, tumefarijika kupata kitabu ambacho alihutubia Rais hivi juzi na tumefurahi sana kwa sababu kinatoa mwongozo mzuri kabisa. Lakini pia Rais, alikuja kuhutubia katika Bunge lako Tukufu hapo nyuma na ukatueleza kwamba tutapata nafasi ya kujadili yale ambayo aliyahutubia.

Kwa bahati hatukupata hata *hansard* au kitabu cha aina yoyote kutokana na maelezo yale na ile hotuba mpaka leo hatujajua tumefikia wapi. Kwa hivyo tunataka mwongozo wako, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Wewe unataka kufahamu tu, hakuna cha mwongozo wowote hapo. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Hotuba hiyo ya mwaka jana nadhani tarehe 21 Agosti, 2008 ilikuwa ni ndefu sana, kiasi cha saa tatu na nusu au nne hivi.

Kwa hiyo, kama ilivyo kawaida hata kwa *hansard* zetu za dakika 15 ni haki ya anayetoa mchango wowote humu ukumbini pamoja na wageni wetu mashuhuri kama Mheshimiwa Rais, kurejeshewa ile *hansard* ilivyo aweze kuangalia masuala ya uhariri. Nadhani kwa haya uliyosema sasa hivi Mheshimiwa Yahya itabidi tukumbushane tena. Mniwie radhi ilibidi Sekretarieti wafuatilie ili tuweze kupata ile hotuba rasmi, tutafuatilia, Ahsante sana. (*Makofi*)

Katibu endelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2009/2010 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2008 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2009/2010**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, bado ninao wachangiaji 24, pengine leo tutaweza kuwafikia 20, hao wanne nitashauriana tuone kama kesho asubuhi tunawenza kuwamaliza. Na nikumbushe tu kwamba kesho kuanzia pengine, nadhani itakuwa jioni nakuombeni sana Waheshimiwa Wabunge, tuwepo katika Ukumbi kwa sababu tunakamilisha upigaji kura unaohitajika Kikatiba. Nao ni wa *role call* ili kuweza kupitisha au vinginevyo Makadirio ya Bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo, kwa tangazo hili hata wale wenzetu ambao pengine walikuwa na udhuru wako Dar-es-Salaam na nini, tunaomba waje kwa sababu kesho tutapiga kura kwa kuitwa majina. Ninadhani tutaanza jioni, nitatoa nafasi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Mawaziri na kadhalika, kuweza kujibu hoja saa za asubuhi na baada ya hapo kwa mtiririko mzuri wa upigaji kura nadhani tutapiga kura kuanzia saa 11.00 jioni. Naomba tuwepo ili tukamilishe hilo.

Sasa nitawataja basi Wabunge wanenye wanaoanza, ni Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, bahati mbaya Mheshimiwa Ester Nyawazwa hayupo, ana shughuli maalum kule Mwanza. Atafuataia basi Mheshimiwa Dora Mushi, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro na Mheshimiwa Raynald Mrope, kwa mpangilio huo.

Kwa hiyo, sasa namwita Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dora Mushi, ajiandaye.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, utanisamehe sana leo kwa sababu sauti yangu siyo nzuri sana. Lakini niliona ni vizuri nichangie, leo niko vizuri zaidi kuliko jana.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nizungumze machache kuhusu Bajeti yetu. Bajeti ya serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi.

Lakini pia naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nafasi kuweza kuwa hai mpaka saa hii na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi ninapongeza serikali kwa Bajeti yake na mimi naamini yale ambayo hatutaafikiana nayo yatapata marekebisho.

Kuna Ndugu zangu, Wabunge wenzangu jana walichangia wakasema kila *direction* unayoangalia unaangalia *progress*. Yes, there is progress na hata Marekani ambako kuna Maendeleo ya Hali ya juu bado Wabunge wakienda Bungeni wanaiambia Serikali tunataka mfanye zaidi ili tuende mbele zaidi. Sisi Waheshimiwa Wabunge kazi yetu ni kusimamia na kuishauri Serikali. Kazi yetu humu ndani sio kuisifia Serikali tu, tunaisimamia na kuishauri Serikali na tunafanya hivyo ili na sisi tuendee.

Ni kwanini sisi tunaendelea kuwa *a low income country tuna resources* nyingi sana katika Taifa hili tuna kila kitu na Mwenyezi Mungu katupendelea sana kama Watanzania, Maziwa makubwa, mito mingi, ardhi nyingi kila kitu kipo. Wataalam na watu waliosoma tunao. Tunachohitaji ni kuendeleza ili wasije wakafungua maana hayo mashule yetu yasipokuwa mazuri watapungua na ndiyo maana tunasema vipaumbele vyetu vimekuwa shule.

Mheshimiwa Spika, ninakupongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wako na wataalam wote wa Wizara ya Fedha ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, yako matatizo ambayo tunayo ndani ya nchi hii na matatizo mengi tuliyo nayo ni ya menejiment, menejiment kwa maana ya kutofanya maamuzi yanayostahili katika nyanja nyingi hata pale ambapo tunaona kwamba tungeweza kufanya vizuri zaidi bado tunashindwa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sekta mbalimbali ambazo pengine wenzangu wameshazizungumzia. Lakini labda nifanye masahihisho kidogo, ile *volume* namba *two vote 23* nianze na ile ukiangalia ile *vote 23* naomba Mheshimiwa Waziri na Watu wake wacheki, ile *vote* kuna *sub vote* karibu kumi zote hazionyeshi mishahara ya zile *various section* ziko wapi, kuanzia 3002 mpaka 3025 mishahara haionyeshwi hizo pesa ziko wapi? Pamoja na *sub vote 7001* ya pili *Vice President Office sub vote 1006 page 104*. Pia haionyeshi *ethics and secretariat page 160* nayo haionyeshi hakuna, *sub vote 1002* mpaka *1006 salaries* hazipo ziko wapi fedha hizi.

*Prime Ministers Office vote 37, 1007, 1008* nayo hakuna, *defence sub vote 1007 land forces command, 1008 air defence command, 1009 navy command* mishahara iko wapi kwenye hizi haiko kwenye kitabu hiki, *vote 40 page 165 sub vote 1002* na *1003 internal audit finance and account unit* hakuna, *vote 45 national audit office sub vote 1002* mpaka *1008 zote hazipo, Ministry of Health* ukienda pia nazo hazipo, *sub vote hiyo*

mpaka 1004 mpaka 1007 hakuna vote 55 *Commission for Human Rights* hiyo mishahara yote haionyeshwi humo lakini mapesa ndiyo yamerundikwa pale. *Defence and National Service sub vote* 1006 mpaka 2002, *Commercial Courts, Estimates* zote hazionyeshwi, vote 92, vote 93, vote 99 na *High Court sub vote* 1006 na vote 19 sub vote 1001, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze hizo pesa ziko wapi.

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Serikali kwanza kwa kuona umuhimu wa mkoa wa Kigoma na kutambua kwamba sasa ni wakati wa mkoa wa Kigoma kupatiwa barabara kupatiwa miundombinu halisi ya kuleta maendeleo katika mkoa ule. Mkoa wa Kigoma kusema kweli kwa takribani miaka yote toka uhuru hatujawahi kuomba chakula. Lakini miaka yote tumekuwa tunapiga kelele hapa Bungeni, kelele zile zinagonga mwanga, lakini Magharibi yote ni kwamba sijui kwanini hivyo vipaumbele havikuona kwamba navyo vinafaa ili maendeleo yapelekwe mkoa wa Kigoma, Tabora, Rukwa mikoa ambayo inazalisha sana.

Mheshimiwa Spika, tulitahidi kutumia hata nadharia ya Maendeleo, tukatumia tukajaribu kuishauri Serikali tukasema kwanini hawatumii *Economics of Geography* ambayo ingewaeleza kwamba uki-develop the western corridor maana yake ni kwamba uta-develop port ya Kigoma, uta-develop barabara ya Tabora Kigoma, uta-develop barabara za Kigoma Nyakanazi, mpaka Kagera, Shinyanga na vyakula vinavyolimwa mkoa ule wa Kigoma vyote vitawenza kupanda na kuja pale juu lakini yote haya yalikuwa hayasikiki, sasa ni wakati umefika wakati wa mkoa wa Kigoma sasa kupewa kipaumbele.

Namshukuru Waziri Mkuu juzi siku ya Ijumaa alifungua barabara inayojengwa kwa lami ya kutoka Mwadiga kwenda Manyovu na mimi nilikuwepo nilishuhudia na Wabunge takribani wote walikuwepo tulishuhudia hii barabara ile ikifunguliwa pamoja na barabara ya Kigoma, Kidawe mpaka Ilunde na katika hili naipongeza Serikali ninaomba muendelee kufanya zaidi bado tuna matatizo ya maji katika mkoa wa Kigoma.

Katika jimbo langu ninaomba Serikali ifikirie kupeleka maji katika viji vili vyoko kwenye miinuko, viji vya Helujuu, Mnanila, Lusaba, Nyaluboza, Mwayaya ambako mimi mwenyewe natoka hakina maji vinahitaji maji sana. Ni muhimu sana kazi hii kufanyika kwa ajili ya mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, ninakwenda haraka haraka kwa sababu sina muda, kuzungumzia bandari ni aibu kabisa kabisa kwa taifa kama la kwetu, kuzungumzia bandari ni aibu *its shame*, kwamba bandari tuliyonayo rasilimali kubwa haifanyi kazi wakati kuna nchi nyingi zinaendeshwa kwa bandari peke yake ni aibu. (*Makofi*)

Leo tunazungumzia habari ya kuweka *flow meter* pale bandari, niliwaambia *flow meters* pale bandari niliwaambia *flow meters are just as good as a person who looks after those meters they can work* ndiyo maana hatujui *supply* ya mafuta ndani ya nchi ni kiasi gani toka tumeziweka faida yake imekuwa nini? Leo tunaweka Bajeti ya kuweka *flow*

*meters za kazi gani wakati hatujaweza ku-manage zilizopo vizuri tukajua hata mafuta yanayoingia nchi ni kiasi gani. Mtu ambaye hajui zile mashine anasema ni fake, si fake zimeharibiwa ili kuleta maslahi wanaoleta mafuta. (Makofi)*

Tembeeni mkaone *port* zingine zinavyofanya kazi, tuna *port* nyingi, *port* ya Mtwara *port* ya Tanga, miaka iliyopita tulishauri *port* hizi zipanuliwe zote kwa pamoja zifanye kazi mizigo ya Uganda iwe *handled* na bandari ya Tanga, ijengwe barabara nzuri kutoka Tanga kuititia Manyara kwenda Musoma. Tukashauri *port* ya Mtwara kuititia *Southern Corridor* itengenezwe vizuri sana ili kusudi mali za kule ziwe kutengenezwa na barabara zitengenezwe, Hakuna aliyesikia *as if that was not development*. Sasa tunajikuta tumekwama hatuna maendeleo mpaka leo, leo unasema kuna *progress* ya kwenda hatua moja mama yako nyumbani ni maskini wapiga kura wangu maskini nijisifu kuna *progress* iko wapi. Ninyi Wabunge achane utani hapa ndani bwana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kodi mbalimbali zimefanywa lakini nizungumzie kodi moja hapa iko kodi ambayo imeondolewa, ukurasa wa 61 *item* ya 15 katika mchango huu ninataka ni *recommend* kuondolewa kwa kodi hii kutaleta *unfair competition* na zile ambazo zinazaliwa *locally* kwenye viwanda vyetu. Kwa hiyo, naomba kodi hii iondolewe ili tusaidie viwanda vyetu maana na *level play field* kwenye hii, iondolewe hii kodi msamaha huo usitolewe. (Makofi)

Mwisho nimekuwa nazungumzia mafuta ya kupikia. Ni aibu kwamba tunakuja hapa tunazungumza habari ya mafuta hatuelewani na watu hawaelewi. Mnazungumza habari ya kilimo. Wabunge mnasema mnaleta kilimo cha kijani, cha wapi kinatoka wapi? Naomba niwaambie mnisikilize vizuri, niliwaambia hakuna malighafi inayotoka Indonesia, wala mahali pengine popote pale. Huu ni wizi unaofanyika, rushwa hiyo mliyopewa muilette tugawane hiyo rushwa mliyopewa leteni tugawane. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili nataka kushauri....

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kusema moja kwa moja watu wamepewa rushwa halafu kutaka tena mgawane yote yanaudhi tu na ni kinyume cha Kanuni ningeomba ufute usemi huo kwa sababu hauna ushahidi wowote. (Makofi)

**MHE. KILONTSI M. MPOLOGOMYI:** Mheshimiwa Spika, nafuta usemi, ninachosema ninaashiria maneno yasiyokuwa mazuri na hakuna sababu kutoelewa na hakuna sababu yakutoelewa kwamba mafuta ghafi yanayotoka Asia na mahali popote. Mimi naomba ni-*recommend* ili kuondoa utata huu ni-*recommend* tuchague Kamati Teule ifanye *research* kama tunasema *East Africa* wanafanya hivi Watanzania hatuwezi kutumia akili zetu na sisi tukafanya kwa mambo yetu tunavyojua. (Makofi)

Sisi tunajua hakuna malighafi inayotoka Malasia ni *congestion* 95%. *Ni refined oil.* Leo tuna mafuta yanayozalishwa hapa mengi tu, leo *nasikitika sunflower* inayozalishwa Dodoma iko 9000 *tones* ziko hapa Dodoma peke yake. Babati leo hii tunapozungumza kuna 25,0000 *tones* ya *sunflower*. Kigoma kuna *tone* 2005 za *palm oil*, Kyela kuna *tone* 2500 karibu za mafuta ya mawese. Singida kuna karibu mara mbili ya yale ya Dodoma ambayo ni zaidi ya tone 100,000 na kiasi chote hiki mnataka kife tu hao

wanalima kilimo hiki wafe tu muende kuwasaidia hao wafanyabiasha wawili watatu ndiyo walete hayo mafuta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu ninaliomba, hii habari ya kuleta mafuta ghafi tuiache hata kama Kenya hawataki hata kama Uganda hawataki, hata kama Ruanda hawataki, wapeni mashamba walime hao wanaozalisha waunganishwe na watu wetu leo. Tuna Watanzania hapa ambao wanataka kuanzisha viwanda vya kutayarisha mafuta na hapa Dodoma kiko kiwanda kinachoitwa Sensozopa ambao ni *sunflower processors association*. Hivi sasa wanatafuta *the latest equipment* ili waweze kuzalisha mafuta ya kupikia ya *sunflower*.

Leo sisi tunasema tunataka kuleta 95 ya kuja kupikia tunawasamehe 10 percent kodi. Kodi hii iondolewe ifutwe kama tulivyoifuta miaka mingine. Ninaomba isiletwe tena humu Bungeni. Isiletwe tena Bungeni, maana hili Bunge tunalifanya kama Bunge la mchezo mchezo. Kwa nini inakaa inarudi eti kwa sababu Kenya wamesema huku tunajua hakuna anayezalisha mafuta ghafi, mafuta yanayokuja 95% ni *final*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naomba ile Kamati teule ninayoshauri itakwenda nje ihakikishe kama kuna mafuta ghafi yanatolewa Malasia, itakuja itafanya *local capacity* mbegu za mafuta zilizoko ambazo zinakosa soko. Naomba tuteue Kamati ile ya Bandari ninaomba nayo nilete hoja, iundwe Wizara ya Bandari, Wizara ya Bandari zetu zote itakayoangalia bandari za maziwa, bandari ya Kigoma ipanuliwe, Kongo kuna biashara kubwa huko kwenye *dry port* zote ziangaliwe na hii Wizara kuliko hii Wizara moja iliyoshindwa kufanya kazi yake. (*Makofi*)

Viwanda vyetu mviangalie, mbona hamuangalii viwanda vya ndani mnaangalia vya nje tu, na vichache vya watu wachache kama wawili watatu wanaozalisha ambao mpokaribu nao. Haya maneno siyasemi kwa kujifurahisha wewe uliona yale niliyokuwa sikuwa nasema kwa kujifurahisha *is because am exist for what is happening here, thank you very much.* (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hivyo ndivyo sauti yako ikiwa mbaya sijui safi kabisa nadhani mike ingepasuka hapo. (*Makofi*)

**MHE. DORAH H. MUSHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima hata nikaweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mkulo, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wataalam wote kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la msukosuko wa uchumi wa duniani, nasema hivyo kwa sababu umeathiri maeneo mengi, mimi ni Mbunge ninayewakilisha wananchi

wa mkoa wa Manyara, ambao nao pia wameathirika sana na uchumi huu, kuanzia katika sekta ya madini, sekta ya kilimo, mifugo, utalii na kadhalika.

Nikianzia upande wa madini, wananchi wengi wamejikita katika uchimbaji wa madini na wengi wanategemea uchimbaji wa madini kama ndiyo kitega uchumi chao.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vijana wengi wamefukuzwa kazi kutokana na eneo hili na kutokana na msukosuko wa uchumi duniani, machimbo ya madini au *Tanzanite* kwa ujumla imeshuka bei katika soko la Dunia kwa asilimia 50. Hivyo basi imepelekea wananchi wengi ikiwa ni wachimbaji kuweza kusimamishwa kazi. Hili ni tatizo kubwa katika mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumpongeza pia Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alivyozungumza na wananchi tarehe kumi hapa Dodoma. Hotuba yake imetutia moyo na imewatia wananchi wengi moyo kwa jinsi ambavyo ameeleza nini mtizamo wa Serikali katika kukabiliana na tatizo la msukosuko wa uchumi duniani. Hii imetupa faraja kubwa na wananchi wamepata moyo kwamba Serikali yetu inapambana na hali hii na imeonyesha pia mikakati ambayo imeshaandaliwa kwa ajili ya kupambana na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika kilimo, eneo hili limeingiliwa sana na utandawazi kiasi kwamba mkulima hana ulinzi wa kutosha kupambana na hali hiyo ukiangalia masoko, hasa masoko ya ndani utakuta hasa wale wa kipato cha chini hawawezi kukabiliana na hali hii katika kukaabiliana na masoko.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wanaolima kilimo kwa mfano cha nyanya, maembe, nanasi hayo ni mazao ambayo yanaharibika. Ukiangalia katika mtazamo wangu Mkakati wa uzalishaji Usindikaji na hata kusafirisha.

Ni vema Serikali ikaangalia ni namna gani ya kuwasaidia wazalishaji wa mazao hayo kwa sababu mara nyingi utakuta nyanya zinaharibika zinatupwa. Maembe yanaharabika tanayatupa. Utakuta mkulima bado anaendelea kulima na hapati faida yoyote. Kwa kweli Serikali iangalie ni namna gani ya kuweza kuwasaidia wakulima wa mazao kama yale hasa katika kusindika na pia *packaging*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nchi yetu tunalima mazao mengi sana. Utakuta nchi jirani ndiyo inafaidika sana na mazao yetu hasa yale kusindika utaona kwamba watu kutoka nchi jirani wanachukua matunda wanayasindika na *ku-park*. Utakuta tayari *juice* zao ziko kwenye soko duniani kote na utakuta wanatuletea hapa tunanunua na tunafurahia kumbe tungkuwa na uwezo pia wa kusindika na *ku-park* ili na sisi tuweze kuuza bidhaa zetu kama vile wanavyotuuzia sisi kwa bei ya juu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, hapo hapo kwenye kilimo mimi naona kwamba Serikali pia iangalie namna ya kumsaidia huyu mkulima mdogo, ukiangalia Serikali imejidhatiti katika kuwapa wananchi mbolea ya ruzuku na pembejeo kukopeshwa matrekta *power*

*tillers* lakini bado utakuta hatujamsaidia kwa sababu bado tunaendelea na kile kilimo cha zamani.

Kwa mfano, *apples* zinayotoka *South Africa* utakuta watu wengi wanaipenda utakuta inanunuliwa shilingi 600 hapa kule Korogwe na Mombo ardhi ni nzuri tunawenza tukazalisha *apples* na tukawa *na apples* ambazo ni bora. Serikali ifanye jitihada za kumtafutia huyu mkulima mbegu bora ili na sisi tusiendelee na zile *apple* pori ambazo hazina ladha na hata haziwezi kuendana na masoko ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeomba tu pale kwenye mbegu, Serikali iangalie tu uwezekano wa kumpatia mkulima mbegu, halafu pia tupate elimu ya kilimo bora ili basi na sisi tuweze tukafaidika na kujiingizia kipato katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la mifugo. Hatuna wataalam wa kutosha katika Mkoa wa Manyara ni wafugaji na wakulima. Utakuta wataalam 236 katika vijiji 326 tuna upungufu wa wataalam 90 tunapozungumzia ufugaji bora, ufugaji bora tutawezaje hatuwezi kuendelea maana hatuna elimu ya kutosha. Kwa hiyo, tunahitaji wataalam na watoe elimu kwa ufugaji bora ili na sisi tuweze kujiingizia kipato eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee upande wa elimu. Zimetengwa hela nydingi kwa ajili ya elimu, lakini bado hatuna walimu wa kutosha, hatuna vifaa vyta kutosha, tungeomba sana tupate vifaa tutazame kwa makini ukizingatia watoto wengi walioandikishwa katika shule za msingi ni kwa asilimia 30.

Tungeomba kwamba kwa kuwa hatuna walimu wa kutosha tuangalie namna nydingine ya kuweza kupata walimu maana yake sasa elimu haitaendana na walimu tulionao sasa hivi. Kwa nini basi tusitafute watu ambao wamemaliza chuo ambao wanangojea kuajiriwa, hawajapata ajira bado. Kwa nini wasijitolee katika shule zetu za msingi ili waweze kusaidia katika eneo hili, huku walimu wakiendelea kupata mafunzo, kipindi watakapomaliza utakuta ule mzunguko unaweza ukasaidia zaidi. (*Makofi*)

Huku tunaajiri wafanyakazi ambao tayari ni wanataalamu na watasaidia wakati ule walimu wanachukua mafunzo hivyo naona ingekuwa ni afadhali kuliko kungojea au kuwaondoa walimu kabla ya kuhitimu mafunzo ya ualimu.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena eneo la madini, pale kwenye madini nilikuwa nasema kwamba tuangalie pia wawekezaji kwa sababu wawekezaji hawasemi kweli hata kama wamepata faida hawasemi kweli. Kwa hiyo, Serikali iangalie ni namna gani ya kudhibiti maana yake hata yale mapato wanayosema wanayatoa lakini siamini kama kweli yanalingana na kipato au uzalishaji wanaozalisha.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri niishie hapo ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuongea na kuchangia kwenye Bunge lako Tukufu.

Napenda kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na Serikali yake kwa mambo mazuri yote wanayofanya pamoja na Waziri Mkuu Mheshimiwa Pinda kwa kukipa kipao mbele kilimo. Mambo yote yanaweza kusubiri lakini sio kilimo, ndiyo sababu tunasema kilimo kwanza. Pia natoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Naibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha kwa kazi nzuri sana waliyoifanya kwenye Bajeti hii ya trillioni 9.5 nawapongeza sana. Nisije nikasahau naunga mkono kwa asilimia mia moja Bajeti hii ya mwaka huu. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kama ifuatavyo kwanza naanza na elimu, Serikali yetu imefanya mambo mazuri kwa upande wa elimu. Tumejenga shule za sekondari kila Kata hii kila mmoja anakubali kuwa tumenusuru watoto wengi ambao wangekuwa mitaani. Watoto wengi sasa hivi wanasoma kwa hiyo hiyo ni jambo zuri na mafanikio kwa Serikali yetu ya awamu ya nne. Kwa upande wa shule za kidato cha tano na sita Serikali yetu ina mpango natumeshaanza kusema kuwa kila Wilaya ni vizuri liwe na shule moja au mbili za kidato cha tano mpaka cha sita yaani A level. Ombi langu kwa Serikali yetu nikuweka mkazo kwa Bajeti hii ambayo inalenga sana na imetoa kipaumbele kwenye upande wa elimu kwa kuipatia trillioni 1.7 ikiwa ni ongezeko la asilimia 22 kusudi tukishirikiana pamoja na wananchi wetu tuweze kujenga kwa haraka hizi shule ambazo ni za *A level* la sivyo kutokana ongezeko la *Olevel* watoto wengi watabaki mitaani.

Mheshimiwa Spika, pia kwa upande wa elimu, tujielekeze vizuri sana kwa upande wa maabara ili kusudi tuweze kuwa na Wanasyansi wa kutosha kwani sasa hivi shule nyingi tulizozijenga hazijawa na maabara lakini nashukuru kutokana na maelekezo ambayo yametolewa na Naibu Waziri. Ninavyofahamu mimi ni kuwa Serikali yetu imeanza kujenga hizi maabara ila tuweke msisitizo ili hizi maabara ziweze kujengwa tusije tukatoa wanafunzi wengi ambao wanachukua mchepuo wa *Arts* bila ya Sayansi. Sasa hivi ukiwa na wananchi ambao hawana Sayansi huwezi kufanya kitu chochote kwa sababu *Engineer* wote, wanakilimo wote, umeme, yote hayo inategemea Sayansi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miundombinu, ni kweli wote tunaamini Serikali imejitahidi kutengeneza barabara kuu pamoja na barabara za Halmashauri. Kwa hiyo, kwa upande wa barabara naomba kuongelea kidogo barabara ya Tunduru – Namtumbo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tunduru – Namtumbo, kusema kweli ni mbaya sana na sasa hivi haijapata wafadhili na tayari nimeshaongea na Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Kawambwa kuhusu barabara hii. Kupitia Bunge lako hili Tukufu, nazidi kuomba wananchi wa Tunduru na Namtumbo huko Mkoani Ruvuma tuweze kupata hela za kuweza kutengeneza hii barabara kwani huko Tunduru kuna mazao mengi kwa mfano tunalima Korosho na mazao mengine, kwa hiyo, naomba ipewe kipaumbele kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali yetu kwa upande huu wa miundombinu, naongelea upande wa Ruvuma tumepata wafadhili wa kutengeneza

barabara ya kutoka Namtumbo mpaka Mbinga – Mbambabay kule Ziwani. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali yetu kwa upande huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Morogoro, mimi nikiwa Mbunge wa Viti Maalum, barabara za Mkoa wa Morogoro hasa mijini, naipa hongera sana Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwani barabara nyingi za mijini ni nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijijini ni nzuri wakati wa kiangazi lakini wakati wa masika ni vigumu kupita kwenye hizi barabara. Kwa hiyo, kwa sababu Mkoa wa Morogoro ni mmojawapo kati ya Mikoa sita ambayo imepewa kipaumbele kwenye mambo ya kilimo na zenyewe naomba zitiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu kwa kuiona na kuitambua hii Mikoa inayozalisha mazao kwa wingi ikiwepo Mkoa wangu wa Morogoro, Mkoa wa Ruvuma, Rukwa, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Kigoma....

**SPIKA:** Mbona umeruka Mkoa wa Tabora Mheshimiwa Mbunge? (*Kicheko*)

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora bado haujafikiriwa kwani bado haujafikisha vigezo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupewa kipaumbele hicho, naomba kwa upande wa Serikali ambayo kweli imetambua kilimo na kukipa kipaumbele na kukapa hela ambazo ni bilioni 666.9 ilenge sana kuwapa mbolea kwa wakati hasa wananchi wa Morogoro na Ruvuma maana wao shida yao ni mbolea tu tayari wana mwelekeo wa kulima hawana matatizo. Kwa hiyo, tunaomba hizi hela ambazo zimetengwa mbolea iweze kusatikana kwa wakati kwani kilimo bila ya mbolea siyo kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, naishukuru Serikali hela nyingi zimetengwa kuptitia kwenye mpango wa ASDP ambapo unateremka mpaka DADPS. Naomba sana Viongozi tuwashauri wananchi wenzetu, waweze kuelewa hii mipango ya DADPS na waweze kuibua miradi ambayo inaleta manufaa kwa kupunguza hali ya umaskini ambayo imekithiri kwani hela ni nyingi ila hatujazitumia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umwagiliaji, nashauri tuweze kuibua miradi mingi ya kutosha. Kama tunavyoona, nchi yetu ya Tanzania kuna mabadiliko sana ya hali ya hewa, mvua ni matatizo hasa kwa upande wa Mikoa mingi kwa hiyo tukiweza kukazania kilimo cha umwagiliaji na uvunaji maji, tutapata mazao ya kutosha kwa Mikoa mingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kufuata hali ya hewa ambayo inabadilikabadilika, naomba hizi bajeti pia ziweze kulenga Mikoa yote ili waweze kuendesha kilimo cha Muhogo. Muhogo ni zao ambalo linavumilia ukame na mimi mwenyewe naamini Muhogo unaweza ukalimwa kwenye Mikoa mingi hapa Tanzania. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania tusichague chakula, tuweze kulima Muhogo kwa wingi kwa Mikoa mingi. Serikali yetu ikipe kipaumbele zao la Muhogo kwani unaweza ukaula ulivyo kama

Muhogo kwa kuchemsha au kwa kutengeneza unga, Muhogo unaweza ukala majani, Muhogo mti wake unaweza ukautumia kama kuni. Kwa hiyo, Muhogo ni fedha, ni lishe, ni utajiri na Muhogo ni kila kitu ambacho unaweza ukahifadhi na unaweza ukautumia kwa wakati wowote wakati wa chakula kingi na wakati ambapo kuna upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ruzuku ya mbolea, nawa semea wakulima wangu wa Mikoa hii yote ambayo imepewa kipa umbele, bado wanalia na wanasema kuwa licha ya ruzuku bado bei ya mbolea iko juu. Kwa hiyo, tunaomba ruzuku iongezwe kusudi waweze kupata na kununua hii mbolea kwa bei nafuu ili waweze kuzalisha kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ambaye alitoa tamko kuwa haya matrekta madogo yaani *power tiller* kila Halmashauri iweze kununua angalau 50 kwa kila mwaka. Naamini kwa bajeti tayari Halmashauri nyingi zimetenga kununua haya ma-*power tiller* 50. Kwa hiyo, kwa kupitia hizi *power tiller*, tukizitumia vizuri, wakulima wengi watajikomboa kuliko kutumia jembe la mkono na wataweza kuzalisha mazao mengi ukilinganisha na kutumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Spika, umeme vijijini. Nilikuwa nasema kuwa Serikali yetu imejitahidi kuleta umeme vijijini lakini bado haujafika mahali popote. Mikoa hii inazalisha kwa wingi kwa mfano Mkao wa Morogoro unazalisha kweli matunda, tukipatiwa umeme vijijini, tutasindika kwa wingi matunda na tutazidisha ajira kwa wingi hasa kwa akina mama na vijana. Kwa hiyo, naomba Serikali yetu ituangalie kwa macho mawili kwenye Mkao wetu wa Morogoro ambao tunazalisha sana matunda na mboga. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano kwa Mkao wa Ruvuma hasa Tunduru na Namtumbo, huwezi kuamini kuwa ni matatizo sana kupata Redio Tanzania na *station* nyingine za hapa nchini kwa mfano *TBC*. Wananchi wa Namtumbo hasa huko Tunduru, *station* ambazo wanazipata kwa urahisi ni *station* kutoka Malawi na Msumbiji ambayo inakuwa matatizo sana. Kwa hiyo, wananchi wengine wanaowekeza kwenye mambo ya mawasiliano, naomba muangalie na wananchi wa Ruvuma hasa huko Namtumbo pamoja na Tunduru kwani wanasikiliza mambo ya Malawi na Msumbiji wanashindwa kupata habari za nchi yetu kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawa si fu na kuwashukuru sana Wanawake wa Morogoro ambao ndiyo wameniweka hapa Bungeni, nazidi kuwa omnia Wanawake wa Morogoro popote walipo tuweze kushirikiana kwa pamoja hasa kwa upande wa kilimo kwani Wanawake ndiyo wachapakazi na kama tunavyojuza zaidi ya 80% ya Watanzania wanaishi kijijini na wanaishi kijijini kwa kutegemea kilimo. Zaidi ya 50% ni Wanawake na hapa Tanzania na hasa nchi za Afrika wakulima wengi amba ni Wanawake ndiyo wanaozalisha chakula cha hapahapa nchini. Kwa hiyo, akina mama wa Morogoro tushirikiane kwa pamoja kwenye mambo ya kilimo.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili hiyo Mheshimiwa Mbunge!

**MHE. DR. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja hii ya bajeti kwa asilimia mia moja.  
*(Makofî)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro na atafutatiwa na Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope na wakati huohuo Mheshimiwa Lucy T. Mayenga ajiandae.

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninapenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia hoja hii adhimu ya Mipango na Bajeti kwa mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoapongezi zangu za dhati sana kwa mpPENDWA wetu Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya M. Kikwete, kwa hotuba yake nzuri ambayo aliitoa tarehe 10 ambayo ilitoa matumaini makubwa kwa wananchi kuona jinsi gani tunaweza kujinurusu na kuiendeleza kutokana na hali mbaya ya uchumi inayotokana na kuyumba kwa uchumi wa fedha duniani.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninapenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii na Taasisi zake kwa mipango na bajeti nzuri ambayo wameleta mbele yetu leo.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaingia katika uchambuzi wa bajeti hii, ninapenda kuchukua fursa hii vilevile kutoapongezi zangu nyingi za dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkinga, kwa Serikali ya Awamu ya Nne kwa jinsi ambavyo imehamasisha na kushirikiana na wananchi kikamilifu katika kuijenga na kuiendeleza Wilaya mpya ya Mkinga. Miundombinu na shughuli nyingine nyingi zimeteklezwa kwa mujibu wa ilani na tumeweza kupata mafanikio makubwa sana, tunashukuru sana kwa hilo, ni imani yangu kwamba mtazidi kuendelea kushirikiana katika miradi mingine zaidi.

Mheshimiwa Spika, nina faraja kubwa sana kwamba Makao Makuu ya Wilaya yetu yamekamilika na yanaendelea vizuri, nina faraja kubwa sana kwamba baadhi ya miundombinu katika Wilaya hiyo imeshaanza kujengwa vizuri. Hata hivyo, bado tuna maeneo ambayo bado yana kero kubwa na tunaomba katika bajeti nyingine zijazo iweze kufikiriwa ili tupewe misaada inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya kero kubwa sana ambayo inatukera sasa hivi kule ni maji. Tunashukuru kwamba kutokana na ushirikiano tuliuopata kutoka kwa Serikali, tumeweza kuandaa miradi mbalimbali. Nashukuru na ninafurahi kwamba miradi ile ya vijiji 10 chini ya Benki ya Dunia, imefikia hatua nzuri ya utekelezaji na ninaamini kwamba katika bajeti hii tutaweza kuitekeleza kwa ufanisi.

Hata hivyo, Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga, Kasera na Mheshimiwa Rais anayatolea sifa sana popote anapokwenda kutohana na mipango mizuri iliyotengenezwa kujenga mji huu mpya yana dhiki kubwa sana kwani hayana maji. Kutohana na hilo, ujenzi wa majengo na shughuli nyingine pale zinashindwa kutekelezeka. Hivyo ni imani yangu kwamba kutohana na mazungumzo tuliyokuwa nayo na Wizara na Serikali kwa ujumla, mji wa Kasera utaweza kupatiwa maji ili jithada zetu za kuujenga na kuuendeleza mji huo uweze kupata mafanikio yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa zaidi na inayoudhi zaidi, ni kero ya umeme. Tunashukuru kwamba Makao Makuu ya Wilaya tayari imeshapatiwa umeme lakini kuna ahadi ya miaka mingi sana, zaidi ya miaka saba au nane iliyopita ya kupatiwa umeme kwa viji ya Daluli, Gombero, Kwale, Vuga na Boma. Tumepewa ahadi mara nyingi na hata kuwekwa katika bajeti kwa miaka miwili au mitatu iliyopita lakini utekelezaji haujaja. Siku zote tunapewa ahadi ambazo hazitekelezeki, mara tunaambiwa iko chini ya *MCC* miradi ambayo inatekelezwa chini ya *REA* lakini hakuna tunachofaidi katika masuala haya. Kwa hiyo, ikifika Wizara ya Nishati na Madini, nitalizungumzia suala hilo kwa urefu na mimi nitakuwa mkali bila kulaani lakini nitakuwa mkali ili suala hili liweze kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya mazungumzo haya ya jumla, ninapenda sasa hivi nijikite katika hatua ambazo zimependekezwa katika bajeti hii na mpango wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu ya kilimo kwanza ni kauli mbiu rasmi na nzuri inayoendana na hali halisi tuliyonayo sasa hivi. Sote tunaelewa kwamba kutohana na hali mbaya ya uchumi iliyopo duniani na ambayo imetuathiri nchini kwetu, hakuna njia nyingine muafaka na bora ambayo inaweza kutunusuru sisi na kutufanya tuendelee zaidi isipokuwa hiyo ya kuchukua kauli mbiu ya kilimo kwanza.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kufafanua juu ya dhana nzima ya suala hili na vilevile kuelezea ni jinsi gani tunatakiwa sote tujiunge katika uendelezaji wa dhana hii.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kilimo kwa upana wake mkubwa, tunazungumza kilimo cha mimea, mifugo, uvuvi, maliasili kama misitu na vitu kama hivyo. Baadhi yetu tunafikiria kwamba tunapozungumzia kilimo, tuzungumze kilimo kile tu peke yake cha mimea. Mimi kwa fikra zangu ni kwamba kilimo kwa upana wake kinahusu sekta zote hizi nyingine ambazo zinahusika na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa basi, tunapozungumzia kilimo kwanza, maana yake ni kwamba kilimo katika sekta zote hizo kwa upana wake huu ndiyo cha kupewa kipaumbele, ndiyo cha kutuokoa sisi kutupeleka mbele. Hapo zamani tumekuwa na kauli mbiu nyingi na tumekuwa na mikakati mingi juu ya suala hili lakini naamini safari hii, hii mikakati tuliyoiweka ni ya dhati zaidi na ya nguvu zaidi na linalotakiwa kwa sisi sote,

wananchi wote, Viongozi wote, sekta zote mbalimbali tufikirie kilimo kwanza, tutoe kipaumbele kwa kilimo katika jitihada zetu za kujikomboa na kujiendeleza katika uchumi wetu ili kilimo kiweze kuchangia kwa kiasi kikubwa zaidi katika pato la taifa kuliko ambavyo sekta nyingine zinafanya sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hii, ninapenda kutazama ni vipi sekta mbalimbali zinaweza kuchangia katika suala hili, wengi tunesema kwamba ingawa asilimia ya bajeti tuliyopewa kwa kilimo ni ndogo, ni ndogo ukifikiria kwa kilimo kama Wizara peke yake lakini ukifikiria miradi mbalimbali kwa mipango mbalimbali iliyopo kwa mfano *ASDP* na mingine imetoa fursa ya Sekta hizi nyingine kuchangia kwa karibu zaidi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, ninapenda kutazama namna gani sekta nyingine zinatakiwa zichangie katika hili kwa mfano sekta ya viwanda. Tunatakiwa katika viwanda kufikiria ni jinsi gani tutachangia katika kuboresha kilimo. Kwanza, kuna viwanda vya kuzalisha pembejeo za kilimo, mbolea, madawa mbalimbali, matrekta ya kulimia na majembe mbalimbali pia. Sasa katika mipango yetu hii, ni vizuri tuzingatie kwa kiasi gani tutaelekeza viwanda vyetu hivi viweze kusaidia sekta ya kilimo ipate tija na maendeleo yale yanayotakiwa na hatua gani tuchukue kufufua viwanda vyetu vile vya zamani na kujenga viwanda vingine vipyambavyo vitasaidia katika jitihada hii kwa kuweka sekta ya kilimo iwe sekta ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, kwa mfano kiwanda kilichokuwa kinaitwa *UFI*, sasa hivi hakishughuliki tena kuzalisha majembe ya aina mbalimbali, kinazalisha mabomba. Kwa hiyo, kuna haja Serikali kuchukua hatua thabiti ya kuhakikisha kwamba wale wawekezaji wanafanya kazi iliyokusudiwa. Kiwanda chetu cha mbolea cha Minjingu kichukuliwe hatua thabiti ya kukiendeleza. Nafurahi sana kuona kwamba Serikali imeamua kuweka hisa kule ili kiwanda cha mbolea cha Mtwara kiweze kuzalisha na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, viwanda vingine ni viwanda vya usindikaji. Viwanda vya usindikaji vingi tulikuwa navyo hapa ambavyo vinaongeza thamani lakini bahati mbaya kwa mfano viwanda vya nguo vingi vimetetereka, nashukuru jitihada zimefanywa kuvifufua viwanda hivyo. Lakini bado jitihada kubwa inahitajika kuviendeleza viwanda hivi ili viweze kuchangia katika kuongeza thamani ya mazao na ili kilimo kiweze kupanuka.

Mheshimiwa Spika, kuna viwanda kwa mfano vya mikokoteni, viwanda vingine vya kusaidia uchukuzi katika kilimo, fikra zetu tuzielekeze ni vipi viwanda hivi vinaweza kusaidia kurahisisha shughuli zetu. Tumezungumza habari ya matrekta madogo na mengine, sasa kuna taasisi zetu kama vile *CARMATEC*, *TEMDO* imetengeneza mitambo mingi mbalimbali lakini bahati mbaya tunashindwa kuiendeleza kwa sababu hatukuweka umakini unaotakiwa katika suala hilo. Kwa hiyo, tujielekeze ni namna gani taasisi hizi na vifaa hivi vilivyotengenezwa vinaweza kuelekezwu katika kuendeleza jitihada zetu za kusaidia kilimo ili kuleta mafanikio.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano tunapokuja katika suala la biashara na masoko, suala la utafiti ni suala muhimu sana. Tumeweka taasisi mbalimbali na bodi mbalimbali ambazo zinashughulika katika masuala haya lakini pengine mkazo hatuweki katika kufanya utafiti wa masoko. Kwa hiyo, zile fedha ambazo tunatakiwa tuzitenge kwa utafiti wa masoko, utafiti wa kuboresha mazao katika *RND institutions* na katika taasisi nyingine hatuna budi tuhakikishe kwamba ile 1% ya pato la taifa inatumika ipasavyo katika kuendeleza taasisi hizi za *RND* mbalimbali katika kilimo na maeneo ya viwanda ili shughuli hizi ziweze kuelekezwa katika kuendeleza kilimo kwanza.

Mheshimiwa Spika, magilio yetu yamejipanga namna gani katika kusaidia mazao yetu yaende kwa kasi nzuri na kupata bei nzuri zaidi na kwenda katika hali nzuri zaidi? Tumezungumza habari ya masoko ya Kimataifa kwa mfano pale Segera na Makambako, muda mrefu tunesema kwamba tutayatengeneza masoko ya Kimataifa kuweza kusaidia uzalishaji wa bidhaa za mboga na matunda, lakini hayo ni masuala ambayo tumezungumza miaka nenda miaka rudi hatuoni maendeleo yoyote yanayofanywa juu ya masuala haya. Ni muhimu tukajizatiti ili haya mambo yakaweza kufanya.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna mfumo wa stakabadhi ghalani, mfumo huu umeanza vizuri katika maeneo ya kusini kwa bidhaa mbalimbali za Korosho lakini ni vizuri mfumo huu tukauboresha, tukauelezea vizuri zaidi ili uweze kuwapa wakulima fursa ya mazao yao kwenda vizuri zaidi na wao kuendelea kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, tumezungumzia habari ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko lakini hii hadithi nayo imekwenda miaka mingi hatujaona maendeleo ya Bodi ya Mazao Mchanganyiko imefika wapi, hili ni suala la kutazama.

Mheshimiwa Spika, masuala ya miundombinu kwa mfano mawasiliano ni muhimu sana katika kuendeleza biashara ili wananchi waweze kujua habari ya masoko yao. Jitihada zimefanyika lakini tunapofikiria mawasiliano, tuone vipi tunaweza kumsaidia mkulima na wafanyabiashara na wenye viwanda kuendeleza biashara zao katika masuala haya. Bandari, Reli na Barabara Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia masuala haya, tufikirie ni jinsi gani tunaweza kuziboresha Bandari zetu, Reli zetu na Barabara zetu ili zitoe mchango wake katika kuboresha kilimo na chenyewe kiweze kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, nishati na maji, ni mambo muhimu sana katika umwagiliaji, katika uendeshaji wa shughuli mbalimbali za uzalishaji na yameshaezwa, haya mambo tuyashughulikie ili tuone ni kiasi gani Nishati inatakiwa iweze kuchangia katika uboreshaji na ufanisi wa kuleta kilimo kwanza. Vilevile maji kwa umwagiliaji na maji kwa mifugo na shughuli nyingine kama hizo.

Mheshimiwa Spika, habari ya fedha, Sekta ya Fedha ina kasi kubwa sana, tumefurahi kusikia kwamba Benki ya Kilimo itaanishwa, lakini hata hizi benki zilizopo, hata mifuko mbalimbali iliyopo, ina haja ya kufanyiwa marekebisho kama yalivyozungumzwa na sera zake zikawekwa sawa ili kuwasaidia wananchi kihalisi. Sasa hivi kuna kiu sana ya wananchi wanaotaka wawezeshwe ili waendeleze kilimo lakini

utekelezaji unakuwa ni hafifu. Kwa hiyo, utekekelezaji unastahili uboreshwe katika shughuli hizi ili shughuli ziende vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengine muhimu kwa mfano viwanda vyetu muhimu ambavyo tunatakiwa kuvilinda humu ndani. Waheshimiwa wengi wamezungumza habari ya viwanda vyetu vya ndani kuvilinda. Viwanda vya Pamba, Ngozi, Chai, Kahawa na hata viwanda vya Matairi ambavyo tu siyo vinatumika sana kuendeleza bidhaa zetu lakini vinatoa ajira na vinaleta mapato. Sasa hivi kisera, inatakiwa sera za fedha zivilinde viwanda vyetu hivi. Tumezungumza mbegu za mafuta, tunaachia wazi na tunaachia ushindani, haya ni masuala ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyasisitiza na mimi ninapenda nisisite kwamba ni vizuri tukaangalia jinsi gani tunaweza kupeleka sera zetu na taratibu zetu hizi na mikakati mbalimbali ili kilimo chetu kiweze kupata nafasi ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, sasa elimu. Elimu bado ni kipaumbele cha kwanza. Tunataka Wataalamu ambao watafundishwa na kupata eimu nzuri ya kujua taaluma zao mbalimbali za ughani na shughuli za ujasiriamali, ziweze kuchipua vizuri ili wawe wajasiriamali wazuri, waghani wazuri waweze kuchangia katika uchumi wa taifa hili. Kwa hiyo, zote hizi ni fikra zetu, tunaposema kilimo kwanza katika sekta mbalimbali tuone vipi sekta hizi zinaweza kuchangia katika kufanikisha azma hii ya kufanya kilimo kwanza, vivyo hivyo, katika utafiti na katika shughuli nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, napenda kuchukua fursa hii kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, sasa ni zamu ya Raynald A. Mrope, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga na wakati huo huo Mheshimiwa Salim Yussuf Mzee ajiandae.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia angalau kidogo hii bajeti iliyo mbele yetu.

Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri wa Fedha kwa kuturahisishia, wamefanya kazi kubwa sana ya kueleza na kupanga vizuri bajeti hii kiasi kwamba imekuwa rahisi kwetu na kwa wananchi ambao wanaielewa.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika yale yanayonisibu katika bajeti hii na ninataka niongelee Mtwara ambayo mpaka sasa hivi katika bajeti hii haijaongelewa.

Mheshimiwa Spika, Mtwara wakati huu ndiyo ulikuwa hasa hasa wa kuzinduka, kwa sababu ya kutumia raslimali walijonayo. Pale *Mnazi bay* kuna *gas* nyingi sana sana, kuna *gas* kiasi cha *2.6 trillion cubic feet* ambapo kama tungeitumia kwa umeme tu, tungeweza kuitumia kwa miaka 700 na kama tungetumia kwa viwanda, tungeweza

kutumia kwa miaka 100 ijayo. Sasa kwa nini nchi hii isiendo Mtwara ikaanza kutumia fursa hizi na kwa nini haipo katika bajeti hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kuna mahesabu ya kitaalam ya Artumas na Wizara ya Nishati, yanayoonyesha kwamba Serikali kwa kipindi cha miaka 15 ingeweza kupata faida ya dola 391 milioni, *TPDC* wangepata dola 331 milioni na *ARTUMAS* wenyewe wangepata dola 235. Kuhusu kutengeneza *gas* hii ili iwe na faida yaani kwa mfano *compressed gas* ama *liquefied gas*, hizo peke yake zingetoa dola 477 milioni, *TPDC* wangepata 364 milioni na *ARTUMAS* wenyewe wangepata 230 milioni. Kwa maana nyingine Mtwara ingetoa mabilioni na mabilioni, sasa watendaji Serikalini hamuoni? Hamna macho? Hamsikii? Mipango iko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi Mtwara jamani ina balaa gani? Kwanini Mtwara? Mwenyezi Mungu alivyoijalia namna hii, kwanini tusikimbie moja kwa moja kwenda kuhakikisha kwamba, hizi rasilimali zote zinatumika mara moja ili tujiokoe sisi wenyewe, kwa nini mambo yanakwenda polepole? Hivi tunakwama wapi?

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunakwama kwa watendaji wakuu katika Wizara za Nishati, Fedha, Benki Kuu, *TANESCO* na kwa kiasi kidogo *TPDC*. Hawa wanapelekewa hii mipango lakini kwa namna moja au nyingine hawaipeleki kwa Mawaziri, ili waweze kutoa *informed decisions*, hii ndiyo shida kubwa. Kwa hiyo, utakuta faili linakaa kwa Mkurugenzi wiki tatu au wiki nne na akipata safari ndiyo hakuna lolote atakalofanya, hakuna atakayeshughulikia. Kwa hiyo, Mawaziri au hata Rais, hakuna ushauri mzuri wanaopelekewa. Sasa kwa nini tuendelee na utaratibu huu jamani? Eeh Mawaziri kwa nini msifuate Ari Mpya, Kasi Mpya, Nguvu Mpya na badala yake katika suala hili mimi naona kwa mambo ya Mtwara, imetiwa gia ya *reverse*? Tunarudi nyuma kwa Kasi Mpya, Nguvu Mpya, mambo gani haya? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa taifa hili kuwa na gesi nyingi namna hii, kwa kweli tungekimbia upesi upesi kuhakikisha kwamba, tunapata faida, lakini mimi najiuliza hivi watu hawa wako wapi? Eeh, hawa wataalamu wetu wanafanya nini? Mtwara kwa nini ina balaa hizi zote hizi? Kwa nini hamuitaki Mtwara? Hebu fikiria, *ARTUMUS* ilitaka kueneza umeme nchi nzima kwa kutumia *Mega Watt* 300, mara baada ya kuwaleza *TANESCO*, *TANESCO* wakaonyesha dhahiri kwamba, hawapendi. *Barrick Gold* kwa kuwa wanautaka umeme huu wakasema sisi *tuta-invest*, yaani tutatoa fedha ili mradi huu utekelezwe, kipingamizi cha kwanza kilitoka wapi, *TANESCO*. *TANESCO* wakakataa wakasema wakitaka *Barrick* fedha hizo wapewe *TANESCO*, wakupe wewe kwa ajili gani bwana? Kutokana na hayo *Barrick* wakajitoa kwani hawapendi fedha zao zifujwe na *TANESCO*. Wamekataa kwa sababu fedha hizo haziji kwoao ili wazile sawasawa. Sasa jamani Wizara zipo, mambo haya mnaangalia mpaka lini, watu wa kwetu ndio wanaoumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tumetegemea kwamba, kwa hivi sasa kwa kutumia huo umeme tungeweza kabisa kubadili hali ya kusini. Hapo hapo mwaka 2007, wenzetu wa Kenya walikuwa wanataka kuchukua MW 200 za umeme na wenzetu wa *ARTUMUS* walitayarisha mpango wa kupeleka Kenya, umeme wa *Mega Watt* 200 kwa kuitia meli

mbalimbali zilizotengenezwa kwa madhumuni hayo, tungepata fedha nyingi sana zaidi ya bilioni 500. Toka mwaka 2007 mpaka leo, uamuzi haukutolewa. Kwa hiyo, Kenya wenyewe wamesitisha wamesema hatutaki tena gesi yenu kutoka Tanzania, wamekwenda Ethiopia na wameishatiliana saini ili Ethiopia ipeleke gesi hiyo Kenya. Sasa tunakosa mabilioni yote haya kwa sababu Serikali haijatoa uamuzi ama hawaitaki Mtwara au hawataki mradi huu utekelezwe, sasa mambo gani haya jamani? Serikali ipo? Nazungumza kwa uchungu sana na nafikiri watu wote wa Mtwara wanajiuliza kuna nini? Kuna nini? Kuna nini? Labda Waziri wa Fedha utajibu haya. Mwishoni kabisa tunakuja kukuta hata ile mipango iliyokuwa imekamilika ya kujenga viwanda vyta sementi, viwanda vyta mbolea, viwanda vyta chuma chakavu, nayo hiyo yote imefutwa katika mpango huu, sasa najiuliza kwa nini? Kulikoni? (*Makofi*)

Waziri wa Fedha, naomba utuambie hivi kuna nini? Miradi hii ndiyo ambayo baada ya barabara kuja, yange-*create* ajira na pia yangebadili hali ya Mtwara. Kwa hiyo, sisi katika bajeti hii tunaiunga mkono na kuiomba Serikali kuwa sasa nendeni Kusini huko ili kuhakikisha kwamba, gesi hii inatumika vizuri, tafadhali sana, haya mambo haya yanaudhi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ijue kwamba, ina wajibu wa kuendeleza Kusini na kuendeleza kwake wangeanza sasa kutokana na gesi hii, yaani kutakuwa na viwanda vingi mno, sasa mtu ye yeyote anayezuia maendeleo haya sisi hatuwezi kumwelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *ARTUMUS* kupewa mkopo ni sawasawa kabisa. Ni sawasawa kwa sababu, umeme vijijini dunia nzima haulipi, lazima Serikali isaidie. Kwa hiyo hizi bilioni 7 wala sio fedha nyingi. *TRA* wanasema kila mwezi wanaingiza mapato ya bilioni 340, sasa bilioni 7 kweli mnaweza kushindwa ikawa *issue*? Naomba hili wala lisiwaumize vichwa kwa sababu ni utaratibu wa kawaida na kumekuwa na msukosuko, fedha hizi zinahitajika na baada ya hapo miundombinu hii yote itakuwa ni mali ya wananchi wa Tanzania sio *ARTUMUS*, sasa mnalalamika nini? Roho mbaya tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niende upesi upesi kwenye mambo mengine. Kuna suala la elimu. Katika upande wa elimu sisi tumesikitika sana kwamba, kumekuwa na kampuni moja inayoitwa *Bayport* imewarubuni Walimu wetu wengi katika Mikoa ya Lindi na Mtwara. Kwa bahati mbaya, kampuni hii, mimi naona ni afadhali ya *DECI*, walisema kwamba, watakuwa wanakopesha kwa asilimia 18 lakini ukifanya mahesabu inaonekana asilimia waliyochukua ni 198.

Mheshimiwa Spika, nitawapa mfano, yupo Mwalimu wangu hapa, Prudenciana Mwambe wa Mkalapa. Yeye amekopa shilingi Laki Tisa (900,000), analipa Milioni 1, 507,866, jamani haki ya wapi? Mwalimu Brigita Germanus, huyu yuko Mwena pale. Amekopa laki Saba, anatakiwa alipe Milioni 1,000,172. Naomba Wizara ya Fedha iingilie kati, iiambie Benki Kuu, hizi asilimia kubwa za namna hii kwa kweli ni wizi, ni utapeli tu.

Mheshimiwa Spika, hawa Walimu hawawezi hata kidogo kufundisha katika hali ya namna hii. Mwalimu anapata shilingi 12,000 au elfu 20,000 kwa mwezi atafundisha namna gani? Hawa matapeli hawa ndio wanaoiba fedha zetu. Benki Kuu, chonde chonde hivi hamna kanuni za kuhakikisha kwamba, mtu anayekopessa anaweka riba inayoelewaka sio kutunga tu riba yoyote apendayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, twende sasa katika ujenzi, jamani upande wa miundombinu kuna daraja la Nangoo. Daraja la Nangoo hili ndiyo kiunganisho cha Mtwara *Corridor*, lisipojengwa hili, kwa vyovyote vile hata tuka-*invest* Kusini ni bure, hatutafika. Kwa hiyo, tuambiwe katika bajeti hii, lini daraja la Nangoo litatengenezwa ili wananchi wasiwe na wasiwasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maji, mimi nashukuru Waziri amejitahidi sana sana kwamba, mradi wa Mbwinji uendelee. Naomba Serikali ikamilishe mradi huu ili maji yapatikane Masasi na si hivyo tu hata vianzio vingine kwa mfano, bwawa la Mchemwa au chemichemi nyingine hizi, Mwena, Ndanda, Nahinga sehemu zote hizi zinaweza kupatikana vyanzo vizuri vya maji yakaenda Masasi. Kwa hiyo, hapa napo ni mahala pa kubwa pa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, upande wa TAMISEMI. Jamani kwa muda mrefu mmeahidi kwamba, Masasi itakuwa mji, tunaomba Halmashauri ya Mji wa Masasi ianzishwe. Kuna miji mingi sasa hivi imekuwa Halmashauri za Miji, Miji midogo tu. Masasi ni kongwe lao, lakini mpaka sasa hivi bado Masasi haijawa Mamlaka ya Mji, tafadhalii sana katika bajeti hii hili liwekewe mkazo.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo, Mkoa wa Kusini, tunakumbusha, kwa Wilaya za Tunduru, Nanyumbu, Masasi, Nachingwea na Liwale. Wataalamu wote ukiwapelekea suala hili, hawataki kutu-*support* kwa sababu wanajua madaraka yao yatapungua, lakini sisi wananchi tunasema, Mkoa huu uanzishwe kwa maendeleo ya kule Kusini, ooh!

Mheshimiwa Spika, naona nimefikia mwisho na naunga mkono hoja ila haya niliyoyazungumza, naomba sana sana yazingatiwe, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, Ahsante sana kwa kunipa nafasi hii walau na mimi kuweza kutoa mawazo yangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa hotuba nzuri ya kuelezea mpango mkakati wa kuweza kukwamua Taifa letu katika hali mbaya ya kiuchumi tuliyonayo. Lakini la pili, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake wote wawili, kwa hotuba nzuri ya bajeti ambayo wameitoa.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila, ninaomba nitumie nafasi hii kuwashukuru Wabunge wote Wanawake, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kunifanyia kampeni kubwa na kunisaidia kuwa, Mjumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UWT, Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia wachukue pongezi hizi, kwa niaba ya Wenyeviti wote wa Umoja wa Wanawake, Tanzania, Mikoa ya Bara pamoja na Visiwani, pamoja na Makatibu wote wa UWT, Mikoa ya Bara na Visiwani, nashukuru sana kwa kura zao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema yafuatayo, ninapokuwa nina nyumba yangu, nikawa na watoto wangu, watoto wangu watakuwa wana mahitaji mbambali. Lakini vilevile, ninaweza nikawa na mtu ambaye ni mhudumu wa nyumbani, anaweza akawa ni mtu mzuri sana, ni mwaminifu sana na kutokana na uaminifu wake wa muda mrefu na kazi yake nzuri ya muda mrefu, inatokea tu kiubinadamu mtu unamwamini kwamba, mhudumu mimi nakuruhusu kuna pesa nitakutengea, naweka chumbani kwangu, ninaomba inapotokea tatizo lolote kama ni chakula, kama ikitokea dharura yoyote, ingia chumbani kachukue. Lakini inapotokea mhudumu huyu nikaja nikagundua dosari yoyote katika ule uhuru niliompa, nitafanya uamuzi amba kwa kweli mtu yeyote anaweza akaufanya. Kwa hiyo, nitakachokifanya ni kufunga mlango wangu. Nikifunga mlango wangu, sitarajii watoto wangu waje waanze kusema, kwa nini mama umefunga mlango. Ninatarajia kwamba, watoto wangu wataniuliza, hivi sababu ya mama kufunga mlango au sababu ya baba, *lets say* baba kufunga mlango ni nini?

Mheshimiwa Spika, hili lina maana gani? Misamaha ya kodi ambayo imekuwa ikitolewa katika Taasisi za kidini pamoja na makampuni ya madini imekuwa inatumiwa vibaya sana. Nchi yetu hii ambayo ni masikini, mwaka 2008/2009, imetoa msamaha wa kodi asilimia thelathini (30%) ya mapato yetu, Kenya na Uganda mkiachilia mbali wako katika uchumi mzuri, wanatoa msamaha wa kodi kati ya asilimia 14 na 15. Sasa wema wetu huu unatuponza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu taasisi hizi za kidini kila mwaka kutokana na misamaha hii ya kodi, kiasi cha shilingi bilioni 1.26, Serikali inapoteza kutokana na misamaha hii. Hii nchi bado ni masikini sana, inahitaji kuwepo na utaratibu maalum wa kuhakikisha kwamba, tunajaribu kuangalia vyanzo vya mapato kokote vilipo ili walau haya ambayo tunalalamikia hapa kwa mfano barabara ni mbovu, bandari haifanyi kazi na nini, walau kwa njia moja au nyingine, huduma za wananchi ziweze kupatikana. Napenda kuchukua nafasi hii kuunga mkono uamuzi wa Serikali kufuta hii misamaha kwenye taasisi za kidini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, nchi yetu inajulikana kwa tatizo moja, mipango inakuwa mizuri sana, mikakati ni mizuri sana lakini utendaji unakua ni mbovu. Suala hili la misamaha limekuwa likizungumziwa na sasa hivi naona limekuwa tena ni kama vile la kisiasa. Watu wamekuwa wakilizingumzia sana na taasisi za kidini zimekuwa zikilalamika sana. Mimi natoa pendekezo, kama ikiwezekana basi hii misamaha isiwe *blanket*, yaani isiwe tu kwamba, ni misamaha inatolewa basi. Naomba kwa sababu imethibitika na inajulikana, kwa sababu najua Serikali haijakurupuka tu kuamua hii misamaha kwenye taasisi za kidini iondoke, ilikaa ikifanya *research* na kuangalia ni sehemu gani inaonekana kuna *loop hole* ndiyo maana wakafikia uamuzi huo, ninashauri ifuatavyo. Kwa sababu imegundulika kwamba, zipo taasisi za kidini ambazo

viongozi wake sio waaminifu, watu wamekuwa wakitumia *exemptions* hizi vibaya, mtu anasema *let say*, anataka kujenga jengo fulani, kama ni jengo la ibada au ni jengo la kitega uchumi kwa ajili ya taasisi hiyo, anaomba *exemption* kwa ajili ya kuingiza vifaa kwa ajili ya ujenzi huo kiwango ambacho ni zaidi ya ukweli halisia wa kile kiwango ambacho anatumia na matokeo yake yanakuwa ni nini? Matokeo ni kwamba, hawa viongozi wanajihusisha na biashara kwa sababu, anapoingiza hivi vitu vinazidi kiwango atatumia kile kiwango kwa kile kitu chake ambacho anakifanya, lakini kiwango kinachobaki anakuza.

Mheshimiwa Spika, sasa tusifikie mahali hizi taasisi za kidini ikawa sasa kuna kama ugomvi, wamefanya kazi nzuri sana katika nchi hii, wamehudumia wananchi wengi sana katika hii nchi, sasa isiwe tena wanatumia hii kwamba ni ibada, ni mambo ya Mungu na hii mambo ya ukarimu na utaratibu na Umungumungu, wakatumia hii misamaha vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, napendekeza kama hivyo ndivyo, Serikali basi walau iweze kuangalia utaratibu ambaao utahakikisha kwamba, masuala yote ya taasisi za kidini, misamaha hii iwe na utaratibu ambaao unajulikana. Kwa mfano, kama taasisi hizi za kidini ziko 200 ingawa mpaka sasa hivi ziko zaidi ya 300, basi walau ziwe na utaratibu, kama ni Waislam wawe na utaratibu wao kuwa huyu ndiye mtu ambaye atakua anashughulikia *exemptions* za Waislam, kama ni Romani Katoliki, iwe ni kwamba, huyu atakuwa ni mtu ambaye anazungumzia *exemptions* za Romani Katoliki, kuwe na utaratibu maalum. Lakini Serikali imeacha watu wanajifanyia mambo yao, watu tunakaa hapa tunalamika kwamba, mambo hayaendi, Serikali kila siku inasema haina pesa, Sungura Mdogo, Sungura Mdogo wakati mnaacha mambo yanaenda hovyohovyo namna hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na suala hilo, ninaomba Serikali iweke utaratibu maalum katika hizi taasisi za kidini ambaao utawezesha huduma hizi ambazo wao wanazihitaji kwenda katika mpango maalum ili kuepusha masuala ya wizi na udanganyifu ili tusirudi kule ambako tunapafikiria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo nataka kulizungumzia, ni kuhusu suala zima la Sheria ya *Public Financial Act* ya mwaka 2001 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2004. Sheria hii inamtambua Mkaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na mlipaji kodi lakini ipo Sheria ya *Local Government Finance Act* ya mwaka 1982. Hapa kuna *contradiction* kidogo. Kwenye hii sheria ya kwanza, inamtambua huyu mlipa kodi pamoja na Mkaguzi, lakini huyu anatambulika katika ngazi ya *Central Government*. Hivi sasa Serikali, hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, alielezea kuhusu suala zima la *D by D*, imekuwa ikihubiriwa sana mpaka kwenye ngazi za chini, Serikali inajaribu kupeleka matumizi moja kwa moja kule, pesa nyingi sana zinapelekwa kule lakini msimamizi wa pesa zile ni nani? Haiwezekani ikawa mpaka leo, Serikali inajua hiki kitu na inafahamu hili tatizo lakini imenyamaza kimya! Mimi nashindwa kuelewa na ninashangaa sana. Kwa nini katika Serikali za Mitaa hakuna Mkaguzi wa Hesabu? Kwa sababu hawa wakaguzi wengine ambaao wanatambulika na hii sheria ya kwanza, ni wakaguzi ambaao wanatambulika wako katika *level* ya juu kabisa hawawezi kushuka huku

kwenye ngazi ya Serikali za mitaa na kuanza kukagua huku. Kazi ambayo inafanywa na Kamati hizi nyingine za *LAAC* na Kamati nyingine, ni kama *physical evaluation* lakini kama kukiwa na Mkaguzi Mkuu huyu ambaye atakuwa katika ile ngazi ya *Local Government*, itasaidia matumizi ambayo yako kule, kwa sababu kuna matumizi mengi na Serikali bado inaendelea kusema kwamba, tunataka *ku-decentralize* masuala yote ya matumizi ya fedha na huduma nyingi ziwe zinakwenda moja kwa moja kule kwa wananchi, lakini haya mambo hayawezi kwenda bila hizi Sheria kubadilishwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nashangaa sana kwa sababu pia kuna suala lingine kwenye haya masuala ya kubadilisha Sheria. Sheria ya Madini, hivi hii Serikali nani anakwamisha Sheria ya Madini kuingia humu ndani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nimetoka kuzungumzia hizi *exemptions* za taasisi za kidini, lakini bila Sheria ile ya Madini kuletwa humu ndani itakuwa ni hadithi, itakuwa tunaongea hapa, watendaji wanatusikiliza na hakuna hatua ambayo wanaichukua. *Exemptions* ambazo zinatolewa kwenye makampuni ya madini, mpaka hivi sasa ni shilingi bilioni 1.25, hizi zinatolewa kila mwaka. *Exemptions* hizi, Serikali imesema kwamba, zinafutwa kwa yale makampuni ambayo yataanza usajili tarehe 01 Julai. Kufanya namna hii, tunarudi kulekule kwa wale watu ambao walisaini hii mikataba maana yake tunaambiwa kikwazo ni kwamba wale waliishaingia mikataba kwa hiyo itabidi tena kuanza kuivunja, inakuwa ni kama vile ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Spika, mimi huwa nasema hivi na kila siku huwa nasema na naelezea kwamba, yale mawazo ya yule *DC* aliyeamua kuwachapa Walimu viboko, alifanya na alikwenda kinyume na Sheria, lakini unaweza ukawa na hayo mawazo hata sasa hivi, unajua kabisa kwamba, hiki nachofanya navunja sheria lakini unaweza ukawa na hayo mawazo. Kwa sababu haiwezekani, hawa watu wameingia mikataba, hii mikataba ndiyo ambayo inatukwamisha. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini hii mikataba hailetwi basi iangaliwe upya? Au kama ni hivyo, kama kuletwa haiwezekani basi walau Serikali ipitie tena hii mikataba upya, kwa sababu hizi *exemptions* ambazo tunazisemea, haiwezekani tuzungumzie kwenye Taasisi za kidini ambazo tena hao wanatoa huduma na wanasaidia wananchi wetu huku kwenye madini tuweke *loophole* tu! Ninaomba sana, Serikali iweze kuliangalia suala hili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba kuzungumzia kuhusu utendaji Serikalini. Serikalini imekuwa ni kama kimbilio la watu ambao wanakwepa majukumu. Kuna *private sector* na kuna Serikali. *Private sector*, ukienda kwenye mabenki ya nje ambayo yako hapa nchini, hawa watu ni watu ambao wanakuwa na utaratibu kwamba kuwe na *performance report*, lakini huku Serikalini mtu anajiona kwamba, nikitoka kwenye *private sector*, nikienda Serikalini tena anasema kabisa, anajisifu kwamba, sasa hivi walau nitapumzika, kwa sababu huku unakaa unakula taratibu tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tunawalipa hawa wafanyakazi kwa kodi zetu, kodi za wakulima, kodi za watu ambao ni masikini, Watendaji wanakwenda kule wanakaa,

wanajifanyia kazi tena ni ile kwamba, kwa taratibu tu, wala mtu hana presha. Utaratibu huo lazima ubadilike kwa sababu, sasa hivi nchi yetu inakoelekea, hali ya uchumi imebadilika kwa hiyo kama tutaendelea na utaratibu wa watu kufanya kazi kama walivyozoea, haya mazoea ni mabaya sana.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, napenda niwatetee hawa Mawaziri kidogo kwa sababu, hawa Mawaziri hizi ni *political posts*. Wapo watendaji ambao Mheshimiwa Waziri, anaweza akawa ana wazo fulani kuboresha huduma fulani, anachukua lile wazo anapeleka kwa wataalam wake pale Wizarani, wale wataalamu wanapeleka kwenye *Cabinet Secretariat*, zinapita kwa *Chief Secretary* zinarudi kwake tena ndiyo wazo hilo linakwenda lakini wanaweza wakaamua tu kwamba, hiki kitu sisi hatukipeleki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Obama, Rais wa Marekani, wakati anaingia madarakani, alilingia na watu 3000. Mimi napenda kushauri kuptitia Bunge hili, Rais aweze kuwaondoa hawa watu, wameshakuwa ni kero, wanachosha watu. Hii huruma ambayo inafanyika sasa hivi, mtu anasema unajua huyu mtu ni Katibu Mkuu, lakini ametumikia hii nchi kwa muda mrefu sana, anastaafu baada ya mwaka mmoja, ngoja tumvumilie baada ya mwaka mmoja, hilo sikubaliani nalo, kwa sababu wanatuharibia nchi na tukiendelea na utaratibu huo, hatutafika.

Mheshimiwa Spika, Mahakamani mtu akibaka anaambiwa kwamba, tunakuhukumu miaka 30 iwe fundisho kwako na wengine wanaofikiria kufanya kitendo kama hiki. Sasa hii iwe na sisi kwetu, tuwaondoe hawa watu ili iwe fundisho kwa wale watu wazembe wengine waliobakia. Kwa sababu mtu anakaa mambo yale ya kulindanalindana tu, kwamba jamani unajua huyu mtu, ametumikia nchi hii vizuri sana, hata kama ametumikia, tunashukuru sana kwa huduma zako, tunaomba uondoke. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanachosha, wanachosha sana. Watendaji wetu ni wabovu, ni wabovu, ni wabovu sana. Matokeo yake tunakaa tunaanza kulaumiana hapa kwamba, jamani sijui barabara haziendi, sijui nini, sio wabunifu. Tulichozungumza mwaka jana, mimi mpaka wakati mwingine naona hata uvivu wa kuuliza swali, maana unauliza utajibiwa tu vilevile, unajua, eeh Serikali yetu bado inashughulikia, nani ambaye anashughulikia, ndiye anayekwamisha haya mambo?

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana sana sana Serikali, Mheshimiwa ukiwa kama Spika unaweza kuongea na Waziri Mkuu, una uwezo wa kuongea na Rais, hebu jamani mkikaa nao washaurini, washaurini kwa sababu haya mambo yanavyoendelea kuwa namna hii, hii nchi itaenda kubaya. Watu wana malalamiko mengi sana na watu kama wakiwa na malalamiko na hawa watu wanaendelea kuwepo, mbaya zaidi unaweza akatoka hapa akahamishiwa sehemu nyingine, unaweza akatoka Kusini akapelekwa sehemu nyingine. Anaweza akatoka Kilimanjaro, wanasema huyu tunampa adhabu anapelekwa Kusini au anapelekwa Rukwa, huo sio utaratibu! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy. Eeeh vijana mnatutia hamasa. Ujumbe wako, mzuri sana, ahsante sana. (*Makofi*)

Sasa namwita Mheshiwa Salim Yussuf Mohamed, atafuatiwa na Mheshimiwa Monica Mbega, wakati huo Mheshimiwa Salim Hemed Khamis ajiandae.

**MHE. SALIM YUSSUF MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nitoe mchango wangu mfupi katika bajeti hii ya Serikali. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama hapa leo mchana huu nikitoa mchango mdogo katika bajeti hii ya Serikali. Lakini niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na watendaji wake wote kwa kutuletea bajeti hii ambayo sasa hivi ndiyo tunayoishughulikia. Pia niwapongeze viongozi wa Kambi yetu ya Upinzani, kwa kuendelea kuleta mshikamano katika kambi yetu. Mbunge aliyezungumza sasa hivi alisema kwamba wananchi wanalamika, kumbe anajua sasa hivi kama wananchi wanalamika, lakini wananchi walilalamika zamani lakini nashukuru sasa wanajua kama wananchi wanalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kuhusu suala zima la Pato la Taifa na wastani wa pato la mwananchi Tanzania. Katika kitabu cha uchumi cha Mheshimiwa Waziri, kinaonyesha wastani wa Pato la Taifa limepanda na wastani wa pato la Mtanzania vile vile limeongezeka. Kwa mwaka huu tunaoumalizia wa 2008 ilikuwa ni Sh.624,259 kwa mwaka. Sasa unapofanya hesabu utapata kama wastani wa pato la mwananchi Tanzania ni karibuni shilingi 1,765/=. Sasa kwanza tuijulize sisi wenyewe humu ndani ikiwa kwa siku mwananchi pato lake ni shilingi 1,765/= hivyo anawezawezaje kuzitumia. Hebu tujitazame na tumwambie chukua hizi shilingi 2,000/= halafu utumie kwa kutwa moja, kwa kweli inashangaza sana. Sasa naiomba Serikali hapa kwa kweli izidi kuona aibu kidogo na kujaribu kurekebisha hii mipango lakini sasa wakati ule ule utazame huu ni wastani ina maana kuna wengine hawafikii hapo.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano mdogo tu, tulipokuwa shule, tulikuwa tunafanya mitihani na baadhi ya mitihani ilikuwa ni migumu na wengine tulikuwa tunakwenda mchomo sana, wengine wanapata *zero*, wengine wanapata moja, wengine kumi, lakini wamo wengine wanapata sabini, themanini hadi tisini na ikiwa wastani ni sitini ina maana hata yule aliyepata *zero* naye anaingizwa katika wastani kama amepata sitini. Sasa na hii ndiyo hali yetu ilivyo, ni vyema Serikali ilione hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi katika kitabu hiki alichokitoa Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, naomba kumnukuu, amesema:-

*“Kigezo kinachokubalika Kimataifa kuwa matumizi ya chini kabisa kwa mtu mzima asihesabiwe kuwa ni maskini wa kutupwa ni dola moja kwa siku”.*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa takwimu walizotupa Serikali ni kwamba sasa hivi kila Mtanzania anaishi zaidi ya dola moja. Lakini hizi ni takwimu zetu lakini ukweli ni kwamba na maelezo yaliyojitokeza humu, wananchi sasa hivi wana hali ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, hapo hapo aliendelea kusema kwamba Benki ya Dunia inakadiria kwa kutumia kipimo hiki yaani maskini wa kutupwa ni anayetumia chini ya dola moja. Umaskini Tanzania umeongezeka toka asilimia 73 mwaka 1990 mpaka kufikia asilimia 89 kwa mwaka 2000. Sasa kwa kutumia kigezo hiki cha Kimataifa na takwimu za uchunguzi wa Bajeti ya Kaya yaani *Household Budget Survey* wa mwaka 2007 yaani juzi tu zaidi ya Watanzania 90 katika kila Watanzania 100 ni maskini wa kutupwa. Sasa hii ndiyo hali halisi, sasa hii ina maana gani? Hawa watu 10 tu waliokuwa sio maskini wa kutupwa ndio wanaowabeba hawa 90. Sasa Serikali izidi kukiri kama zaidi ya wananchi wengi sana kwa kweli wana hali mbaya sana hasa tukitazamia kwamba wengi ni watoto, kuna wazee waliokuwa hawajiwezi tena, kuna wengine hawawezi kufanya kazi. Kwa kweli hii ni hali mbaya sana. Sasa tufanye nini?

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi waliozungumza hapa wamesema kwa kweli Serikali ina mipango mizuri tu, maandishi unapoyasoma ni mazuri tu, lakini utekelezaji haulingani na hali halisi ilivyo. Sasa nafikiri la kwanza, ni hilo kwamba utekelezaji sasa uende sambamba na maneno yanayotolewa hapa. Kila mmoja anasema bajeti ni nzuri, tokea nilipoingia hapa ni wachache tu wanaosema kama bajeti ni mbaya na hasa watu wa Kambi ya Upinzani. Kila mmoja bajeti ni nzuri, bajeti nzuri lakini sasa mwisho wa siku wanapokuja kuitathmini bajeti ile ile ya mwaka jana (uliopita) waliyoita nzuri utamwuliza wewe mwaka jana hukuwepo?

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Serikali imeunda Tume ya Mipango, kuunda Tume ya Mipango ina maana labda hii mipango yetu haitekelezeki. Sasa ni vizuri ile Tume ya Mipango ifanye kazi haraka kwa vile tunasema itakuwa ni *think tank*, ina maana itaweza kutuongoza katika mipango yetu na labda huenda tukafanikiwa. Lakini kwa hali hii inavyoonyesha sasa hivi matumaini ni madogo, nayasema haya makusudi Serikali ipate ari iyatekeleze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye kitabu hiki cha Matumizi ya Serikali *Volume II*, mwaka jana nilizungumzia kidogo kuhusu kitabu hiki ambacho kina kasma tofauti. Sasa nilipozungumzia kitabu hiki kulikuwa na kasma ya 26110, kasma iliyokuwa inazungumzia *other charges and services not classified above*. Kwa sababu katika kitabu hiki kuna kasma chungu nzima ya mishahara, marupurupu na halafu kuna kifungu cha mambo yaliyokuwa hayakutajwa. Sasa niliwahi kusema kwa kweli ni ajabu kama tunapitisha mambo ambayo hatuyajui. Namshukuru Waziri alipokuja akatoa ufanuzi na akasema atakiangalia tena kile kifungu, bahati nzuri sikukiona tena wakati huu, lakini katika maelezo yake alisema hivi, naomba kunukuu *Hansard* ya tarehe 20 Juni, 2008 majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

*“Tangu mwaka 1999 na mwaka 2000, Serikali ilianzisha kuainisha kasma za mapato na matumizi ya Serikali kwa utaratibu wa Kimataifa ambao unaitwa General Finance Statistics. Chini ya utaratibu huu, Serikali nyingi duniani, huanisha kasma zao kwa mfumo mmoja na kuziwezesha kasma hizo katika mafungu ya kiuchumi yaani Economic Clusters”.*

Mheshimiwa Spika, hili sina wasiwasi nalo hata kidogo wakati dunia inafuata mpango huo na sisi si kisiwa lazima twende kwa mujibu huo. Mapema kabisa katika Mkutano huu wa Bunge, Bunge lilitengua Kanuni ya kwamba tupunguze muda wa Mkutano huu. Miongoni mwa sababu ambazo tulizozipata na ni za kweli ni kuhusu mtikisiko wa uchumi duniani. Sasa katika hali hiyo nilidhani kwamba na Serikali itakaa chini katika kufafanua au katika kuyatazama mafungu yaliyomo humu ambayo kwa kiasi kikubwa yatakuwa hayana athari kwa utendaji wa Serikali aidha iyapunguze au iyaue kabisa. Kwa sababu pamoja na kwamba dunia inazungumza au inafuata utaratibu huu lakini kuna msemo unaosema “*Think globally but act locally*”. Bunge tuliona hiyo na sasa nilidhani na Serikali itafanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mnyaa jana alipochangia alizungumzia baadhi ya vifungu vinavyohusu safari za nje na ndani, akasema kwa kweli ilikuwa ni vizuri tufanye utaratibu kupunguza hizi safari za nje na ndani, zile tunazoziona hazina maana au zinapunguza kidogo ufanisi na akatoa kama shilingi 34.6 bilioni zinazotumika kwa safari hizo. Sasa pengine Serikali kama ingekaa na kutafakari ikapunguza, pengine hali ingekuwa nyine.

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, mimi nilitazama kuna kifungu kimoja, kuna kasma moja 210500 inayohusu *Personal Allowance In Kind*. Sasa kwa kitabu hiki nilichonacho *Personal Allowance In Kind* inazungumza kama ni fedha zinazotumika kwa chai na vitafunwa kwa watumishi wa Idara. Sasa kwanza naomba nielekewe, kunywa chai sio jambo baya hata kidogo, lakini inategemea wakati na ile hali yetu ilivyo. Sasa ikiwa utachukua hali yetu ilivyo sasa hivi, kuna haja kabisa kwa vifungu kama hivyo viondolewe kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mahesabu haraka haraka tu kwa mfano Wizara ya Kilimo, kwa kifungu hicho tu kinatumia shilingi milioni 226.3. Maliasili milioni 232.3, Wizara ya Fedha milioni 532, Wizara ya Elimu bilioni 3,432 lakini kwa vile muda unakwenda jumla Serikali imetumia kwa kifungu hicho tu karibuni bilioni 19. Sasa kwa mwananchi wa kawaida ambaye kwa kweli mapato yake ni mlo mmoja kwa siku, ukamwambia Serikali imetumia kiasi chote hicho kwa chai, kwa kweli ni kumuumiza sana. Sasa kwa kweli na mimi najiuliza hivyo hivyo, Serikali kweli itakuwa inamwonea huruma mwananchi lakini itakuwa inamwonea huruma za mamba. Nilipata hadithi kwamba mamba anapomla binadamu anatoka machozi kuonyesha kama anamwonea huruma lakini kumbe anamla. Sasa sijui kama ni kweli ama si kweli, kwa hivyo kwa kweli naiomba Serikali yetu ilione suala hili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye Tume ya Pamoja ya Fedha, ukurasa wa 19 kitabu cha bajeti. Mwaka jana tulipewa taarifa kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha namna inavyofanya kazi na hapa, pana *paragraph* moja tu na mwaka jana tuliambiwa Zanzibar kwa mgao wake itapata fedha kiasi gani, lakini wakati huu hatujaambwi kabisa. Lakini cha kusikitisha zaidi ni kwamba kila siku tunapiga kelele kuhusu mgao wa Zanzibar wa 4.5 ufanyiwe marekebisho. Cha ajabu ni kwamba michakato inaendelea, Serikali ya Zanzibar inapewa mgao ule ule mambo yako Baraza la Mapinduzi, mambo yako Serikali

ya Tanzania Bara, bado Mawaziri hawajakaa lakini suala la mafuta mwelekezi tayari na ameshachambua mambo yote na tayari mambo yamekwishakamilika. Hivi kweli kuna nia nzuri kwa uchumi wa Zanzibar kwa wenzetu wa Tanzania Bara? Kwa kweli, hili naomba Serikali iliangalie haraka na halafu atakapokuja Mheshimiwa Waziri naomba atuambie kwamba mgao wa Zanzibar kwa kipindi hiki ni kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, nimalizie suala zima la uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Kwa kweli Serikali inajitahidi kwa kiasi fulani lakini kutokana na kitabu hiki cha bajeti, ukurasa wa 20, Serikali ilihimiza wananchi kuanzisha *SACCOS* na nawapongeza wananchi kwa kuanzisha *SACCOS* tena kwa wingi sana, mpaka mwaka 2008 kuna *SACCOS* 4,780. Lakini kutokana na mpango huo wa kuwezesha kiuchumi, naomba kunukuu:

*“Mfuko wa uwezeshaji wa wananchi na mradi wa kuhudumia biashara ndogo ndogo yaani SELF kwa pamoja ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 68.58 kwa wajasiriamali 131,640 kupitia SACCOS 210 na vikundi 86”.*

Mheshimiwa Spika, sasa *SACCOS* 4,780 kwa mujibu wa kitabu hiki lakini zilizofaidika na mpango huu ni *SACCOS* 210, ina maana *SACCOS* 4,570 hawakufaidika na mpango huu. Hawa wajasiriamali ukitazama kwa haraka haraka utaona *figure* ni kubwa 131,000 lakini ukifanya hesabu ya ghafla ghafla kwa wastani wa kila Wilaya basi ni kwamba ni wajasiriamali 1,097 tu jambo ambalo kwa kweli ukiliona *figure* ni kubwa lakini mchanganuo ni mdogo. Sasa haidhuru Serikali inasema kama imepata mafanikio lakini ni madogo. Kwa hivyo, naomba Serikali wakati inapoamua jambo iliangalie, kwanza sasa *SACCOS* 4,570 hizi zilizokosa misaada, kwa kweli wananchi tutawavunja moyo sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli sina mchango mkubwa, nakushukuru sana ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Salim, mchango wako haukuwa mdogo.

Namwita sasa Mheshimiwa Monica Mbega, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na nadhani kwa mchana huu atakayeongea mwisho atakuwa Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Fedha na pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake, Katibu Mkuu na Manaibu wake, pia wataalamu wote wa Wizara hii ya Fedha na Taasisi zake zote, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu haya ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii, kwanza naomba nianzie na upande wa mapato, naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuongeza mapato. Serikali imekuwa ikipunguza baadhi ya kodi au kufuta baadhi ya kodi lakini wakati mwingine kuongeza baadhi ya kodi. Nadhani hili si jambo baya ni jambo jema kwa sababu kupitia hatua hizi mbalimbali tunakuta mapato yanaongezeka au yanaboreshwani.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ilikuwa katika upande wa vinywaji baridi katika kodi mbalimbali ambazo zimeongezwa katika vinywaji. Napenda kusemea katika vinywaji baridi kwa sababu vinywaji baridi vinagusa rika kubwa ambalo ni la vijana na watoto. Sasa kama tunataka kupata fedha nyingi zaidi nadhani si vizuri kuongeza kodi. Kwa mfano ukipiga hesabu kama ukichukua shilingi 54/= labda kwa watu milioni 10 wanaokunywa soda maana yake unapata milioni 540/. Ukiongeza kodi maana yake watu wengi wanapungua kunywa vinywaji vile na wanapopungua maana yake kodi ile sasa inapungua badala ya kuongezeka. Nadhani tungepiga hesabu vizuri, tungeona ingekuwa vizuri kodi ikapungua ili watu wengi zaidi ambao ndio rika kubwa tulilonalo la jamii watoto na vijana wanywe kwa wingi ili kodi nyingi zaidi iweze kuongezeka kuliko ilivyo sasa hivi unakuta soda zinanyewa wakati wa sherehe au wakati wa harusi au wakati wa misiba kwa sababu watu wengine hawana uwezo au kama mgonjwa yupo hospitalini ndio anapelekewa, lakini mtu mwingine hawezi kunywa kwa sababu soda sasa zimekuwa bei kubwa. Sasa kwa lengo la kupata kodi nyingi, ni vizuri kupunguza ili watu wengi zaidi wanywe fedha nyingi ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kupunguza kodi ya mapato kwa Makampuni ambapo ilikuwa asilimia 30 sasa hivi itakuwa asilimia 25. Lakini ombi langu hapa au ushauri kwa Serikali ni kwamba wafanyakazi wamekuwa na kilio cha muda mrefu sana kwamba kodi ya mapato au PAYE ni kubwa sana. Kwa hiyo, nashauri mwaka huu haiwezekani, lakini kwa mwakani basi iangalie katika kuleta motisha kwa mfanyakazi, kodi hii iweze kupungua na hii itawasaidia sana wafanyakazi kuweza kufanya kazi zao vizuri. Kwa sababu ukipiga hesabu, kodi anayolipa mfanyakazi kwa mwaka wakati mwingine inazidi maradufu hata kwa wafanyakabiashara wakubwa amba wanapata faida kubwa. Kwa hivi naomba sana na kwa kweli hiki ni kilio cha wafanyakazi kwa muda mrefu na nikiwa Mbunge, pia Mkuu wa Mkoa, kila nikipita kuongea na wafanyakazi, ombi lao kubwa ni hilo kwamba gharama za kodi ni kubwa sana katika mishahara yao. Kwa hiyo, naomba kwa mwakani iweze kutekelezwa kama ambavyo mwaka huu imepunguzwa kwa Makampuni. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia naipongeza Serikali kwa kuweza kuongeza kima cha chini cha pensheni. Kwa kweli hili ni jambo jema kwa sababu wastaifu wengi walikuwa na malalamiko makubwa na sasa Serikali imesikia kilio hiki. Lakini pia naomba nipongeza Serikali kwa kuweza kupunguza au kuondoa kodi ya ushuru wa asilimia 10 kwa dawa kwa sababu hiki nacho ni kilio cha madawa mengi kwamba bei yake ni kubwa sana wakienda hospitalini. Kwa hiyo, kwa kupunguza gharama hizi basi tunategemea dawa zitapatikana kwa bei rahisi lakini ninachoomba tu pengine usimamizi mzuri huko mahospitalini au kwenye mahospitali ya watu binafsi ili dawa hizi zisipande sana kwa sababu utafiti unaonyesha kwamba wakati mwingine Serikali imekuwa

ikipunguza kodi au kutoa kodi kwenye baadhi ya vitu, lakini wale wanaohusika, wafanyabiashara hawachukulii kwamba kodi hii imepungua na hivyo wapunguze bei. Kwa hivyo wanaacha bei vile vile na wananchi wanaendelea kuteseka wakati Serikali imechukua hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nashauri kwamba kwa upande wa madawa, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inazungumzia suala la wazee wakienda hospitalini wapate huduma bure au watu wasiokuwa na uwezo. Wazee ni wale kuanzia miaka 60 na kuendelea, lakini wale wasiokuwa na uwezo, mara nyingi wazee hawa wakienda hospitalini wanakosa dawa na wakati mwingine wanapata dawa lakini wakati mwingine wanakosa na wanatakiwa kwenda kuzinunua hizi dawa kwenye *pharmacy* au kwenye maduka ya watu binafsi. Sasa huyo mzee kama ameshapata msamaha wa kutokulipa gharama za hospitali je, atapata wapi fedha nyingine za kuweza kununulia hii dawa kwa mtu binafsi? Kwa hiyo, inaonyesha ni tatizo bado kwa huyu mzee au mtu ambaye amepewa ule msamaha. Naishauri Serikali kwamba Wizara ya Fedha wakishirikiana na Wizara ya Afya kuwe na utaratibu ambao utawezesha kama dawa hazipatikani hospitalini zinatakiwa zikanunuliwe kwa mtu binafsi basi zikishanunuliwa ile kadi au ile risiti ambayo ametumia kununulia irudishwe pale hospitalini na hospitali ikusanye vile vyeti ili vikalipwe na Serikali na hivyo kweli tutakuwa tunatekeleza Ilani ya kwamba huyu mzee anapata huduma ya bure. Bila ya hivyo inakuwa kwa kweli ni usumbufu na kwa kweli wazee wamekuwa wakilalamika sana kama Ilani yetu ya Uchaguzi haitekelezeki kwa upande wa wazee kwa sababu wakienda hospitalini dawa hawazipati na wanatakiwa kuzinunua na wakati huo hawana uwezo kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu upande wa kilimo. Napongeza sana utaratibu huu ambao umetokea sasa hivi wa kilimo kwanza. Ni utaratibu mzuri kwa sababu sasa hivi tumetekeleza kwa mfano mimi kwa sababu niko Serikalini tumeambiwa tununue *power tillers* 50 kila Halmashauri ili wananchi waweze kuzitumia na kwa maana hiyo kilimo kiwe na tija kwa sababu tunatakiwa tutoe jembe la mkono ili liwe jembe ambalo litamsaidia mwananchi kulima eneo kubwa lakini bila kuchoka sana. Sasa hili ni jambo jema lakini pia tuna suala hili la kuongeza sana ruzuku ya pembejeo. Sasa hili nalo ni jambo zuri ambalo natumaini hata wananchi wa Manispaa ya Iringa ambao huwa wakati mwingine wanaambiwa sio wakulima wakati ni wakulima watapata ruzuku kwa sababu ruzuku hii imeongezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu au ushauri kwa Serikali ni kwamba ruzuku hii najua wamezungumzia watu wengi sana kwamba ipatikane mapema lakini na mimi nasisitiza kwamba ipatikane mwezi Agosti. Mwezi Agosti, Mikoa ya Kusini Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma ndio kipindi ambacho wananchi wanavuna mazao yao, hii ruzuku ikitoka wakati huo maana yake wakulima watakuwa na uwezo wa kununua mbolea na kuziweka ndani na kwa maana hiyo sasa lengo la Serikali la kupata mazao ya kutosha au Tanzania kujitosheleza kwa chakula inawezekana kabisa. Mara nyingi wakati mwingine mbolea hii imekuwa ikichelewa au ruzuku hii imekuwa ikichelewa wakati inapokwenda wananchi wanakuwa fedha zile wameshazitumia na hivyo inakuwa ni shida kuweza kupata fedha nyingine na wanaanza kuhangaika na wakati huu ni kipindi ambacho vocha zimekuwa zikitumika. Kwa maana hiyo vocha zile zinakuwa hazina

maana zinakwenda wakati ambapo wananchi wamekuwa wameshaanza kulima au mvua zimeshanyesha na kwa maana hiyo hata ruzuku ya mbegu inakuwa haina maana tena. Kwa hiyo, ili kuleta mabadiliko tunahitaji mwezi Agosti ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu lingine kuhusu kilimo hiki kwa upande wa ruzuku hii, ni kwamba ipatikane kwa mwaka mzima. Sasa hivi unakuta inapatikana kuanzia mwezi Oktoba, ikifika mwezi Machi ruzuku ile inakuwa imekwisha, lakini kumbe kuna maeneo kwa mfano sasa hivi mimi ni Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Kilimanjaro mwaka huu hawakupata mvua kabisa, lakini wana maeneo ambayo wanamwagilia. Kuna *Lower Moshi* kule, Masame na Kirya kule wanamwagilia. Sasa nashukuru kwamba mwaka huu nilipopeleka maombi ya ruzuku hii iendelee kwa hawa watu wanaomwagilia Serikali wakakubali. Lakini sasa isiwe ni ombi la wakati maalum iwe ni kitu cha kudumu kwamba ruzuku hii itapatikana mwaka mzima ili maeneo yale ambayo wanamwagilia waweze kufaidika na mimi nadhani kama ruzuku hii itapatikana kwa mwaka mzima maana yake hata bei za mbolea hizi zitakuwa nafuu kwa sababu kutakuwa hakuna sababu kwa wafanyabiashara kuweza kungojea wakati ruzuku imekwisha halafu wao wapandishe bei. Kwa sababu wanajua ruzuku ile ipo kwa mwaka mzima na kutakuwa hakuna sababu yoyote mfanyabiashara aweze kuficha mbolea aje auze wakati anajua ruzuku ile ipo.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kilio kikubwa kwa sababu baadhi ya wafanyabiashara sio wote lakini baadhi ya wafanyabiashara ni watu wajanja sana. Pamoja na kwamba sasa hivi utaratibu umebadilika wa ruzuku lakini bado anaficha mbolea ili aje auze kwa bei kubwa wakati msimu ule wa ruzuku unakuwa umekwisha. Sasa kwa sababu tumeshaongeza ruzuku hii kwa kiwango kikubwa sana sasa hivi basi mimi naona ni vizuri iwe mwaka mzima na hivyo wananchi watafaidika, maeneo yote watafaidika yale ya umwagiliaji na wakati ambapo mvua hainyesi basi kilimo cha umwagiliaji kitasaidia sana na wale wanaomwagilia basi waweze kupata mbolea hizo ili tuweze kuongeza Uzalishaji na mimi nadhani tukiongeza uzalishaji kutakuwa hakuna haja ya kuzuia wananchi wasiende nje ya nchi kuuza chakula.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Wakuu wa Mikoa tumeshaambiwa usiruhusu chakula kitoke nje. Lakini unapozuia chakula kisitoke nje ya nchi maana yake unazuai wakulima wasilime zaidi kwa sababu motisha ni kuuza ili wapate fedha zaidi. Kwenye kitabu hiki nimeona kuna suala la kutafuta soko la wakulima. Soko la wakulima haliwezi kupatikana kama hakuna motisha ya kuwafanya walime zaidi. Kwa hiyo, walime zaidi wapate soko na soko hilo lisiwe tu ndani mahali popote ambapo inawezekana waruhusiwe kuuza ili kusudi iwe motisha kwao ya kulima zaidi. Kutakuwa hakuna haja ya kusimamia limeni, limeni kwa sababu anajua kabisa kwamba akilima akipata anauza mahali popote iwe ndani ya nchi au nje ya nchi. Sasa hivi kwa mfano Mkoa wa Kilimanjaro hamna chakula kabisa najua wananchi wa Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma ni fursa nzuri kuleta chakula Kilimanjaro ili watu wapate chakula na hivyo waweze kufaidika. Kwa hivyo, tusizuiusafirishaji wa chakula ili kusudi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, mwisho tumetengua Kanuni inayohusu uchangiaji, Waziri amepata muda mfupi wa kuweza kujibu hoja mbalimbali. Kwa maana hiyo,

inavyoelekea hoja nyingi zilizopo hapa ndani zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa jazba na kwa uchungu mkali, hazitaweza kupata nafasi ya kujibiwa kutokana na muda uliopo. Nashauri hasa kwa suala hili ambalo limekuwa ni *discussion* kubwa hapa kwetu Bungeni lakini kwenye magazeti kwa maana ya wananchi na hasa yakihuisha viongozi wa dini, suala la kutoa msamaha huu wa baadhi ya bidhaa zinazoagizwa za Mashirika ya Dini au NGO's, umekua ni mjadala mkali ambao unataka kutugawa kwa kufuata dini. Maana kuna siku nilikuwa nasilikizamu mmoja anasema:-

*“Tunapochangia hapa ndani tusimuangalie yule mto hoja”.*

Mheshimiwa Spika, sasa mto hoja mimi nikimuangalia ni Muislam na mimi ni Mkristo maana yake sasa tunaanza kupambana kwa namna ya udini. Nadhani hatutakiwi kuipeleka nchi yetu kwenye masuala haya. Mimi ninavyoona masuala yote yanayoletwa hapa Bungeni yanapita katika Baraza la Mawaziri, lilijadaliwa kwa ngazi zote zinazokubalika na ndani yake kukiwa na Wakristo au Waislam au mtu asiyekuwa na dini. Sasa tunapoanza kuchangia kwa kusema kwa sababu kaleta Muislam basi inakuwa ni nongwa, tutaanza kuipeleka nchi yetu mahali ambapo si pazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu suala hili limekuwa ni kubwa na linataka kutishia nchi yetu, ninashauri kwamba Waziri atoe maelezo mazuri sio wakati wa kujibu hoja; wakati wa kujibu hoja ni muda mfupi sana, kuwe na wakati pekee wa kujibu hoja hiyo vizuri kwa sababu inavyoelekea sio bidhaa zote ndiyo zimefutiwa hizo msamaha. Kwa hiyo, atoe maelezo ya kina kinagaubaga kila mmoja aweze kuelewa ili kufunga mjadala huu katika nchi yetu na kuleta amani la sivyo tutaanza kugombana pasipo kuwa na maana yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu alietujalia kufanya haya tunayoyafanya leo.

Pili nakushukuru wewe kwa kunipa ruhusa ya kuchangia asubuhi ya leo. Tatu namshukuru Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake wawili na wataalamu wake kutuletea bajeti hii. Nne, nampongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa hotuba yake nzuri. Lakini tano, namshukuru kwa shukurani maalum, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani; hotuba yake nzuri sana, ambayo nikiri kwamba kwa miaka mingi sijawahi kuona hotuba nzuri kama hiyo. Nawashahuri na ninawasihi, Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wote, muisome, muitafakari na muifanyie kazi kwa sababu itawasaidia katika chama chenu na Serikali yenu ya CCM na kufanya maisha ya Tanzania bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze na msamaha wa kodi, ambao amemaliza nao Mheshimiwa Mbunge. Tanzania inapoteza pesa nyingi kwa sababu ya kodi, sitaki niende mbali sana kwa sababu, tunajua athari za msamaha wa kodi katika uchumi wetu lakini nataka ni *substantiate with figures and examples*. Nataka nitoe mifano ya *figure* na mifano ambayo ipo. Kuna wafanyabiashara, wanajisajili katika *TIC*

(*Tanzania Investment Centre*), kwamba wao ni wachimbaji madini. Baadaye wanunuua ma-*bulldozer* mabovu na matrekta, wanakwenda milimani kule, wanasema wao ni wachimba madini. Wanasubiri msamaha wa kodi, wakipata mafuta, wanawauzia wananchi kwa bei ya soko; wanatengeneza hela nyingi sana. Watu hao ni wa miaka mingi, wanajulikana, lakini Serikali iko likizo. Tunaomba hatua zichukuliwe, ili wale wasiohusika na misamaha, wachukuliwe hatua mara moja za kunyimwa fursa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuna asasi mbalimbali ambazo nataka nizitolee mfano, zinafaidika na msamaha wa kodi ambao pengine wengine hawastahiki. Lakini, hayo ni makundi. Kwanza kuna Mashirika ya Umma, yanasamahewa kiasi ya bilioni 5.9, Taasisi za Serikali, bilioni 8.8, Taasisi za kidini na zisizo za kidini milioni 34.7, miradi inayogharamiwa na wafadhili bilioni 21.2 na *TIC*. *TIC* ambao humu kuna wachimbaji wa madini na wengine, huko ndio kwenye balaa huko. Wao peke yao wanachukua asilimia 83 ya msamaha wa kodi. Lakini nimesikitishwa sana na Zanzibar kama nchi, ambayo, imesamehe kodi ya shilingi bilioni 18.38; katika nchi ambayo inakusanya bilioni 28. Hii ni kwa kipindi baina ya Julai 2008 na Aprili 2009. Sasa utaona ni kwa kiasi gani athari hii imetokea, ya kusamehe kodi pengine kwa watu ambao hawatusiki. Kwa hiyo, mimi ninaishauri Serikali, isimuonee haya mtu wala Taasisi, wale ambao kisheria, hawaruhusiwi kusamehewa, wasisamehewe. Ingawa Nyerere alitufundisha hivi, akasema:-

“*na wavisavigoroweri, akrikimbora*” maana yake ni kwamba ukifichaficha maradhi kilio kitakufichua, Wazanaki watanisahihisha kama nimekosea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tujaribu kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria kwamba wale ambao hawatusiki na misamaha, wasisamehewe kwa sababu inatia dosari katika uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nataka nichangie kuhusu kilimo kwanza. Inaelekea Watanzania wengi na baadhi yetu tuliyomo humu, hamjafahamu hasa hii *concept* ya kilimo kwanza. Kilimo kwanza ni *concept* ilikuja katika mkutano uliyofanywa kule Kunduchi na Baraza la Taifa la Biashara tarehe 2-3 mwezi huu ambao na mimi nilihudhuria. Wale waliona kilimo hakijapewa msukumo wa kutosha wakataka pale kukusanya watu wa *sector* mbalimbali watoe mawazo ili waondoke na mikakati na maazimio na michango ilikuwa mikubwa na mikakati ilipatikana ya kutosha na sasa hivi inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa ile kauli mbiu yao ilikuwa ni kilimo kwanza kwa sababu kilimo hakikupewa msukumo wa kutosha. Wizara ya Fedha nayo ikachukua kauli mbio hiyohiyo kilimo kwanza na unaposoma bajeti lugha iliyotumiwa inaonyesha kana kwamba sasa hivi kilimo kimepewa kila kitu kwa hiyo watu wamefurahi sana. Lakini kuna watu ambao wamesema kuna sura za kisiasiasa, ninakubaliana nao, kwa sababu utasemaje ni kilimo kwanza wakati hujaipa kilimo ile haki ya kuwa kilimo kwanza, huwezi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika kwa hiyo, ni kweli kwamba kuna sura ya kisiasa, tunatengeneza mazingira ya kisiasa. Lakini bado wakati haujafika wa kusema kilimo

kwanza kwa sababu kilimo kwanza ukipatie zile *inputs* zote za kufanya kilimo kwanza. Mheshimiwa Rais alijitahidi kutanguliza mambo ambayo yangefanyika, bilioni ishirini kwenye TIB (*Tanzania Investment Bank*) na wakulima sasa hivi wanauliza kuwa jamani dirisha la Benki limeshafunguliwa tayari maana yake tunataka kukopa. Lakini nasema kuna bilioni 20 za zana za kilimo, bilioni 20 za vifaa vyachakula, hayo ni mambo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatangaza lakini wakati wake bado. Lakini vilevile kuna taarifa rasmi kwamba kuna ile *stimulus package* ambayo inaelezea mkakati hasa wa namna ya kunusuru uchumi wa Tanzania dhidi ya mtikisiko wa uchumi wa Dunia. Sasa hii bado hatujaifahamu vizuri Mheshimiwa Waziri atupe maelezo hii *stimulus package* iko vipi ambayo nadhani Mwenyekiti wake ni Meneja wa Benki Kuu ya Tanzania, ndio wanaofanya mkakati huu. Kwa hiyo, kilimo kwanza maana yake ni huo wakati ukifika tutajadili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa niingie kwenye kuchangia hotuba yenewe. Katika Mpango wa Maendeleo wa 2009-2010, kuna vipaumbele kama kumi hivi, lakini mimi nitavizungumzia viwili tu. Cha kwanza kinasema, kuhimiza matumizi ya zana za kilimo katika uzalishaji, usafirishaji na usindikaji. Suala sio kuhimiza matumizi ya zana za kilimo, nani hajui kama jembe la mkono halimsaidii mkulima wa leo? Nani hafahamu kama trekta, ndio njia pekee ya kukuza kilimo chetu? Suala ni kwamba, hayo matrekta, hayo ma-*power tillers* yatapatikanaje?

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pembejeo mwaka jana, ulitoa matrekta makubwa 99, na *power tillers* 27, katika nchi ambayo ina Watanzania karibia milioni 40; tuseme milioni 20 ni wakulima, hayatoshi. Mwaka huu katika bajeti, kuna shilingi bilioni 700, kwa wingi unaweza kununua matrekta 20, bado mchango wa *mechanization* katika kilimo chetu ni mdogo mno lakini kama kwamba hiyo haitoshi, sasa, upatikanaji wake ndiyo tatizo. Ili kupata trekta, lazima uwasilishe hati ya nyumba au ya shamba, bila hiyo hupati trekta. Ninayo taarifa kuna Mawaziri humuhumu, wameomba mkopo wa matrekta; hawakupata kwa sababu nini, kwa sababu hawana hati ya nyumba wala ya shamba. Sasa ikiwa Waziri hakupata, bibi mkulima wa pamba kule Bariadi inawezekana kupata? Bibi mkulima wa korosho atawea kupata? Haiwezekani! Kwa hiyo upatikanaji wake kwa kweli, ni mgumu mno.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa pili, ninashauri Serikali ijaribu kutafuta *power tillers*. Tunayo taarifa kwamba *power tillers* zinapatikana kwa bei rahisi sana kule China. Lakini wajanja wanazinunua kule, zinauzwa kiasi cha bilioni moja na nusu mpaka bilioni mbili lakini zikifika hapa, Dar es Salam zinauzwa bilioni 6 mpaka 7 lakini ukienda Mikoani huko inafika bilioni 10 na zaidi. Mimi nashauri Serikali, iende kwenye *base*, kwenye *source*, inunue *power tiller* zile, kwa sababu wakulima wamezipokea, wamezitumia, halafu zikija hapa ziuzwe kwa bei nafuu. Lakini kwa sababu China ni marafiki zetu, kwa nini tusiwaombe basi kujenga kiwanda hapa cha ku-*assemble* hizo *power tillers*, tununue *engine*, tu *assemble* hapa hapa ili iwe rahisi sasa kwa kila Mtanzania kutumia *power tillers*. Unaweza kupata pengine kwa shilingi milioni 3 badala ya milioni 7 au 10. Ushauri wangu kwa Serikali, ushauri wa bure.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni Serikali kukuza maendeleo ya viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Hili ni sawa lakini sasa hivi ni kukuza maendeleo ya viwanda, hasa mkakati huo upo vipi? Kilimo bila viwanda, si kilimo, hakiwezi kuendelea. Lazima kilimo kiwe na viwanda ili kuongeza thamani ya bidha za kilimo. Tanzania, mwaka jana ilisafirisha ngozi ya thamani ya bilioni 21, kama tungetengeneza viatu hapa, kwa ajili ya Majeshi yetu yote, tukasema Wanajeshi lazima wavae viatu vinavyotokana na ngozi ya hapa, wanafunzi wote, nafikiri tungepata faida zaidi, lakini tumesafirisha ngozi zile, zimekwenda China.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna wakulima wa korosho. Korosho zinanunuliwa kwa bei chini, bila kubanguliwa zinakwenda kule, India na China wanapeleka Ulaya, wanazibangua vizuri kwa hiyo wanapata bei kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine la haraka haraka, nizungumzie juu ya program hizi za kilimo. Wizara ya Kilimo ina *program* nyingi sana. Kuna *ASDP*, *program* ambayo ilikuja kwa vishindo hapa, mradi wenye trilioni 2.7 kwa miaka 7, kuna *PADEP*, kuna *DASIP*, kuna programu nyingi nyingi. Kuna utitiri wa *program* za maendeleo za kilimo. Sasa hii *program* ambayo tulifkiria kwamba ingeisaidia kilimo ya *ASDP*, kwa kweli imefeli kwa kiasi fulani. Kwa sababu huu ni mwaka wa tatu, ningetegemea kwamba labda tungekuwa kama kwenye asilimia 20 hivi ya utekelezaji, lakini tupo kama asilimia saba tu. Lakini zaidi kama ukienda, vijijini, huwezi kuona mambo mengi ambayo yamefanywa na *ASDP* tofauti na *PADEP*, *PADEP* ukienda mpaka Pemba utaikuta.

Mheshimiwa Spika, hasa kwa sababu mradi huo tunaoutegemea una pesa nyingi sana, mwaka huu tu una bilioni 21, wakati *PADEP* wana bilioni 2 tu, kwa hiyo, nafikiri kwamba iko haja sasa ya *ku-shift emphasis* kutokana na hii miradi ambayo haifanyi vizuri, kuipeleka kwenye miradi ambayo inafanya vizuri. Tatizo lipo katika Halmashauri za Wilaya, hakuna *coordination* baini ya Wizara na Wilaya. Kama hili limeshindikana, mimi sisemi *D by D* ni sera mbaya, lakini utekelezaji wake sio mzuri; kupeleka madaraka kwa wananchi ni nzuri, lakini utekelezaji wake sio mzuri. Kwa hiyo, hili likishindikana basi tulipeleka kwenye *PADEP*, programu ambayo inafanya vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa kwa sababu ya wakati, nizungumzie MKUKUTA, MKUKUTA umefeli. Tukubali sote.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti hii iliyopo mbele yetu nikiwa kama kitinda mimba kwa kipindi cha asubuhi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri, hotuba aliyotoa Waziri kwa kweli imetia moyo, nawapongeza sana pamoa na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioshiriki kuanda bajeti hii.

Vilevile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya tarehe 10 aliyotoa kwa Wazee wa Dodoma pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kweli hotuba ilikua nzuri kwani ilitoa mwelekeo mzima wa bajeti katika kipindi hiki cha mtikisiko wa uchumi wa dunia. Baada ya pongezi hizi, sasa nianze kutoa mchango wangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwenye mchango wangu kuna maeneo ambayo nitakua mkali kidogo lakini ni kwa nia njema tu kwa maslahi ya wana-Singida na Watanzania kwa ujumla. Takwimu za Serikali zinaonyesha kwamba Mkoa wa Singida, ni Mkoa wa kwanza kwa umaskini, takwimu ambazo hazifurahishi, mimi mwenyewe hazinipi furaha kabisa hata Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Singida haziwfurahishi na wananchi kwa ujumla haziwfurahishi. Napenda kuihoji Serikali, kutokana na tatizo hili la Singida kuwa Mkoa wa kwanza kwa umaskini, kupitia bajeti hii, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inatutoa huko?

Mheshimiwa Spika, ninauliza hivyo nikiwa na maana kamili kabisa. Kuna Mikoa mitano hapa imepewa ruzuku ya ziada katika kilimo ili iweze kuzalisha zaidi. Kama kweli Serikali inataka kuwa *fair*, basi ingeangalia ile Mikoa ya mwisho kiuchumi ukiwemo Mkoa wa Singida, Lindi na Mikoa mingine angalau Mikoa mitatu ya kwanza kwa umaskini tunyanyuliwe kidogo kwa kutengewa ruzuku ya ziada kuhakikisha tunanyanyuka kidogo. Sidhani kama kuna mtu anayependa kuitwa wa mwisho kwa umaskini. Ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho, aniambie ni kiasi gani amejipanga kuhakikisha Singida tunaondoka huko. Hakuna mtu anayependa kuwa wa mwisho kwa uchumi. Kwa hali ya uchumi ya uchumi wa Singida ninavyofahamu na watu walioko Singida, sitarajii kuwa watu wa mwisho. Hata ukiangalia Wabunge wa Mkoa wa Singida, nikisema wasimame ukiwatuma kwenda kuomba chakula hawatapewa. Ni watu ambao tuna afya nzuri kabisa tunaonyesha watu ambao tumetosheka kabisa na watu wetu wako hivyo hivyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo napata wasiwasi kwamba takwimu za nchi hii labda sio sahihi. Ukiangalia Singida kuna wananchi wafanyabiashara, tunazalisha kuku kama kazi, tunailisha Dar es Salaam, lakini siamini kama kuna takwimu zinazowekwa na wafanyabiashara hawa wa kuku. Bado tunawafugaji wazuri, Mkoa wa Singida, tunasafirisha ng'ombe, sidhani kama hawa wafugaji wanatakwimu kwamba wanaauza ng'ombe kiasi gani. Tuna wakulima wazuri Singida, sidhani kama hawa wakulima wana takwimu za kutosha, wanazalisha mazao kiasi gani, wanaauza mazao kiasi gani? Tuna vitunguu, tuna alizeti, tuna ufugaji wa nyuki, ninaomba sasa kupitia bajeti hii kuwe na fungu lililotengwa kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi waanze kuweka takwimu zao vizuri kuanzia leo kama kweli tunataka kupata takwimu za mwaka 2012 vizuri. Kikubwa ni takwimu ziwekwe vizuri. Nina hakika, takwimu hizi zikikaa vizuri, Singida huko mwisho hatupo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, naomba nizungumzie suala la kilimo. Kwenye kilimo, mimi nitazungumzia masuala mawili tu, zao la alizeti na pamba. Kabla ya kuzungumzia hayo mazao mawili, napenda kutoa angalizo kwa Serikali. Kauli mbiu ya Serikali, ni Kilimo kwanza. Lakini ukiangalia kwenye bajeti, kilimo hakijapewa

kipaumbele kwa fedha kama elimu, miundombinu, afya na maji. Sasa tunaposema kilimo kwanza wakati bado hujamwezesha huyu mkulima kwa kumpa fedha za kutosha, hii kauli mbiu inaenda vizuri jamani? Hii kauli mbiu naomba tuitekeleze vizuri mwaka kesho. Bajeti ya mwaka kesho wekeni kilimo namba moja, lakini namba moja bado ni elimu. Ninahakika tukiwa *serious* na kilimo tutaweka bajeti ya kilimo kuwa ya kwanza. Hilo ni angalizo langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya angalizo hilo, sasa naomba nizungumzie zao la alizeti. Alizeti ni zao ambalo linalimwa mahali pengi hapa Tanzania ukiwemo Mkao wa Singida. Wananchi wamejitolea kulima kweli kweli zao hili. Singida mwaka 2006, tulizalisha tani 28,000, mwaka 2008 tukazalisha tani 130,000 na mwaka huu tunategemea kuzalisha zaidi ya tani 140,000, hii inaonyesha ni jinsi gani wananchi wamejikita katika zao la alizeti. Zao hili ndiyo hili ambalo linazalisha mafuta. Lakini mafuta ya Singida bado ni utata. Mheshimiwa Merry Nagu Waziri wa Viwanda alituambia atatuletea mwekezaji aweke kiwanda cha kusafisha haya mafuta ili yaweze kuingia katika soko la ushindani. Mpaka leo hii, mafuta haya bado hayajaweza kusafishwa ili yaweze kuingia katika soko la ushindani. Serikali hii itakua inasema tu bila kutekeleza? Tunaomba huyo mwekezaji tuletewe ili mafuta yetu yaweza kuingia katika soko la ushindani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafuta haya ya alizeti mnayafifisha sana pale mnapotoa kipaumbele katika mafuta ya nje. Mafuta ya nje mmeondoa VAT, hivi mnategemea nini hapa? Serikali inategemea nini? Mafuta hayo ya nje kama yameondolewa VAT ina maana yataingia kwa urahisi, yatakuwa yanauzwa kwa bei nafuu sana sasa haya mafuta ya alizeti yatapata soko? Utamlisha mtoto wa mwenzio ukaacha wa kwako. Jamani macho yetu yaangalie ndani kwanza. Tumkomboe mkulima wa Tanzania kwanza, ninaomba sana. Kama kweli tunataka kumwezesha huyu mkulima anayelima alizeti, tuhakikishe mkulima huyu anathaminiwa, mafuta haya yanapata soko na kupata soko ni kurudisha VAT kwa mafuta ya nje ili yasije yakazidi mafuta ya hapa kwetu. Rudisheni VAT mafuta ya nje, yasije yakayameza mafuta yetu yakakosa soko maana watumiaji wanapenda kitu cha rahisi. Baada ya kusema hilo, ninaamini kabisa Serikali itaona umuhimu wa soko la mafuta na yatapewa kipaumbele na hayo mafuta ya nje yapewe VAT ili yasije yakaharibu soko la mafuta ya ndani.

Mheshimiwa Spika, baada ya zao hilo, naomba niongelee pamba. Wanasingida wanalima pamba sana. Miaka ya nyuma sisi pamba tuliiacha na tuliiacha kwa sababu ya bei. Lakini Mkoo wa Mkao, Mheshimiwa Kone, amehimiza na wananchi wamekubali wamelima pamba. Sasa soko la pamba bado utata. Ninaishauri Serikali iweke ruzuku ya pamba kufidia hasara ya pamba. Pale soko linapokuwa baya Serikali ifidie ili isimvunje moyo mkulima. Mkulima aendelee kupata nguvu na uwezo. Bila kufidia soko la pamba na Mtanzania akiacha kulima pamba leo basi atakuwa amekata tamaa jumla. Ninaomba soko la pamba lipewe kipaumbele kwa kutengewa ruzuku ya pamba, tukifanya hivyo, tutakuwa tumemsaidia mkulima wa pamba na watapata moyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongelea hilo, naomba niongelee kiwanja cha ndege cha Singida. Nashukuru Serikali imesaidia kiwanja hiki cha ndege kimekarabatiwa, kina urefu wa kotosha, kina-*run way* nzuri, ndege zinaweza zikaruka na

kutua bila tatizo lakini kiwanja hiki ili kiweze kutumika hata kwa ndege za biashara, tukiweke lami. Nimefutilia bajeti hii sijaona hela yoyote iliyotengwa kwa ajili ya kiwanja hiki. Kama kweli tunataka kuitoa Singida kwenye umaskini tupeni hata kiwanja cha ndege ili wawekezaji waje. Ndege zinazoenda Shinyanga, Mwanza, zitatua Singida. Mheshimiwa Waziri wakati unatoa majumuisho, hebu hakikisha unatamka pesa za kiwanja cha ndege cha Singida, tunaokuomba. Ukifanya hivyo, utakuwa umetukwamua, bila kututengea hata kidogo, hatutakuelewa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, nizungumzie kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu Singida. Niliambiwa hapa kupitia swali langu mwenyewe kwamba jamani Singida kesi za mauaji ni nyingi wananchi wanapata tabu kuja Dodoma kufuata Mahakama Kuu ama Majaji kusubiri mpaka waende Singida ni muda mrefu tujengeeni Mahakama Kuu. Kweli Mheshimiwa Waziri kwa heshima kabisa kakubali na wanasingida tukaitikia vizuri na Mkuu wa Mkoa wetu anapenda kuitikia mambo vizuri kabisa. Tukatenga Kiwanja na tukaanzisha shughuli za ujenzi lakini ndani ya bajeti sijaona hata senti tano ya kujenga Mahakama Kuu Singida. Ninaomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho atumbie huu mkakati wa ujenzi wa Mahakama Kuu upo au umekufa, tuambiwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Diana Chilolo. Waheshimiwa Wabunge, zimesalia kama dakika moja tu na nusu zinaniwezesha kutoa matangazo kama ifuatavyo:-

Mara baada ya kusitishwa kikao hiki cha mchana, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, wanaombwa wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge wamesalia wachangiaji kumi na tatu, saa kumi na moja tutaweza kuwasikiliza wachangiaji kumi na moja mpaka kufikia saa mbili kasarobo. Kesho asubuhi wawili na baada ya hapo nitaanza na Manaibu Mawaziri wa Wizara hiyo husika hatimaye Mtoa Hoja Waziri. Kwa faida tu ya kuelewa ili wajiandae watakaongea kuanzia saa kumi na moja, wa kwanza ni Mheshimiwa James Musalika, atafuatiwa na Mheshimiwa Alhaji Athuman Janguo halafu Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Daniel Nsanzungwanko, Mheshimiwa Wilson Masilingi halafu Mheshimiwa Basil Mramba na hatimaye Mheshimiwa Anastazia Wambura. Kesho asubuhi ni Mheshimiwa Damas Nakei na Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Basi baada ya tangazo hilo, kwa kuwa muda umefika, basi nasitisha Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 7:00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni*)  
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

*Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## **HOJA ZA SERIKALI**

(Majadiliano yanaendelea)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano na mzungumzaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'wale na Mheshimiwa Athuman Janguo ajiandae.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii mchana huu ili niwe wa kwanza kuzungumza katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyang'wale, napenda kutoa shukurani sana kwa Ofisi ya Spika, hususani Spika mwenyewe, Katibu wa Bunge, Dr. Kashillilah, Mama Kippa pamoja na watalaan wengine Watendaji wa Ofisi ya Bunge, kwa namna walivyosaidia kumuuguza Ndugu yetu, Mheshimiwa Marehemu Kabuzi na hata alipozidiwa kumpeleka India na hata baada ya kuaga dunia waliweza kushirikiana na Serikali kusafirisha mwili wake mpaka Jimboni ambako mazishi yalifanyika, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru sana Viongozi wa Wilaya ya Geita, wakiongozwa na Chama Cha Mapinduzi Wilayani, kwa kusimamia shughuli yote ya maziko ambayo yaliisha vizuri. Lakini napenda niwashukuru sana kwa namna ya pekee, wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kuchagua tena Mbunge wa CCM, Mheshimiwa Lollesia Bukwimba ambaye wamempa kura nyingi sana. Tunawashukuru sana wananchi wa Busanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasikia kuna watu sasa hivi wanapitapita huko wale ambao walipoteza kwenye uchaguzi huo, wameanza kupita huko sasa hivi wakati Lollesia yuko hapa Bungeni, sasa wewe mwanamke ameshaolewa, mumewe kaenda kwenye mafunzo, wewe unaanza kupita kwa mke wake na kusema ahsante sana, pamoja na kwamba hukunichagua mimi lakini *Inshallah* labda mwaka kesho, nadhani huu sio ustaarabu. Namashauri Mheshimiwa Lollesia aedeele na kazi hapa, apate mafunzo na mwezi wa nane anaenda kuanza kufanya kazi moja kwa moja Jimboni Busanda. Kwa wananchi wa Busanda nawashauri, hawa wawasikilize tu lakini wawatishe kwamba akija mwenyewe tutawasema, maana mtu akija kwa mkeo, akikwambia nitakusema, pengine anaweza akaogopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini huyu anayepitapita kule, ninamshauri kama anapenda sana Ubunge mwaka huu, upo ushauri mmoja wa bure nimpe na siri kubwa kwamba Mheshimiwa Kikwete bado ana nafasi mbili za kuteua Wabunge, kwa hiyo, anaweza akamwomba Mheshimiwa Kikwete kwamba mimi fulani, chama Fulani, napenda sana Ubunge mwaka huu, niteue basi katika nafasi zile mbili. Mheshimiwa Kikwete ni msikivu, ana huruma anaweza akampa lakini kule Busanda pamejaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme kwamba kuna mdudu mmoja, watu wa mifugo (*veterinary*) wanamwita *parasite* (kupe), kwa neno la

kawaida anaitwa *ticks* (kupe). Kupe ana kawaida ya kumng'ata ng'ombe na anamg'ata sehemu ambapo kuna mrija mzuri, mtiririko mzuri wa damu au maziwa na anaendelea kunyonya na anang'ang'ania hatoki, huyu ni *parasite*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dude linazungumzwa hapa ndani sasa wiki nzima linaitwa *TICTS*. Hii siyo ile *ticks* ya kupe, lakini ni kitengo cha kuhudumia makontena kinaitwa *Tanzania International Containers Terminal Services (TICTS)*. Wengine wameibatiza nayo ni *ticks* ambayo nimeisemea kwa sababu nao wana sifa zile zile kwa sababu wameenda kuuma sehemu nzuri ya uchumi, kwenye mtiririko mzuri kabisa wa uchumi bandarini, wakang'ang'ania na wakanyonya, ni *parasite*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Mkutano wa 15 wa Bunge uliopita, amewahi kusema kwamba Serikali sasa imechoka na matatizo ya *TICTS* na wanafikiria kuvunja mkataba, alisema hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu. *TICTS* ina utendaji mbovu sana ambao unasababisha kurundikana kwa makontena. Makontena yanaporundikana, athari zinazopatikana baadhi yake ni kama zifutazo, makontena yanarundikana na kukosekana kwa nafasi pale bandarini. Kwa mfano, mwaka 2006/2007, kulikuwa na makontena yanafikia zaidi ya 12500 kwa wakati mmoja. Lakini kurundikana huku pia kunaifanya bandari sasa ikose nafasi ya kuweka makontena mengine ya kupakua au kupakia na kwa sababu hiyo meli zinakaa muda mrefu sana pale bandarini. Kitu kingine ni kwamba sasa wafanyabiashara wanahama ile bandari ya Dar es salaam kama wengine ambavyo wamesema, mizigo ya Burundi, Rwanda, Uganda wanapitisha Mombasa na hata Watanzania wengine wanapitisha Mombasa na wale Wazambia wanakwenda Durban, Afrika Kusini ambapo nchi sasa inakosa mapato. Lakini pia bado wale ambao wana makontena pale wanatozwa gharama kubwa sana kulipia gharama ya kuhifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama bandari ingesimamiwa vizuri, ingeweza ikachangia bajeti ya Taifa kwa asilimia 100. Bajeti ya Taifa, ni triliioni 9.5, lakini bandari hii inaweza ikakusanya mpaka zaidi ya triliioni 10 kwa mwaka. Hali halisi ya pale kontena kwa sasa hivi, kwa takwimu za mwezi huu mwanzoni, kulikuwa na makontena ya kuingizwa nchini (*import containers*) kwenye 5300 na yale ya *export* ambayo ni ya kusafirisha bidhaa nchi za nje ili nchi ipate mapato, yalikuwa 690. Kwa hiyo, hata haya ya *export* hayapati nafasi ya kupakiwa kupelekwa nje ili nchi ipate mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeishaagiza makontena yahamishiwe kwenye bandari kavu lakini leo *TICTS* anapuuza agizo hilo wakati huo huo wako Watanzania ambao wamehamashisha na Serikali na kwa agizo hilo, wametumia rasilimali zao, wengine wamekopa Benki, wamenunua eneo, wamewekeza katika bandari kavu lakini *TICTS* sasa wanahodhi hiyo mizigo na wanahifadhi. Lakini ni nini yanayotokea baada ya *TICTS* kung'ang'ania biashara hii? Ni kwamba yako makontena ya aina mbili, kuna lile la futi 20 na la futi 40. Kontena la futi 20 linapokaa pale bandarini baada ya siku saba linaanza kutozwa dola za Kimarekani 20 na lile la futi 40 linatozwa dola za Kimarekani 40. Baada ya siku 21, kontena la futi 20 linatozwa ushuru (*storage charge*) ya dola za Kimarekani 40 na lile la futi 40 linatozwa mara mbili yaani dola 80 kwa siku. Kwa hiyo, ina maana kwamba *TICTS* wanajipatia pesa kwa mwezi mmoja (siku 30) kwa kontena moja la futi 40, wanapata dola za Kimarekani 2,400. Sasa hiki kiasi ndicho nafikiri

mgogoro unaanza hapo kwamba sasa wameona kuna biashara ambayo wananchi wanaumia na wameng'ang'ania hiyo kwa sababu ya biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa kwa nini tunafikia hapa? Wananchi sasa wanalia na kulalamikia *TICTS*, halafu *TPA* wanalia na kuilalamikia *TICTS*, Wizara ya Miundombinu inalia na kulalamikia *TICTS*, Kamati ya Miundombinu inalia na kuilalamikia *TICTS*, Waheshimiwa Wabunge hapa ndani wanalia na kuilalamikia *TICTS*, Waziri Mkuu amewahi kulia na kuilalamikia *TICTS*, kuna Kamati Teule ya Rais imeshawekwa pale kurekebisha mambo, lakini *TICTS* wanapuuza maagizo yake. *TICTS* ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua Duniani hakuna Mamlaka zaidi ya Rais, sasa hawa *TICTS* wanapuuza Mamlaka ambayo ni ya Rais, sasa wako juu ya Rais? Hawa ni nani hawa? Au ni pepo au ni majini? Kama ni majini waseme ili tumwambie Mchungaji Rwakatare ayakemee yalegee! Kwa sababu Bunge zima *TICTS!* (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatilia mashaka, kwa nini Serikali inalalamika, Baraza la Mawaziri linalalamika au ninyi wenzetu huko mmeishachukua kitu kidogo? Kama mmeshachukua kitu kidogo, mteme mzigo huo ni shubiri! Nawaambia Serikali kama mmechukua kitu kidogo huko, rudisheni hela za watu ili nchi itulie! Tumechoka na *TICTS* sasa, nadhani Waziri asingesubiri mjadala uishe, asimame na kuhitimisha suala la *TICTS* kwa sababu kila mtu analijua linanuka kwenye pua za watu, kwenye masikio ni tatizo. Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani niishie hapo kuhusu *TICTS.* (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la elimu. Serikali yetu imejitahidi sana kuhamasisha elimu na sasa hivi kila kata ina shule za sekondari. Lakini shule zote hizi zina upungufu mwangi sana. Kwanza, hazina mabara na hazina Walimu wa kufundisha masomo ya sayansi na kwa hiyo wanafunzi wote wanasoma masomo ya *arts* (sanaa). Mimi nimepitapita kule mara nyangi, unakutana na wanafunzi, unawauliza vipi mnasoma hesabu au sayansi au bailojia, wanakwambia kwamba hesabu haipandi! Sasa nchi nzima tunasoma *arts!* Kwa hiyo, ninaomba katika bajeti ambayo imeongezwa, Serikali ijenge maabara katika shule zote za kata, itoe motisha kwa wanafunzi wanaochukua masomo ya sayansi pamoja na Walimu wa wao kwa kuwaongeza posho, mishahara na nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hapa niseme, nina tatizo kwenye Jimbo langu. Kwenye kata ya ya Bukwimba, shule ya Bukwimba, wananchi wameniambia zilitengwa milioni 14 kujenga maabara, nilishamwambia Waziri wa Fedha, lakini Ofisi Ndogo, Hazina Mwanza ikishirikiana na Mkuu wa shule ile anaitwa Paschal Machibya, zile hela wamezifanya ubadhilifu, pale hakuna msingi wala jengo. Wananchi wameniomba nikirudi mwezi wa nane, kwenye akaunti ya shule hiyo kuwe na hizo milioni 14, halafu Waziri atajuana na Hazina Ndogo Mwanza pamoja na yule Mwalimu Mkuu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana *TANROADS* hasa Mkoa wa Mwanza kwa jinsi ambavyo wanatengeneza barabara nzuri sana kwenye Jimbo langu la Nyang'wale. Barabara zinapitika vizuri sana na zina upana wa kutosha na wananchi wanashukurru. Napenda niishukuru sana *TANROADS* kwa niaba yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana mradi wa umme wa *MCC*. Sasa hivi wakati natoka kule, walifanya *survey*, umeme sasa utatoka kwenye Machimbo ya Mgodi Kakola, utapitia Kharumwa, umeme utaenda Ikangala, Kitongo, utaenda Nyalubele, Nyijundu, Nyaluguguna hadi Nyang'wale. Vijiji hivi vitapitiwa na umeme, nadhani nyaya zitapita, halafu *TANESCO* wataweka taratibu za kuunganishia wananchi, napenda niwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kilimo kwanza, zile pesa ambazo zimetengwa, naomba ziwafikie wananchi. Kule vijana vijijini wapo wana maeneo ya kulima lakini hawana nyenzo. Pesa hizi ziwafikie vijana, wanaka kwenye jiwe. Ukifika, saa mbili wanacheza *pool* au wako kwenye *salon* au kwenye kahawa. Wapelekewe utaratibu wa hela hizi ili ziwafikie, maeneo wanayo, wasimamiwe kama walivyosimamia kujenga madarasa ya MMEM, wanaweza kwa hela hizi wakipewa mashamba ya Pamba, mahindi na mikorosho. Kwa hiyo, hela hizi wapewe, wapewe nyenzo, wapewe na pesa, halafu wasimamiwe. Wapo vijana, hawana kazi, ukifika saa mbili/tatu Mbunge wanakwambia hatujala Mheshimiwa, hatujala. Ni kweli hawajala, hawana kitu. Sasa wapelekewe hela hizi wazalishe pamba. Hasa ninapenda Nyang'wale na Wilaya ya Geita, Mwanza na Shinyanga wapewe hela hawa vijana ili wazalishe Pamba zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe masikitiko yangu makubwa sana. Kwanza, napenda nimpongeze Rais kwa kufikiria kupata ufugaji bora katika nchi, kwa hiyo akasema mifugo ipunguzwe tuache ule ufugaji wa kuhama hama. Lakini zoezi hilo limesimamiwa vibaya sana, Watendaji wa Serikali kuanzia Wakuu wa Wilaya na sehemu zingine Wakurugenzi mpaka Watendaji wa Kijiji wamechukua ng'ombe wa wananchi bila huruma. Sasa hivi Wakuu wa Wilaya na Watendaji, ni matajiri wa ng'ombe na wengi tunafahamu hapa. Wamechukua ng'ombe wa wafugaji ambao wamekusanya vizazi na vizazi, leo anakuja kuuzwa ng'ombe mmoja shilingi 20,000 badala ya 300,000!

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillahi Rahmani Rahim!* Kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi mchana huu na mimi kuwa mmojawapo kati ya wachangiaji wa hoja iliyopo mbele yetu. Kabla sijaendelea, kuna kawaida ya Dini ya Kiislamu kwamba, kila inapofika wakati wa swala huwa mnaitana kwa maana maalumu ya kukumbushana na kuhimizana kwa yale ambayo yanatakiwa kutendwa kwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti , kwa hiyo na mimi pengine nitakuwa narudiarudia si kwa lengo la kuvunja kanuni, bali kwa lengo na madhumuni ya kwamba, tunaitana na kukumbushana yale ambayo yapo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningeomba niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Timu yake, kwa hotuba hii ya bajeti ambayo iko mbele yetu. Mengi yamezungumzwa; pa kusifu watu wamesifu, pa kurekebisha watu wamerekebisha, lakini na mimi ningeomba kidogo nichangie sehemu kadhaa zinazohusiana na Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali, kuna baadhi ya Wajumbe hapa walipochangia kuhusiana na hali ya uchumi, walizungumzia kuhusu Zanzibar kwamba, bei ya karafuu iko chini. Kwa maana hiyo, wangeshauri kwamba wapewe fursa wananchi wenye, watafute soko na wauze.

Labda mimi kidogo niwe kinyume nao, ningeshauri kama wanajua masoko haya yapo na karafuu inaweza pata bei, kwa nini wasiambie Serikali ikaenda kuuza huko tukanufaika sote, kuliko kuwa na lengo la kusema uinufaishe sehemu moja tu ya jimbo lako. Kwa hiyo, ningeshauri sana wapeleke ushauri wao kwenye masoko haya ili tuweze kunufaika sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, niruhusu nizungumze kidogo kuhusiana na Tume ya Pamoja ya Fedha. Naomba ninukuu kidogo sentensi moja; katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, kuna kipengele alisema: “Serikali zote mbili zimekamilisha uchambuzi wa Taarifa ya Tume na sasa zipo kwenye taratibu za kupatiwa maamuzi na Serikali.” Katika ushirikiano kati ya Wizara ya Fedha ya SMT na SMZ; nanukuu tena: “Aidha, kufuatia majadiliano ya pande mbili, makubaliano yamefikiwa ya kuipatia SMZ asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti kuanzia mwaka huu wa 2009/2010.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kufuatia kauli mbili hizi, lakini ningependa kumshauri au kumtaka Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha anifafanulie; ana maana gani anaposema kwamba makubaliano yamefikiwa ya kuipatia SMZ asilimia 4.5 ya mikopo ya kibajeti na wakati Baraza la Wawakilishi nalo liko njiani kupitisha Bajeti yake? Je, makubaliano haya yamo katika Bajeti hii na kama yamo na inazungumzwa kwamba ni ya mikopo; je, utaratibu wa mikopo hii malipo yake utakuwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyoolewa kwamba, hali ya uchumi ya Zanzibar, Tanzania Bara na Ulimwenguni sasa hivi bado ni ngumu na tunakokwenda nako hatujui itakuwa vipi; kutokana na hii asilimia ya mikopo, tunapokuja katika malipo na Zanzibar hali yake kama tunavyoijua; je, Serikali ya SMT itakuwa na jukumu gani kwa SMZ katika kuhakikisha kwamba hatubakii na madeni halafu tukashindwa kuyalipa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza hivi kwa sababu katika hotuba hii vilevile Mheshimiwa Waziri alizungumzia kwamba, kunataka kuimarishwa Bandari. Katika kuimarisha bandari huku zikatajwa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Nasikiasikia tu kwamba, pengine inataka kujengwa bandari kule Bagamoyo ingawa haikutajwa hapa. Sasa ikiwa hii ndio hali halisi na pale Zanzibar bandari ipo; je, katika haya mashirikiano yaliyokuwepo na hali ngumu ya uchumi iliyokuwepo katika nchi yetu; makubaliano haya au matengenezo haya kama walivyozungumza wenzetu; yatafikiria bandari hizi za Zanzibar katika kukuza uchumi wake kwa ajili ya kuzidisha mapato ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo itajengwa bandari Bagamoyo; uhusiano wa bandari kati ya Bagamoyo ambapo ni karibu sana na Zanzibar; una utaratibu ambaopu

njiani wa kupanga na kuona kwamba tutaisaidia Zanzibar katika kipato chake kufuatana na hali halisi ya bandari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu elimu ya juu. Kama tunavyoolewa, elimu ya juu ni sehemu ya Muungano wa Jamhuri ya Tanzania na tangu tumeanza muungano mpaka leo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano bado haijajenga Chuo Kikuu kule Zanzibar. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejenga Chuo Kikuu kimoja ambacho kinaendelea, lakini kinachosikitisha ni kule kuona kwamba, kuna Taasisi ambayo iko chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Sayansi za Baharini (*Institute of Marine Sciences*), kila mwaka kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitano sasa, tunakuja mbele ya Bunge hili tunauliza kuhusu ukamilishaji wa ujenzi wake. Mpaka hivi sasa ninapozungumza, wakandarasi wa kujenga chuo hiki wanahamisha vifaa vya ujenzi kwa kukosa kulipwa hela za kuendelea na ujenzi. Nimejaribu kuvumilia, nimezungumza na Wizara na kuuliza maswali Bungeni hapa, lakini bado jawabu ambalo tunalipata linakuwa haliridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia Chuo Kikuu cha Dodoma kimeanza juzi, lakini kuna taasisi zaidi ya nne zinajengwa kwa utaratibu wa mikopo na hazijasimama hata mara moja. Leo kuna taratibu gani au kuna kosa gani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukosa udhamini wa fedha kidogo tu kulipwa mkandarasi kuimaliza ile Taasisi ya Sayansi za Bahari pale Zanzibar na wao wakajisikia kwamba walau tokea kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna taasisi iliyokuwepo chini ya Vyuo Vikuu vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba Mheshimiwa Waziri, pengine atusaidie au kama si ye ye basi atapokuja Waziri wa Elimu. Ningombwa sana, nielewe fedha zinazohusiana na Chuo hiki ziko wapi ili tuweze na sisi kunufaika na elimu ya juu kwenye vyuo vinavyohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nafikiri *ni-declare interest*; mimi ni Mjumbe wa *Tanzania Commission for University (TCU)*. Nimechaguliwa na Bunge hili hili. Juzi tulikuwa kwenye ofisi ya taasisi hii, tumehama katika jengo la kukodi. Cha kusikitisha ni kwamba, tumetoka jengo la kukodi tumeingia jengo la kukodi kwa hela nyingi zaidi na wakati kiwanja kipo na sijazona hela ambazo zimepangwa kwa ajili ya kusaidia ujenzi wa ofisi hizi. Nimejaribu kuangalia, sikupata uhakika hasa Serikali inasema nini kuhusu ujenzi wa ofisi hii. Tutaendelea kuwa tunahama majengo mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, vilevile Chuo Kikuu cha Muhimbili, kuna eneo linaitwa Mroganza, wenye lugha wanasema mroga njia; pengine hii njia imerogwa, kwa sababu na chuo hiki pia hatujaona kinavyofuutiliwa katika kuchangiwa fedha na ujenzi. Majengo yako pale, eneo liko pale, wanafunzi wanazidi kuja katika vyuo, lakini hatujaona jinsi gani watakavyoendelea na shughuli zao za kukiimarisha Chuo Kikuu cha Muhimbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningependa nizungumzie kuhusu mikopo ya Serikali ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Naishauri sana Serikali, tuangalie suala la mikopo ya wanafunzi, hela ambayo imetengwa naona ni kidogo sana. Lazima tujitahidi kutafuta kila kila kipengele, zipatikane hela za kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, sina zaidi isipokuwa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kwa kuunga mkono hoja. Kama nilivyosema, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia. Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mbunge wa Kisesa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kisesa. Naomba sasa nilihutubie Bunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa sana la Taifa hili, nimeipitia Bajeti ukurasa hadi ukurasa ila nataka kuweka tu sawa kwamba, Waziri wa Fedha, kila alipokuwa anataja Kamati za Hesabu za Bunge alikuwa anataja PAC na LAAC, lakini anasahu kwamba, kuna POAC, Kamati inayoshughulikia Hesabu za Mashirika ya Umma. Kwa hiyo ni vizuri aliweke vizuri ili isije ikaonekana kwamba, Kamati hiyo imekuwa *ignored*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la nchi yetu ni mipango mibovu na matumizi mabovu ya rasilimali za umma. Viongozi wengi sana wamejaribu kuangalia matumizi ya umma yanavyokwenda katika Taifa letu. Waziri Mkuu, alichukua hatua akafikia mpaka kusitisha uagizaji wa magari ya kifahari, watendaji wamefanya hivyo hata ukiangalia kwenye bajeti wamefanya hivyo. Ukweli ni kwamba, ghamama zile zipo palepale, kwa sababu zimeondolewa kwenye ununuza wa magari ya kifahari zimepelekwa kwenye safari.

Wameondoka kwenye semina na warsha ambazo zilikuwa zinapigiwa kelele na viongozi, lakini kimsingi ni kwamba, bado zile ghamama ziko palepale, kwa sababu *already* zimewekwa kwenye posho na ndio maana ukiingia kwenye bajeti, ukatafuta sasa unafuu huo uliojitokeza kutohana na maelekezo ya Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa juu ya matumizi mabaya ya Serikali, unakuta haupo. Bajeti ya Serikali ya Matumizi ya Kawaida mwaka jana ilikuwa shilingi trilioni 4.8, mwaka huu ni shilingi trilioni 6.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la Mkakati wa Kupambana na *Global Financial Crisis (GFC)*, lakini yale matumizi ya Serikali ya mwaka jana yako pale pale. Kwa hiyo, Watendaji wetu wa Serikali, wanaendelea kuendekeza safari za nje na za ndani. Katika Wizara zetu, tatizo kubwa ni matumizi makubwa mno; hivi kwa nini wewe usafiri tu? Hivi kwa nini ukubali kila mwaliko unaoalikwa wa kwenda nje lazima uende? Kwa nini Katibu Mkuu aende nje mara ishirini kwa mwaka? (*Makofi*)

Nchi yako ni maskini, wakati kipato chako ni kidogo, yaani Taifa hili linaenda kukopa eti kwa sababu Katibu Mkuu asafiri kwenda nje; *why?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoona matumizi ya Serikali yalivyo, tunadanganyana; huku tunasema Kilimo Kwanza, kule tunasema mkakati wa kupambana na mtikisiko wa uchumi Duniani. Sasa nenda kwenye kifungu cha safari; ukichukua Serikali tu, pamoja na Idara zake ni shilingi bilioni sitini na tano safari za ndani na safari za nje ni shilingi bilioni ishirini na nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatulitendei haki Taifa hili, hizi fedha zinaweza zikaenda kufanya kazi kubwa sana za maendeleo huko. Wananchi wetu wanateseka, wanakuwa bila matibabu, umeme hakuna, barabara hakuna; tunaimba tu. Tunataka eti tukakope kwa ajili ya kupeleka umeme vijijini, lakini hizi hela zetu hata tukiongeza pato leo, tukiongeza ukusanyaji wa kodi, bado matumizi ya Serikali yatazidi kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunafikia eti mpaka tuwatoze watu wa Mashirika ya Dini kwa sababu ya safari za watu kwenda nje; *why?* Nenda Hazina, safari za nje bilioni mbili, safari za ndani bilioni tano, hizo ni safari tu. Nenda kwenye *training*, kwenye hicho wanasesma, *Training Domestic, Training Foreign, billions of money* zimepelekwa kwenye vifungu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwatendei haki wananchi wetu na hatulitendei haki Taifa hili. Ukienda kwenye Wizara zenyewe sasa utashangaa sana, hata watu wanaosafiri kwenda nje ni walewale kila siku; anatoka Uingereza anapitiliza safari nyingine England yule yule. Ninaona kuna ubinafsí mkubwa sana katika ugawaji wa rasilimali za umma, watu wanasesafiri tu safari za nje kila kitu safi, nenda kwenye ofisi za chini kule, nenda kwa OCD; Ofisi ya OCD hakuna hata *computer* lakin Makao Makuu watu wanapangiana tu; kama Wizara moja safari za nje inapangiwa shilingi bilioni mbili, wanakwenda kufanya nini kule nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *OCD* wa Wilaya ya Meatu, aliniambia Mheshimiwa Mbunge tununulie hata hizi *used* tu tufanyie kazi, maisha magumu kweli kweli. Nilipita pale Manyoni, wakanambia Mheshimiwa Mbunge, hata hizi *ream* unazoziona tumenunuliwa na Mheshimiwa Diana Chilolo pale Manyoni; hata *ream* hawapati!

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaonekana bajeti hizi tunazopanga, watendaji wetu wanahakikisha zile za Wizarani zinapatikana, lakini zile za kushuka chini zinashuka kwa kiwango kidogo sana. Ndio maana tunasema, kila kwenye bajeti tutasoma tumedhamiria kupeleka *computer* na vitendea kazini, lakini ukija kufuatilia huku hakuna *computer* wala vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu ni mfupi mno, sasa nizungumzie Nishati na Madini. Nishati na Madini pale, tumeona bajeti imeshuka kwa kiwango cha asilimia 24.6; kushuka huko ni sawa kabisa, kosa lililofanyika ni kwamba, zile fedha

zilizookolewa kwa sababu tulikuwa tunazilipa kwenye mikataba, yalikuwa ni matumizi ya kawaida, tumeokoa pale shilingi bilioni 93.3, lakini fedha hizi hazijakwenda kwenye maendeleo, zote hizi zimemezwa kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu; namwomba sana Waziri Mkuu, tusikubali matumizi haya. Nchi yetu iko kwenye hali ngumu, matumizi haya makubwa yaliyopangwa kwa safari; hatuwezi kukataa safari, lakini safari hizo basi ziwe na utaratibu wake. Ukiingia kwenye bajeti utakuta safari za nje na za ndani, kuna mafunzo ya ndani na mafunzo ya nje na posho.

Gharama hizi zote nilizozitaja, lakini bado kuna mafuta na vitu vingine. Gharama hizi zinaweza kupunguzwa na bado Wizara zikaenda vizuri. Nchi hii tulikuwa tunakusanya shilingi bilioni ishirini na tano, Serikali ilikuwa inaendesheka, leo tunakusanya shilingi bilioni mia tatu, lakini zote tunazitumia kwenye matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napendekeza katika haya matumizi ya kawaida, zile *items* nilizozitaja zipunguzwe kwa asilimia arobaini. Fedha hizo zipelekwe kwenye ujenzi wa barabara vijijini. (*Makofi*)

Wananchi wetu wana mateso makubwa, akina mama wanakufa bila matibabu, hawana zahanati, naomba sana fedha hizi tutengeneze fungu la kwenda kuchonga barabara za vijijini. Tunapanga fedha za kutengeneza barabara za vijijini, tunapanga fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara kila mwaka, lakini hakuna fedha inayopangwa kwa ajili ya kwenda kuchonga barabara vijijini. Kwa hiyo, naomba sana fedha zipelekwe kule zikajenge barabara vijijini. Ninaamini Daraja la Lubiga litajengwa na litakamilika ili Wananchi wa Lubiga waepukane na matatizo makubwa wanayoyapata. Barabara za vijijini zote zinazowasumbua wananchi wangu zitakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Kilimo imepambwa kwa rangi nzuri mpaka na pamba imewekwa juu. Tatizo lililopo ni kwamba, tumeamua kuwasaidia wafanyabiashara; ni vizuri lakini tumfidie bei huyu mkulima. Mkulima wetu safari hii atanunuliwa kwa bei ya chini na kwa maana ya mfumko wa bei uliopo na huu mtikisiko, lazima Serikali ifidie fedha hizo na Waziri wakati anahitimisha hoja hii lazima atamke kwamba, Serikali imekubali kufidia hasara ya wakulima watakayoipata, kwa sababu na wakulima walijua kuwa bei itashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mtikisiko wa uchumi na mfumko wa bei ni vizuri sasa bei ya mkulima iweze *ku-break even*, yaani kutokupata hasara wala faida, akachangiwa walau bei yake ifikie shilingi mia sita. Kwa hiyo, wanunuzi watakapokomea, Serikali ikili kwamba, italipa upungufu wa fedha hizo angalau mkulima wetu apate kati ya shilingi mia sita mpaka mia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Serikali imesema sana juu ya suala la GFC, sasa mimi siwezi kabisa kuunga mkono hoja hii kama Serikali haitatamka kwamba, wakulima wetu watafidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri; tumezungumza muda mrefu sana suala la viwanda vyetu nchini na tunategemea wawekezaji na wafanyabiashara binafsi wawekeze katika viwanda ambavyo sisi tunavitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina pendelezo na ushauri wa moja kwa moja kwamba, tufunque mlango wa *venture capital* katika benki yetu ya TIB. TIB ikiwa *venture capitalist*, itakuwa inajenga viwanda tunavyovihitaji nchini, kulingana na mahitaji yetu na kwa wakati ambao tunautaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumzia shilingi tisini na tatu bilioni, ambazo zimeondolewa kwenye Wizara ya Nishati na Madini, zirejeshwe pale na zipelekwe LEA. Umeme wa Ng'oboko, Isengwa, Lubiga na Mwandoya, nina uhakika sasa utawez kujengwa na Wabunge wenzangu wamelalamika hapa wana upungufu mkubwa, watapata fedha. Hizi shilingi 93.3 bilioni zimeokolewa kutoka kwenye kulipa gharama za mikataba na sasa ni fedha ambazo tunazo ila zimeingizwa tu kwenye matumizi ya kawaida, zinyofolewe kule zipelekwe LEA. LEA wana mipango mingi sana ya kujenga miradi ya umeme na hawana fedha, kwa nini fedha hizi ziendelee kutumika kwa matumizi ya kawaida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Kiwanda cha Nyama Shinyanga, tunategemea watu binafsi kila siku. Watu binafsi wawekeze, lakini mtu binafsi anawekeza kama anavyoona yeye; miaka ishirini, miaka kumi; Shinyanga tunahitaji kiwanda cha nyama tangu mwaka 2005, tunaambiwa kitajengwa mpaka leo hakijajengwa na hakijaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafugaji wetu wanalamikiwa kila siku kwamba, hawauzi mifugo wala hawapunguzi mifugo, lakini tatizo kubwa ni Serikali. Sote tunashuhudia ng'ombe wanatoka Meatu wanasafirishwa mpaka Dar es Salaam kutafuta soko, wananchi watembea kwa miguu kutoka Meatu mpaka Arusha, wengine wanaauawa njiani na wengine wanaibiwa ng'ombe wao. Leo serikali inasimama kumlaumu huyu mfugaji; inatakiwa ijue sasa inao wajibu wa kutengeneza masoko ya kuvuna hizi rasilimali za wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitanga mkono hoja. (*Makofit*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa mchango wako, Mheshimiwa Mpina, Mbunge wa Kissesa. Kama nilivyosema mwanzo, anafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Ludovic Mwananzila ajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wake, Katibu Mkuu, na Wakurugenzi. Vilevile naomba niipongeze TRA na

pongezi hizi ziende kwa Mkurugenzi Mkuu, Bwana Kitlya, kwa kutukusanya mapato katika nchi yetu. Kazi ya kutoa hotuba waliyoifanya ni kubwa. Nakumbuka miaka ya nyuma, Waziri wetu mmoja alikwenda Ujerumani; Waziri wa Fedha wa Kijerumani alikuwa haelewi kila anavyoolezwa, mwisho akamwambia, bwana wewe hebu njoo ushike Serikali ya Tanzania kwa mwezi mmoja, mimi nipe niendeshe hii Bajeti ya Ujerumani uone tofauti. Mzee mwenyewe nadhani alikuwa ni Msuya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika kazi ya kutengeneza bajeti na kuendesha Wizara ile ni ngumu. Nawapeni pungezi sana hasa kwa bajeti hii, lakini nilitaka nihitilafiane na ndugu zangu, kila ukisimama basi uiseme tu Serikali, mimi nadhani ni uungwana mtu akisimama aseme mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuipongeza Serikali ya Awamu ya Nne, kwa kazi nzuri waliyoifanya Rufiji. Boma sasa linag'ara na hii kazi ni heshima inayokwenda kwa aliyekuwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo, sasa hivi ni Waziri Mkuu. Yeye mwenyewe alisema tutakarabati limeshakarabatiwa. Mji wa Utete, umeme nimeahidiwa sasa hivi utawaka, maji wanaendesha vizuri wameshachimba mitaro katika Mji wa Utete, sasa wataanza Ikwiriri na Kibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji kumi vya maji vijiji vya *World Bank*, mambo yanaendelea vizuri. Tumeahidiwa kununuliwa panton, itaanza *operation* ikichelewa sana mwezi wa kumi na moja. Mimi naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Serikali kwa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja inayofuata ni bajeti yetu na hali ya uchumi. Niende moja kwa moja kwenye vitabu; ukurasa wa 18 wa Kitabu cha Hali ya Uchumi, ibara ya 33 - 35 na Kitabu cha Bajeti yenye ni ibara ya 98 -100, ukurasa wa 50 hadi 54.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujikita kwenye kilimo na kwamba, Kilimo Kwanza ni habari kubwa katika maisha yetu. Sisi sote tumekula kabla hatujaja hapa na bila chakula utu wa mtu unadhalilika. Hii si mara ya kwanza kwetu sisi kusikia kaulimbiu hizi, katika miaka ya sabini kulikuwa na kaulimbiu ya Siasa ni Kilimo, Azimio la Iringa; miaka ya themanini kukawa na Kilimo cha Kufa na Kupona, Kilimo Utu wa Mgongo; mwaka wa 2006/07 - Tanzania *Green Revolution*, kabla haijaisha tupo Kilimo Kwanza; hivi mambo haya mtu anaweza kukosa wasiwasi? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napata faraja kwamba, Mheshimiwa Rais mwenyewe, ameshikilia bango juu ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo na mimi namwombea Mungu, afanye hivyo asiachie. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika mimi nimeshangazwa, ukitazama ibara hizi tulizosema utakuta pale majigambo makubwa sana; kwanza, tunatengeneza mbolea ya ruzuku, tunatengeneza dawa ya kuulia wadudu, dawa ya magugu, halafu wakataja mikoa inayolima kwa wingi; ningombaa niitaje lakini msinune, nayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Kigoma, Rukwa, Morogoro na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, mbolea imenunuliwa, mvua zilikuwa nzuri tumepata chakula, mwaka huu mbolea imenunuliwa, lakini mvua mbaya hatuna chakula. Huu mchezo wa bahati nasibu ni lazima uishe na hauwezi kwisha kwa kupeleka fedha katika mikoa hii tu bila kutanabahi kwamba, kule Misri na Sudan mvua hazinyeshi, lakini kwa kutumia Mto Nile, hakuna njaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekanaje watu wa Mipango wakasahau kwamba, kuna bonde kubwa la Mto Rufiji? Mto Rufiji ni mkubwa na ni ukombozi, kama tutakwenda kufanya kilimo cha umwagiliaji kule. Ukitazama kitabu kizima hapa, Rufiji haipo; hivi tumewakosea nini? Nitapenda kupata maelezo wakati Waziri ana-wind up. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rufiji haikuandikwa humu na mnajua ni ardhi nzuri, kubwa na ina mto mkubwa. Misri hawana mvua, lakini wanapata chakula kwa ajili ya kutumia ardhi na *irrigation*. Sisi tungeweza kufanya hivyo, tungeepukana na umaskini wa kuombaomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani itabidi kupatikane mabadiliko, maelezo na fikra; haya maneno ya njaa ikija ni Rukwa, hakuna tena kuleta fikra mpya. Tungejaribu kwenda zaidi na kujua ni namna gani tutajikomboa na kuikomboa nchi hii kutokana na njaa.

Mheshimiwa Profesa Mwандося na Mheshimiwa Injinia Chiza, waende pale Rufiji, ardhi tunayo, *wa-irrigate in a big way* na maji yapo. Mnaposikia *Green Revolution of India* ya Gandhi, ilikuwa ni kwa sababu alifanya *irrigation* kubwa, siyo maneno ya kwamba, Rukwa, Mbeya; kila siku mtaandika Rukwa na Mbeya tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kilimo kila mtu anaujua, mpaka sasa hivi pamoja na kuwa kilimo ni yatima, kinachangia asilimia 25 ya pato letu na ukuaji wake ni asilimia 4.6. Tunahitaji kwenda mbele zaidi, tunaomba sana Serikali kama tukipata mahali fedha zaidi, tuipe Wizara hii ya Kilimo ili tupate mazao zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kutanabahi kwamba, huwezi kulima kwa maneno, kwa kununua pikipiki elfu sita na kadhalika, haya majibu ni ya mkato; ukweli ni kwamba, nchi hii wakulima wenye trekta hawazidi asilimia 10; nchi hii *plough* ulimaji wake hauzidi asilimia 20 na kwamba nchi hii asilimia 70 wanatumia jembe dogo; ukombozi ni kununua matrekta mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nirudi kwa wafugaji, ufugaji huu usio endelevu upigwe marufuku. Ufugaji wa huu baba yetu Adam mpaka leo na watu wengine wanadhani kutembea na wale wanyama kila siku ndiyo utajiri, tubadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu kule Rufiji ardhi imeharibika. Inaharibiwa na wafugaji wa ng'ombe waliozidi kiwango bila haki yoyote. Kwanza, tukubali waigawe nchi hii katika sehemu mbili; ya kuchungia na ya kulima chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ukulima leo unachangia asilimia 25, lakini ufugaji unachangia asilimia 4.7; wapi na wapi? Kwa nini usitoe kipaumbele ardhi ambayo ni ya kilimo ibaki kuwa ya kilimo na ardhi kavu ibaki kuwa sehemu ya kulisha mifugo mradi watajengewa mabwawa huko. Hatuwezi kuchanganya ardhi ya kilimo na ardhi ya ufugaji hapo hapo, kama ilivyo Rufiji sasa hivi mnataka kuigeuza Ihefu ya pili, kwa kweli hili jambo *planners* waliangalie kwa makini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Mtulia, nakulinda maana naona Mheshimiwa Lekule Laizer, amegeuza kitikabisa, endelea. (*Kicheko*)

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka mimi ni ufugaji wa kisasa, ardhi igawiwe kabissa; ya kilimo iwe ya kilimo tu na ufugaji ibaki kuwa ya wafugaji. Wafugaji walindwe na wasomeshwe namna ya ufugaji bora, siyo kuwa na makundi makubwa na kuwepo kwa matibabu ya wanyama wao na shule za vijana wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba, nchi hii tumepata Janga la UKIMWI kama nchi nyingine. Jambo ninalozungumza hapa ni kwamba, Serikali yetu sasa ianze kukubali kwamba, kila kilio kina mwenyewe, ukitazama *funding* ya UKIMWI fedha nyingi inatoka *Global Fund Against HIV, Malaria and TB* au *CDC*, lakini sisi wenyewe *hardly more than five percent* ya shughuli za UKIMWI nchini kwetu. Nilikuwa naomba Serikali igeuke iweke fedha pale, kwa sababu hawa jamaa wakikataa nchi yetu tutafanyaje; tukae tu hivi hivi? Hilo ndilo ninaloliomba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni la wanafunzi wetu, kwanza, nashukuru safari hii nimejifunza kwamba, wanafunzi wa sayansi wote watachukuliwa *University* na watapewa mkopo kamilifu. Kitu kinachotisha hivi, niseme tu kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tumejifunza kuwa kuna upungufu wa fedha za mkopo wa wanafunzi. Jambo hili naiomba Serikali sana ikubali kwamba ni hatari sana kwa *stability* ya nchi yetu. Wakianza wale patakuwa hapakaliki, lakini hata hivyo ule utu wetu tu kweli tunaweza kumnyima mtoto aliyepasi vizuri Lifujo asiende *University* kwa kuwa sisi hatuwezi kumsomesha, jambo hili naomba litazamwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka nirudie kuiomba *Planning Commision* yetu ikubali kwamba, Rufiji ni ina ardhi kubwa, ina maji mengi na ukombozi wetu ni *mechanisation and irrigation*, wala siyo hii mbolea tu na kudhani kuwa kutaja mikoa sita italisha Tanzania. Haiwezi wala hatutajikomboa, kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni lazima Rifiji iwekwe katika vitabu vyaa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana *funds* za *HIV*, Serikali ifanye hima iweke bajeti kubwa. Naomba kuunga mkono hoja na nashukuru sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitoe shukrani kwa kupata fursa hii ili na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii

ambayo imesomwa na Wizara ya Fedha, ambayo ukiona inaridhisha hasa kwa wakulima ambao wamepewa matumaini kwamba Serikali inawaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo katika nchi yetu hakiwezi kuendelea kuwa cha kizamani, lazima tutafute njia ya kuboresha kilimo na katika bajeti hii tumelizingatia hilo. Serikali imetangaza Kilimo Kwanza, ili tuweze kujipatia chakula cha kutosha, Mikoa ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Ruvuma na Kigoma, wao walianza zamani wakijua Kilimo Kwanza na Mkoa wa Rukwa, ulianza kujipangia mpango wake unaitwa Mapinduzi ya Kilimo Rukwa; hivyo, hili tunalifahamu na wala humsukumi mtu kwenda kulima au kwenda shambani, yeche anajua wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maksai tunatumia kwa asilimia 80; hivyo, kilimo kimesonga mbele, tatizo ni zana za kilimo, pembejeo, madawa na maafisa ugani, usafirishaji wa mazao kwenda katika masoko na bei duni ambazo wakulima katika Mkoa wa Rukwa wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba haya niliyoyasema, Serikali iyazingatie ili tuweze kupata bei nzuri. Inafurahisha na kusikitisha, unapoona makampuni yaliyokuwa yananunua mazao mengine kama pamba, wanapewa fedha ili waendelee kununua mazao, lakini mkulima wa mahindi ambaye amekuwa akililisha Taifa hili kwa miaka mingi, wala hafikirii kupewa ruzuku au fidia kidogo kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima huyu akiomba umeme asindike mazao, anapata umeme wa kubabaisha. Barabara ndiyo hivyo, kwenda kuchukua mazao Mkoa wa Rukwa ukayaleta kwenye masoko, gharama inaongezeka kwa sababu ya barabara ambazo si nzuri. Tunaishukuru Serikali imeliona hilo na wamefikiria ni jinsi gani ya kuweza kuboresha Barabara Kuu ya Tunduma - Sumbawanga ili mazao yaweze kwenda katika masoko kwa urahisi. Tunawaomba kama bei inakuwa mbaya, sehemu nyingine mturuhusu tuweze kuuza kwa majirani zetu, ambao hawana chakula cha kutosha ili wakulima wetu waweze kupata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mtindo huu wa kuleta vocha za pembejeo kwa ajili ya wakulima, usimamiwe vizuri, kwa sababu kuna ujanja ambao umeingia; watu wanunua vocha kutoka kwa wakulima na kwenda kuchukua fedha benki bila kuwapelekea wakulima mbolea. Naomba sana Wizara ya Kilimo, pamoja na wasimamizi wote kama DCs na Watendaji katika Tarafa na Kata, wasimamie hili ili wahakikishe kwamba, vocha zinazopelekwa ni kwa ajili ya wakulima vijijini na vocha hizo zibadilishwe kwa mbolea, mbegu bora au madawa ili tuweze kuongeza kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu zana za kilimo, serikali imetenga fedha za kutosha na wanasema watanunua matrekta. Tunaomba mikoa ambayo kwa asili ndiyo wamekuwa walishaji wa maeneo yenye njaa, wasaidiwe wapate matrekta haraka ili waweze kuongeza maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Prof. Mtulia pia amezungumza jambo ambalo na mimi nilikuwa nimepanga kulizungumzia; kama tunayo maeneo yanayotunusuru kupata chakula,

tuwekeze kwa ajili ya kupata chakula. Tukigeuza kila sehemu ya Tanzania hata ile inayotoa chakula ni sehemu ya kufugia na kuharibu mazingira ili mvua isinyeshe, Tanzania yote itakuwa jangwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kikwete, amekuwa mwalimu kwa sababu anawaelimisha watu kuhusu mazingira. Makamu wa Rais, ofisi yake inazungumzia juu ya mazingira, lakini Watendaji, wapangaji wa nchi hii, sasa wanataka kuigeuza Tanzania yote iwe ni jangwa la kutembea na kuharibu mazingira. Ndugu zangu, ipo siku tutajuta na kama siyo kipindi chetu lakini vizazi vyetu watakuja kutulaani, kwa kuigeuza Tanzania isiwe na maeneo ambayo ni maalumu. Sehemu ya mifugo ijulikane na watu wakae katika maeneo hayo watumie ufugaji bora, hatukatazi watu wasifuge lakini wafuge kwa mtindo bora. Kama mfugaji atakuwa ana fuga kwa ajili ya kutaka ng'ombe elfu ishirini hadi elfu thelathini, mazingira hayo mtayalinda namna gani? Nawaomba sana Watanzania, nchi hii tumepewa na Mungu, lakini sisi ndio tunaiharibu kwa sababu hatuna mipango mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima ni wapole, mmetumia upole waa na kuanza kuwanyanya isivyo kihalali. Ipangeni Tanzania vizuri ili iweze kuleta manufaa kwa Watanzania wote. Tunatoa chakula kule ambako mnakwenda kuharibu, kuwanusuru wenyenjaa ambao wanatoa mifugo kwenda kuharibu katika nchi ile. Hatuwachukii, lakini jinsi wanavyotumia rasilimali hii inasikitisha sana na Serikali msilipuuze hilo, sote tunahitaji Tanzania hii na sote tunahitaji kufaidika na nchi hii na siyo kuiharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu suala la elimu; Tanzania bila elimu haiwezekani, elimu ni mama wa maendeleo yote Duniani; hivyo ni haki ya kila mmoja wetu katika nchi hii, apate elimu na imsaide katika maisha yake. Bajeti hii imezungumzia kipaumbele kwa mikoa ya pembezoni, hili si jambo la kuonea aibu; hawa watu waliopo mikoa ya pembezoni wamesahaulika kwa muda mrefu; tunaiomba Serikali isione aibu, ihakikishe kwamba, nyumba za walimu zinajengwa ili walimu wakipelekwa kule waweze kukaa kwenye mazingira mazuri lakini na umeme upelekwe kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii nikikueleza kwamba, katika Mkoa wa Rukwa hakuna hata kijiji kimoja ambacho kina umeme, umeme upo Mji wa Sumbawanga na Mji wa Mpanda, lakini nchi hii sehemu nyingine vijijini na kwenye vitongoji wana umeme. Nielezeni hapa ni kijiji gani katika Mkoa wa Rukwa walichowahi kukipangia umeme, hakuna. Matai nimepiga kelele tupate umeme ili tuweze kuendeleza kilimo pale hakuna. Bandari ya Kasanga, imeshindwa kuendelea kwa sababu hakuna umeme, Bandari ya Mpulungu ya Zambia ndiyo inang'ara kwa sababu wana umeme, lakini na sisi tukiweza kung'arisha Kasanga, biashara ya Mpulungu itakwisha kwa sababu rasilimali ya samaki tunayo nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumzia mikopo ya wanachuo, tunazungumzia kuhusu barabara, maabara na tunazungumzia juu ya utendaji bora katika Wizara ya Elimu, lakini wakati wote huwa tunasahau maktaba. Mimi kama mwalimu, ninafahamu kwamba, mwanafunzi bila kitabu ni sawasawa na kulima shamba bila kuwa na mbolea na bila kuwa na mbegu nzuri, hivyo mwanafunzi ili aweze kunufaika zaidi na kuweza

kusoma vizuri zaidi awe na vitabu mbalimbali, pia kuwepo na maktaba. Tunazungumzia juu ya maabara; ni vizuri zaidi kwa sababu tutakuwa na vifaa vya kujifunzia, lakini na suala la kuwa na maktaba za kutosha katika shule zetu ili wanafunzi wawe na namna mbalimbali ya kuweza kupata maarifa mbalimbali kutoka kwenye vitabu kwa kutumia *internent* na *computer*, hatutaweza kuwanufaisha wanafunzi wetu. Tunaomba sana suala hili lizingatiwe ili wanafunzi wetu waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, tumekuwa tukizungumzia juu ya uchumi wa kijiografia; Bajeti hii imejitahidi kidogo kuanza kuelekeza nguvu katika uchumi wa kijiografia wa nchi yetu ya Tanzania. Tuna bahati kwamba, nchi yetu ipo katika eneo hili ambapo tumezungukwa na nchi saba zinazohitaji huduma zetu. Wenzangu wamezungumzia sana kuhusu suala hili, lakini tumekuwa tukilipuuza, tungeweza kuchuma sana lakini kwa sababu ya mikataba mibovu kama wenzangu walivyotangulia kusema, ndiyo maana tunapata matatizo haya. Tuendelee kuwekeza katika miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Serikali imejitoswa inajenga barabara, tunashukuru sana Mkoa wa Rukwa umeingia katika mpango wa kujengewa barabara ya Tunduma – Sumbawanga wa *MCC*. Tunashukuru pia Barabara ya Sumbawanga - Mpanda umeingia katika mpango Serikali itatoa fedha; Matai kwenda Kasanga itaanza kujengwa mwaka huu kwa kiwango cha lami. Tunaishukuru sana serikali imetujali, lakini naomba niendelee kuitahadharisha kwamba, kuendelea kutegemea barabara kuchukua mizigo mizito, haitatusaidia maana barabara hizi zitaharibika katika muda mfupi, mbinu ni kuhakikisha kwamba, tunajenga reli ambazo zitabebe mizigo mizito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Congo wana mizigo mkubwa sana, ambao ungeweza kuchukuliwa na reli zetu kama zingekuwa bora kwa kupitia Zambia na kwa kupitia Kigoma, lakini Reli ziko wapi? Mizigo hata ikirundikana pale bandarini ni kwa sababu hatuna reli ambayo inaweza kuchukua mizigo mizito. Tanzania tunategemea asilimia 90 ya mizigo yake ichukuliwe kwa barabara; barabara zetu hazitadumu, tutaendelea kutumia fedha nyingi sana katika barabara, tunaomba sana mzingatie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu simu za mikononi, kuna eneo ambalo likizingatiwa, fedha nyingi zitapatikana kwa ajili ya bajeti zijazo, hasa katika kipindi hiki. Eneo hili ni la tozo zinazotozwa kwa simu zinazoingia katika nchi hii ya Tanzania, ambapo nchi nyingine ni senti kumi na nne, mpaka senti 28, lakini *Tanzania is the most cheapest* katika dunia hii. Kwa nini usiongeze tukafika hata senti 20 ya dola tukapata fedha nyingi? Ukiangalia muda wa maongezi unaotumika kwa simu zinazoingia humu ndani na kuna mchezo wa kubadili simu za kutoka nje zioneckane ni simu za ndani, tukiweza kudhibiti hapa tutapata fedha nyingi na bajeti hii haitatusumbua. Naomba eneo hili pia mlizingatie ili tuweze kuhakikisha kwamba, tunapata fedha nyingi. Kule kuna fedha nyingi zimefichwa na mambo ya vocha haya ni fedha taslimu, ambazo zinazunguka katika nchi hii, lakini Benki Kuu wala hawajui jinsi zinavyoingia. Naomba tufuatilie kwenye maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kidogo kuhusu matumizi katika Serikali yetu. Inasikitisha, tumeona tangazo la *TRA* ambalo limezungumzia kuhusu misamaha kwa Mashirika ya Dini tunapongeza, lakini *NGOs* ambazo watu binafsi wamekuwa wakijinufaisha, wasipewe misamaha ya kodi; hawa ndiyo wamekuwa wakichezea, lakini Mashirika ya Dini ambayo yamekuwa yakihudumia Wananchi wote wa Tanzania, kwa nini mnaendelea kuwatoza? *CAG* anatoa taarifa kila mwaka kwamba, kuna mabilioni ya pesa yamepotea, Serikali inachukua juhudhi gani kuweza kuhakikisha wale wanaopoteza fedha wanazirejesha, hakuna! Mnataka kuondoa misamaha kwa wale ambao wanatoa huduma kwa wananchi, naomba hili mlizingatie ili tusiendelee kufarakana kati ya Serikali na jamii ambayo imekuwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pensheni za wastaafu; tunaomba tuzifahamu na ikiwezekana ziongezeke na maslahi yaweze kuboreka katika mazingira haya magumu ambayo yanajitokeza hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naiunga mkono hoja hii, lakini tunachoomba yale yaliyopangwa yatekelezwe. Mazingira katika maeneo ya wakulima yaheshimiwe na wapewe kipaumbele katika kupewa pembejeo na zana za kilimo ambazo zitawasaidia ili waongeze maeneo ya kilimo na waweze kuzalisha. Vilevile maafisa ugani ambao hawapo katika vijiji vyetu wapatikane ili waweze kuwasaidia wakulima walime kilimo bora na waweze kuvuna vizuri, mbegu bora zipatikane ili ziwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

**MHE. BUJIKU P. SALIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami nichangie Bajeti Serikali ya Mwaka wa 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nichukue fursa hii, nitoe pole kwa Wana-CCM wa Mkoa wa Mwanza na familia ya Mzee Mdodi, ambaye amefariki na leo ndiyo mazishi yake. Kwa Wana-CCM wa Mkoa wa Mwanza, Mzee Mdodi alikuwa ni mfano na alikuwa ni mzazi wa kuigwa. Baadhi yetu tupo hapa kuitia hekima ya Mzee Mdodi. Tulikuwa tunampenda, lakini Mwenyezi Mungu amempenda zaidi; tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kutumia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu Waziri wake na Watendaji wa Wizara hii, kwa Hotuba ya Bajeti ambayo ni nzuri sana. Mimi naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

Hotuba hii ni ya Waziri wa Fedha na Uchumi na ni Mteule wa Mheshimiwa Rais, kwa masuala ya fedha na uchumi. Kwa hiyo, sina wasiwasi na mantiki yake na ndiyo maana naunga mkono hoja.

Nianze na Ibara ya 58 ya hotuba hii na naomba kwa ruhusa yako niisome. Inasema hivi: “Katika mwaka wa 2009/2010, maeneo yafuatayo yatazingatiwa, pamoja

na mambo mengine ni kutekeleza miradi ya maendeleo inayoendelea kama vile ya barabara, umeme na maji.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura wangu, watashangaa sana nikisema siungi mkono hoja hii kwa sababu kuna mradi wa barabara inayoendelea katika Jimbo langu ya kutoka Mwamarwa kuititia Nyamilama kwenda Ngudu. Amesema Mheshimiwa Waziri hapa itazingatiwa. Kuna barabara kutoka Mwamahaya kwenda Itongoitale, inaendelea kujengwa na kukarabatiwa. Kwa hiyo, watu wanaotumia barabara hiyo, nikisema siungi mkono watanishangaa sana. Barabara kutoka Mabuki kwenda Mara mpaka chini ya Mradi wa PMMR, inaendelea kukarabatiwa na kujengwa. Nikisema siungi mkono, watumiaji wa barabara hiyo katika Jimbo langu watanishangaa sana. Mheshimiwa Waziri, amesema itazingatiwa. Kuna mradi wa maji, hapa amesema barabara, maji na umeme, napenda kutumia fursa hii, kumshukuru Mheshimiwa Mwandosya, pamoja na Wizara yake; kwanza, kwa kukubali Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na Kahama kupelekwa mpaka katika Jimbo la Kwimba, hasa katika Tarafa ya Mwamashimba. Ninashukuru sana, mradi unaendelea na Mheshimiwa Waziri amesema utazingatiwa. Kwa hiyo, sina sababu ya kupinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa upande wa maji; kazi iliyofanyika ni nzuri sana, mpaka sasa maji yameshafika mpaka Mhamalo. Kikubwa tunachohitaji watu wa Jimbo la Kwimba, hasa katika Tarafa ya Mwamashimba ni maji kutumika kwa wananchi walengwa. Tunaomba Wizara ya Maji na Umwagiliaji, pamoja na kwamba, tumewekwa kama Wakala wa KASHWASA, gharama ya kusambaza maji haya ni kubwa sana. Kusema kwamba, kazi hii ifanywe na Halmashauri, itachukua miaka kumi au ishirini, hawa watu wa Mwamashimba kuyapata maji ya Mhamalo. Hivi sasa bado tunapata shida kidogo, kwa nini tuombe msaada? Tumeambiwa kwamba, baada ya maji kufika Mhamalo, tuanze kutumia uwezo wetu. Tunaomba Wizara ya Maji ituelekeze kama tuwasiliane na KASHWASA, TAMISEMI au tuwasiliane na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Hivi sasa tumeshafanya maombi angalau tupate shilingi milioni 100, tuweze kufanya *testing* ya *pump* kutoka Mhamalo kwenda maeneo mbalimbali. Kwa sababu *backbone* ya mradi wa zamani, hatufahamu ilikuwa ina uwezo gani. Tunapenda kupata fedha hiyo, tujaribu kuangalia angalau kufikia maeneo kadhaa. Nafikiri kuwa, hekima iliyotumika kutuletea mradi huo, itatumika pia kutupatia fedha hizo angalau tuweze kufanya *pump testing*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi itakayozingatiwa ni ile inayoendelea, pamoja na ya umeme. Leo asubuhi niliuliza swali kuhusu umeme utakavyopelekwa katika vijiji vyangu kama nilivyokuwa nimeahidiwa kwenye bajeti ya mwaka jana. Mradi unaendelea kwa kadiri ya maelezo yaliyotolewa leo asubuhi. Ilimradi Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameshasema kwamba, miradi hii itazingatiwa, naamini mradi huo utazingatiwa. Asubihi nilifanya maombi, tangu mwaka 1996 ninaomba mradi huo wa kupeleka umeme katika maeneo hayo na hasa katika Jineri mbili ya Mwalujo ya Sanka. Tangu mwaka 1996 hali ambayo inapelekea hata wale wawekezaji wanatishia kuondoka. Majibu niliyopata kwa kweli sikuridhika nayo. Mimi niliuliza ni lini umeme utapatikana lakini maelezo yakawa marefu sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema kwamba, mradi huo umezingatiwa, naamini kwamba utazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejitahidi sana kuomba mradi huo mpaka nikaomba angalau Mawaziri waweze kutembelea na kuona adha wanayopata watu katika maeneo hayo. Nashukuru amekubali kuja, atakuja kukaa mchana na usiku, lakini kikubwa ni kwamba, tunachohitaji ni umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye kaulimbiu ya bajeti yetu “Kilimo Kwanza.” Kaulimbiu ni nzuri sana, tangu uhuru tumekuwa tukilia kilimo, angalau sasa hivi tumeweka kaulimbiu. Wakati mwagine maelezo yanakuwa matamu sana, naomba safari hii hebu tuingie ndani zaidi na tuanze kutekeleza miradi ambayo tumeilenga kwenye kilimo. Kaulimbiu hii kabla haijabuniwa, kulikuwa na ndoto na malengo; napenda kufahamu Serikali ilikuwa na malengo yapi na tutarajie nini kufikia mwishoni mwa mwaka huu? Je, ni kujitosheleza au kulima heka nyingi sana au vipi?

Kwa upande wangu, ninashauri kama kweli tunataka kusonga mbele katika Kilimo, tuwekeze zaidi kwenye suala la Maafisa Ugani. Tukipeleka matrekta hayatatusaidia chochote, wakulima wetu wana heka moja au mbili; kumpeleke trekta mtu ambaye ana heka tano itamsaidia nini; tunachohitaji ni wakulima wetu waweze kulima kisasa na hakuna mtu atakayeweza kuwasadia isipokuwa Maafisa Ugani. Mimi nashukuru, wamesema kwamba, hili nalo litazingatiwa, lakini kutaja na kutekeleza ni mambo mawili tofauti na naomba litekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningepewa nafasi ya kupanga, ilikuwa ni pamoja na kuwajengea nyumba vijijini. Baada ya mafunzo wanapangiwa, leo hii unampeleke trekta mtu ambaye hata kupanda mbegu hajui. Unampeleke trekta kila baada ya mita moja; unamsaidia nini hata mbolea hajui kuitumia? Naomba nguvu tupeleke kwa Maafisa Ugani. Tuwajengee mazingira mazuri, wakae vijijini pamoja na wakulima ili wawepo kule tangu mwanzo wa kipindi cha kulima mpaka mwisho, bila hivyo hatuwezi kufika mbali.

Tutaleta matrekta, yataharibika tutashindwa kuyakarabati, yataozea huko vijijini. Mimi napongeza hili agizo kwamba, kila Halmashauri iagize matrekta madogo madogo. Ninaipongeza hatua hiyo, lakini usimamizi unahitajika. Kuwa na matrekta siyo hoja, lakini utumiaji ndiyo muhimu zaidi. Kwa mkulima aliyezoea jembe la ng’ombe, ukimpatica *power tiller* haimsaidi sana, atapata njaa sana kwa sababu anatumia nguvu nyingi, kwa hiyo, watu wengine watachoka.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba, kila Halmashauri itaagiza *power tillers* 50 au 25, lakini kikubwa zaidi ni jinsi ya kutumia, yawafikie wakulima wengi iwezekanavyo. Wananchi wetu wengi hawana maeneo makubwa sana, hata tungeweza kuwekeza kwenye majembe ya ng’ombe peke yake ingetosha ilimradi tuwafundishe jinsi ya kulima vizuri, kupanda vizuri, kutumia mbolea vizuri na mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda nitumie fursa hii, kwanza, kuipongeza Serikali kwa kukubali kuwapatia ruzuku wale walionunua pamba na kupata hasara mwaka jana. Hili ni jambo jema sana. Kwa kufanya hivyo tunawekeza, bila kufanya

hivyo hata ile pamba ambayo iko kwenye maghala, haitaweza kupata mtu wa kununua. Kwa kuwa tumeshawapatia uwezo, angalau wakulima wetu watakuwa na uhakika wa kuuza pamba yao. Ombi langu; wasitumie nafasi hii ya msukosuko wa uchumi duniani, kutoa bei ya chini sana na ndiyo maana naomba hiyo ruzuku isije ikaishia kwa wanunuzi peke yake, iende mpaka kwenye bei ya pamba. Tuwatie moyo wakulima ili hata mwaka kesho waweze kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda niongelee juu ya kodi ya mafuta ya kupikia. Tunavyo vyanzo nya mafuta ya kula nya kutosha hapa nchini, nafikiri jambo la kwanza ilikuwa ni kuyalinda mafuta yetu. Hatuna uhakika na ubora wa mafuta yanayotoka nje. Mimi naomba tuendelee kama tulivyokuwa tunafanya, waendelee kutoza kodi ya VAT. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengine yameshasemwa na wenzangu, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Naomba kwa haraka haraka, nijumuike na wenzangu kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na timu yake, kwa kazi waliyoifanya kwa kutuletea bajeti hapa. Baada ya kupitia hizi bajeti, nataka nisema tu kwamba, Bajeti hii utaielewa vizuri zaidi ukiangalia maeneo makubwa matatu ambayo ni hotuba ya Mheshimiwa Rais, Hali Ya Uchumi na Hotuba ya Bajeti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Rais, ametueleza hali halisi ya dunia na hali ya uchumi imetupa tahadhari na bajeti ya Mheshimiwa Mkulo tunapanga matumizi. Changamoto, upungufu na kadhalika, yote hayo lazima yawepo kwa sababu ya historia ya nchi yetu, pamoja na utegemezi katika bajeti yetu. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii na hasa ukizingatia barabara za Kigoma kwa miaka hamsini sasa ndio zinajengwa.

Juzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameweka mawe ya msingi kwenye barabara zetu mbili muhimu sana; Barabara ya Mwandiga - Manyovu na Barabara ya Kigoma - Kidawe. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikuhabarishet tu kwamba, baada ya wewe kuweka mawe ya msingi, kuna watu hawakuamini wamesafiri toka Kasulu na Kibondo kuja kuona kama kweli hayo mawe ya msingi yapo. Hii ni kwa sababu wamesubiri kwa muda mrefu na katika hilo tunasema tumechelewa lakini tunapiga hatua. Sisi Wanakigoma, tunaipongeza serikali kwa kazi hiyo nzuri ya kujenga barabara hizi za kutuunganisha na mikoa mingine na hasa hasa nchi jirani na barabara hii ya Kigoma - Kidawe - Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu, barabara ya Kigoma - Kidawe ambayo inajengwa, sasa hivi mkandarasi yupo barabarani. Barabara ya Kidawe - Ilunde - Malagarasi Bridge, ambayo nayo nimeona imetengewa fedha na Daraja la Malagarasi kuna ufadhili wa Serikali ya Korea, Mheshimiwa Rais alihangaika na *Foreign Minister*, Bwana Membe, mlighangaika hangaika pale. Hii barabara kwa tafsiri yake, kwa mkakati wake, itakuwa haina nguvu kama njia hii ya Itigi - Tabora haitajengwa. Nilikuwa naomba sana, wenzetu wa Hazina, litazameni hili jambo kama jambo la kimkakati. Bara bara hii

ili ufile Dar es Salaam, lazima uanzie Kigoma na imeanzia mwanzo wa njia inakuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasisitiza kwamba, barabara hii, nawaomba sana wenzetu wa Mipango na Uchumi, muitazame kimkakati. Hii barabara inakwenda Congo, Burundi, Rwanda na Gabon. Sasa nilikuwa naangalia vitabu vya bajeti, kweli kile kipande cha Kidawe - Malagarasi Bridge, kimetengewa fedha. Tunashukuru Mungu, maana ndio njia inakotoka kuja huku, lakini kipande cha Itigi - Manyoni – Tabora, kimetengewa fedha kidogo na tafsiri yake pana ni kwamba, hata kule kukikamilika, njia hii itakuwa haijapitika. Kuna kitu nataka kusema hapa, barabara hizi tuzitazame kimkakati; barabara ni uchumi, barabara sio anasa ndugu zangu.

Nchi hii, kama wenzetu wa Mipango wangekuwa watu makini, watu wenye mapenzi na Taifa hili, wangeitazama kwa ujumla wake sio vipande vipande. Sasa hivi nchi hii, kimkakati inahitaji barabara tatu kwa sasa. Barabara ya kwanza ni hii ya Manyoni - Itigi - Chaya - Tabora - Kigoma. Barabara ya pili ni hii ya kutoka Iringa - Dodoma - Singida - Babati - Minjingu. Barabara ya tatu, inatoka Tunduma - Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi. Ndizo barabara za kimkakati hizi, sasa mimi nilidhani, wenzetu wa Mipango, kaeni chini muitazame nchi kwa ujumla wake; angalieni ramani vizuri, hizi barabara vipande vipande mnazojenga hapa na pale, hazitusaidii kama Taifa, zinakuwa barabara za kujifurahisha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabra za mkakati za kuinua uchumi wa Taifa letu ni hizo tatu nilizozitaja na sababu zipo. Hii ya kati inakwenda Congo kwenye mzigoo mkubwa, hii ya Tunduma - Sumbawanga - Nyakanazi, eneo la kilimo, Iringa - Dodoma - Singida - Babati eneo la kilimo na kupita Makao Makuu ya nchii yetu ya Dodoma. Unashangaa wenzetu wa Mipango sijui kitu gani kinawavutia zaidi katika mipango hii; hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha mnapanga kweli au ni mtu anakuja tu na utashi wake basi? Haiwezekani.

Nchi hii lazima tuitazame kama *unit* moja, sio vipande vipande. Matokeo yake ndio hayo sasa; Bandari tuna tatizo, Reli tuna tatizo, Viwanja vya Ndege vina matatizo, kwa sababu nchi tunaisemea vipande vipande. Barabara ya *Central Corridor*, tuitazame kwa ujumla wake, pamoja na Bandari. Leo tunahangaika na TICTS; hata ukiwaondoa pale leo, bado mizigo haitafika Congo. Kwa sababu Reli ovyo, Bandari ovyo; sasa unafanyaje katika mazingira hayo? Sasa ajabu iliyoko duniani kote na wachumi walioko Hazina pale wanajua; mizigo mizito inasafiri kwenye meli na kwenye treni; sisi Tanzania kichekesho sasa eti asilimia tatu tu, asilimia 97 yote inasafiri kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo barabara zitakuwa hazipo kwenye miaka michache ijayo na gharama zake ni kubwa mnavyoona. Sasa eti Reli yetu ndio inabeba hiyo asilimia tatu; tubadilishe mtazamo wetu katika mipango yetu na tuwe na vipaumbele vinavyoolewaka. Naomba nchi hii tuitizame kwa ujumla wake, sio katika vipande vipande.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa nilisemee ni hili la Kilimo Kwanza. Sisi Kigoma, sio Kilimo Kwanza ni Kilimo Wakati Wote, maana ndio maisha yetu. Kwa hiyo, hii dhana kama ndio Kilimo Kwanza, naifananisha na Kilimo Ndiyo Utu wa Mgongo, lakini sisi ni Kilimo Wakati Wote na kaulimbiu inapaswa iwe Chakula Kwanza maana ata kilimo cha maua ni kilimo eti. Hapa hoja ni kwamba, kimkakati tujitosheleze kwa chakula. Nchi inayoombaomba chakula, heshima yake inapungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe chini ya Mkakati huu wa Chakula Kwanza, kwa tafsiri yangu mimi, ile mikoa sita ya kilimo pamoja na Kigoma, imejipanga vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu hongera sana, ajenda hii umeibeba na imebebeka. Wananchi wapo nyuma yako katika jambo hili. Tujitosheleze kwa chakula. Aibu hii ya viongozi wetu kwenda kuomba chakula nchi za nje, kwa kweli haipendezi. Yapo mambo ya msingi ya kuzingatia kwenye kilimo hiki jamani; kwa mfano, katika Mkoa wa Kigoma, mbolea iliyokuja msimu uliopita, ilikuja wakati msimu umekwisha halafu unasema Kilimo Kwanza; kipi hicho?

Nikubaliane kwa dhati na hoja ya Mzee Bujiku pale; ndugu zangu, tujikite katika kuongeza uzalishaji, *average* iwe ndio *priority* zaidi kuliko kukimbilia matrekta zaidi. Haya matrekta ni safi kabisa yaje kwa sababu yataongeza eneo la kilimo, lakini ni msingi kabisa mtazamo wetu uwe kuongeza uzalishaji. Tuwatoe wananchi wetu pale tulipo, twende hatua kwa hatua.

Leo nazungumza habari ya trekta, lakini mwanachi hajajua kutumia mbolea sawasawa wala hajajua kulima kilimo cha kisasa. Maeneo ya mbolea, mbegu na huduma za ugani ni muhimu sana na ningeomba yazingatiwe na chini ya mkakati huu. Bila shaka, wenzetu wa Wizara ya Kilimo, watakuja kutueleza vizuri, tunataka mkakati uanze mara moja bila kuchelewa ili hatimaye tujitosheleze kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia lipo kwenye Hotuba ya Bajeti, ukurasa wa 14. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ametueleza kwamba, pale Hazina wameunda kitengo cha kusimamia manunuzi, kwa maana ya sera na usimamizi. Kama ambavyo kila mmoja anafahamu, katika nchi yetu, asilimia 70 ya fedha za maendeleo zinakwenda kwenye manunuzi. Kwa hiyo, ningeshauri *strongly* kwamba, eneo hili, kile kitengo ambacho Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba kinaboreshw, kisiwe kitengo, iwe ni Idara inayojitosheleza, ambayo itasimamia manunuzi haya ili kuendelea kumsaidia CAG katika shughuli zake za kila siku. Upotevu wa rasilimali upo kwenye eneo la ununuzi na kila Mbunge analifahamu jambo hilo.

Kwa haraka haraka, niende kwenye vyanzo vipyta vya mapato. Mimi ni kati ya wale watu ambaa hawavutiwi hata kidogo na utamaduni huu wa Hazina, kila mara kusema vyanzo vya kodi ni vilevile; bia, soda; na sasa cha ajabu wanagombana na Makanisa kuhusu misamaha ya kodi; mbona hatuangalii vyanzo vingine vipyta na wakati viro? Pesa zipo kwenye petroli na gesi, tuliwezeshe Shirika letu la TPDC litufanyie kazi nzuri. Leo hii TPDC, kwenye Mfuko wa Taifa wanachangia zaidi ya shilingi bilioni 50, lakini hawawezeshwi hata kidogo; ni wao wenywewe tu. Sisi kwenye Kamati ya Nishati

na Madini na hili nitaomba ufanuzi na ikibidi hata kushika mshahara wa Waziri; je, ile *retention* ya TPDC imekubalika sasa?

Mheshimiwa Waziri, alituambia kwamba, jambo hili mmeshakubaliana huko; kwamba, TPDC sasa *retention* yao, waweze kujisimamia wenyewe iwe ni *source of revenue*; kuna gesi Songosongo pale nyingi, haiwezi kufika Dar es Salaam kisa hakuna Miundombinu! Hazina hawataki kuwapa *retention* watu wa TPDC. Tuondokane na uvivu wa kufikiri, naomba sana suala la *retention* kwa wenzetu wa TPDC, liwe ni jambo la kufa na kupona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niendele, eneo lingine ambalo ni mapato ni STAMICO; eneo la madini. Tuiwezeshe STAMICO itufanyie kazi. Leo hii STAMICO inajientesha kwa fedha zake yenyewe, inazalisha. Serikali iwekeze TPDC na STAMICO ili yawe maeneo ambayo tunaweza kupata *revenue*, kuliko kung'ang'ania bia, soda na vitu vidogo vidogo. Jambo lingine ni Tume hii ya Bomani, nadhani hatuna haja ya kulizungumza hili. Tume ya Bomani imefanya kazi nzuri, mapendekezo yake sasa yafanyiwe kazi na sisi kwenye Kamati tumearifiwa kwamba, ile Sheria mpya ya Madini inakuja Bungeni. Tunaisubiri kwa hamu sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Kiongozi Mkuu wa Serikali, ile Sheria ya Madini tunaitaka leo ili tufanye kazi kama ambavyo Tume ya Bomani iliainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata simu nyingi za Maaskofu na Wachungaji, maana kule kwenye Jimbo langu la Kasuru Mashariki, sisi tuna hospitali nne za makanisa; Hospitali ya Kabanga, Hospitali ya Harry Mission, Hospitali ya Shunga na Msambala. Kwa kuwa nimesikia Serikali inaendelea kuzungumza lugha inayoeleweka na Maaskofu hawa na Wachungaji hawa, niseme tu kwamba, wale Wachungaji na Maaskofu walionipigia simu, wakae mkao poa, mambo yanakwenda vizuri. Nimewaambia kwamba, Serikali yetu ni sikivu, mambo haya bila shaka yatashughulikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee suala la vipaumbele. Ukiangalia kwenye bajeti, vipaumbele visto sita. Waheshimiwa Wabunge, haiwezekani uwe na vipaumbele visto ni vingi mmo; maana yake hakuna vipaumbele, ndio tafsiri yake. Ukiangalia vipaumbele kwa tafsiri yangu mimi, kipaumbele cha kwanza kinapaswa kiwe elimu, miundombinu na kilimo, hivyo vingine vitaafuata. Ukiangalia bajeti ya elimu, shilingi *1.7 trillion*, miundombinu shilingi *1.09 trillion*, kilimo shilingi *0.7 billion*; ukipiga hesabu hivi vipaumbele muhimu ambavyo ndivyo hasa roho ya uchumi wa taifa letu na uhai wa watu wetu ni theluthi ya bajeti; kwa hiyo, hakuna kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya machache haya, maana kama taifa ni lazima tuendelee kuwepo, naunga mkono hoja hii. Nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, jioni hii. Nadhani sote tutakubaliana kwamba, kazi ya kugawa fedha zaidi ya shilingi trilioni tisa kwa mikoa yote ya Tanzania, pamoja na Wizara zote za Serikali ni kubwa na ngumu; na

hivyo nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kazi nzuri aliyoifanya, akishirikiana na Baraza la Mawaziri; hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia jinsi ya kujikwamua na umaskini wa kipato kwa ujumla kwa kupitia mipango tuliyonayo. Bajeti ya Serikali, imetuonesha mipango mingi mizuri na ambayo itasaidia kuiwezesha Tanzania kuwa mionganoni mwa nchi zenyne viwango vya kati vya mapato na hali bora ya maisha ifikapo mwaka 2025. Pamoja na jitihada hizi, bado serikali imekiri kwamba, kasi ya kupungua kwa umaskini hairidhishi. Hili pia tunaliona katika takwimu ambazo zimejitokeza kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, idadi ya watu wasiojitosheleza kwa mahitaji ya msingi, imepungua kutoka 35.6% hadi 33.4% na wale wasiojitosheleza kwa chakula imepungua kutoka 18.7% hadi 16.5%, kuanzia mwaka 2000 hadi mwaka 2007, lakini hata hivyo, Serikali haikuweza katuonesha sababu ya kasi hii kuwa ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pengine tu nichukue nafasi hii, angalau kuonesha chanzo kimojawapo cha sababu ya kasi hii kuwa ndogo kwa kujiuliza maswali yafuatayo: Tunakuwa na mipango hii na tunao watekelezaji katika Halmashauri zetu na katika ngazi mbalimbali lakini je, hivi viongozi wale au watendaji au wananchi, wanaelewa vizuri hii *Vision 2025* au Dira ya Mpango wa Maendeleo 2025? Wanaelewa vizuri masuala ya MKUKUTA na Malengo ya Milenia? Pengine labda tujiulize; je, zipo *performance indicators* kuhusiana na masuala ya upunguzaji wa umaskini wa kipato katika ngazi zote za Halmashauri na hata Kata? Hata hivyo, tunapowapelekea wananchi wetu au watendaji wetu mipango yetu, je, tunawapa miongozo katika kila mpango wa jinsi gani ya kutekeleza hii mipango? Nadhani kama jibu ni hapana, tunaweza kukubaliana kwamba, pengine tunachokivuna ndicho ambacho kinakuwa kimepandwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nieleze kidogo kwamba, pengine Serikali inakuwa imesema kwamba, labda nataka kuvuna magarage, lakini kumbe bila kuelewa au bila kudhamiria, wale watendaji wetu kule wanakuwa wametupandia mbaazi na ndicho ambacho tunakivuna, kutokana na kwamba hawaelewii vizuri nini tunachotakiwa tukifanye na kumbe wanafanya vile ambavyo haitakiwi. Nitoe mfano mdogo tu kwa upande wa elimu; sasa hivi utakapomuuliza hata yule Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Kata kwamba, mna malengo gani ama mmetekeleza vipi Mpango wa MMES, anawenza kukwambia mwaka jana tulikuwa na mpango wa kwamba 75% ya wanafunzi ambao wamefaulu waweze kujiunga na elimu ya sekondari, lakini tulifikia 80% na mwaka huu tulikuwa tumepanga 90% ya wanafunzi waliofaulu walitakiwa wajijunge na shule za sekondari, lakini hata hivyo tumefikia 100%.

Kwa hiyo, hili ni jambo zuri ambalo limeweza kutupelekea kutuleta mafanikio makubwa katika mpango wa elimu. Ninadhani tutakapoweza kufanya hivi hata kwa upande wa kupunguza umaskini wa kipato, tunaweza tukafikia malengo yetu kwa muda mfupi, ikilinganishwa na hivi ambavyo tunaona kwamba, ndani ya miaka saba tunakuwa tumepunguza huu umaskini wa kipato kwa kiwango kidogo sana (kwa 2.2% tu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nichukue nafasi hii kumpongeza huyu ambaye alianzisha utaratibu huu na niombe tuanzishe utaratibu kama huu kwa upande wa kupunguza umaskini wa kipato.

Nitoe ushauri kwamba, kuanzia sasa tunapokuwa na mipango yetu, kwanza, tuanze kuwaelimisha wananchi wetu na watendaji wetu, kuhusiana na hii *Vision 2025*, lakini vilevile waelewe kwa undani masuala mazima ya MKUKUTA na Malengo ya Milenia. Vilevile tunatakiwa tuwe na *performance indicators* katika Halmashauri zetu na hasa katika Kata zetu na tuhakikishe pia miongozo ya utekelezaji wa mipango yetu, inawafikia wananchi wote hasa wale viongozi. Jambo lingine ambalo ni la msingi kabisa; ni vizuri kila mwaka kukawepo na taarifa kuhusiana na *status* ya utekelezaji wa kupunguza umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia ni jinsi gani tunaweza kupunguza huu umaskini wa kipato, labda nizungumzie kuhusu suala la kilimo. Katika kilimo, naomba nizungumzie *specifically* upanee wa korosho. Zao la Korosho katika nchi yetu, lina nafasi kubwa sana kiuchumi. Zao hili linalimwa katika wilaya 35 za nchi hii. Kwa hiyo, kiujumla tunasema Kilimo Kwanza, lakini katika wilaya hizi 35 tutasema, Korosho Kwanza. Korosho katika wilaya hizi ni ajira na ina faida mbili kubwa kwamba; inauzika hata wakati wa *crisis* na pili ni kwamba, wakati Korosho ya Tanzania inakuwa tayari kuuzwa, korosho katika maeneo mengine ya dunia inakuwa bado haijawa tayari kuuzwa. Kwa hiyo ni vizuri Zao la Korosho likapewa nafasi ya kutosha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nafasi hii, korosho inakuwa na matatizo yafuatayo: Kwanza, mikorosho mingi imezeeka. Pili, wenyewe mashamba ya korosho wengi ni wazee na mashamba haya mengi ni ya urithi. Tatizo lingine, mitaji ni midogo, bei ya korosho pia mara nyingi inakuwa ya chini. Matatizo haya yamesababisha kushuka kwa uzalishaji wa korosho kutoka tani laki moja hadi robo tatu hivi sasa. Kutokana na hayo, nchi nyingi zimetupita katika uzalishaji wa korosho. Hata hivyo, pesa za kazi huwa zinapelekwa kwenye Halmashauri, lakini tatizo hakuna *directives* zinazowawezesha kupanda mikorosho mipyä, utakuta kuna *directives* za kukusanya mapato. Kwa hiyo, ninachoomba ili kulipa nafasi nzuri zao hili la korosho, tuwe na mkakati wa kuanzisha *project* maalumu ya upandaji wa mikorosho mipyä na kuwawezesha wananchi kubangua korosho na ikiwezekana wasimamiwe na Bodi ya Korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia kidogo kuhusiana na yale maeneo ambayo yanakuwa na matatizo ya kipekee kwamba, yafikiriwe kipekee pia. Eneo la kwanza, kuna wale wafugaji ambao wapo Ngorongoro na ninawazungumzia hawa kutokana na kwamba, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. *Carrying capacity* ya Ngorongoro inatakiwa iwe watu elfu 25, lakini kwa sasa wapo zaidi ya elfu 60 na Bodi ya Ngorongoro imejitahidi kuwahamisha wakulima 500 ili waende katika maeneo ambayo wanaweza kulima. Kimsingi, wafugaji hawa wanapenda walime lakini sheria hairuhusu. Sasa ukiangalia unakuta kwamba, mzigo unakuwa mkubwa sana kama Bodi inaachiwa ifanye kazi ya kuhakikisha ustawi wa Wananchi wa Ngorongoro unaendelea kuwa mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo lina matatizo ya kipekee ni wale Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu na ninadhani asubuhi hapa tumemsikia Mheshimiwa Mkapa, akilalamika kuhusiana na tatizo kubwa la kuharibiwa mazao yao na wanyamapori. Tatizo hili ni kubwa na ningependa kushauri kwamba, Kamati itembelee maeneo yale ili iweze kuona tunalitatu vipi tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo kuhusiana na barabara. Barabara moja ambayo ni muhimu kiuchumi ni ile inayotoka Mtwara - Nanyamba - Tandahimba - Newala; kuna matatizo makubwa hapa ambayo yanajitokeza; kila mwaka au kila wakati unakuta vifusi vimejaa lakini matengenezo yake yanakuwa ni ya muda mfupi tu. Hili ni tatizo kwa sababu barabara hii ndio inayotumika katika usafirishaji wa Zao la Korosho. Bahati nzuri, nimedokezwa kidogo na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu kwamba, barabara hii ipo katika mpango wa *MCC*; kwa hiyo, ninaomba Serikali ijithahidi ili matengenezo ya kudumu yaweze kufanyika.

Mheshimiwa mwenyekiti, suala ambalo ni zito sana katika Wilaya ya Tandahimba na Newala ni matatizo ya maji. Mpaka sasa, bei ya ndoo moja ya maji ni shilingi 500 na wakati mwingine imepelekea hata matibabu ya operesheni katika hospitali kusitishwa kutokana na kutokuwepo kwa maji. Tunadhani kwamba, itakapofika mwezi wa tisa, pengine bei ya maji itakuwa kubwa zaidi. Hata hivyo, unaweza ukawa na shilingi 500 yako, lakini usiweze kupata maji. Kwa hiyo, ninachoomba ni kwamba, Serikali ichukue hatua za dharura kuweza kutatua tatizo hili la maji katika maeneo haya, kwa sababu zipo pampu lakini hazifanyi kazi kutokana na matatizo ya umeme.

Hakuna umeme katika wilaya zile, tukisema tusubiri mpaka umeme wa *Artumus*, kwa kweli tutakuwa tumechelewa na wananchi wataendelea kuumia. Kwa hiyo, ninachoomba, ikiwezekana Serikali inunue jenereta ili kuziwezesha hizi pampu zifanye kazi na tuwanusuru wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo kidogo linaonekana linawenza kuwa tatizo kwa baadhi ya wananchi ni kutokea kwa pesa za bandia. Unapokwenda Benki Fulani, kwa mfano, unapewa pesa lakini unapokwenda kuzi-*deposit* kwenye Benki nyingine, wanazihesabu pesa zile zile na katikati pale utakuta kuna pesa bandia! Kwa hiyo, niseme tu kwamba, mwananchi atakapokwenda dukani na pesa na wakagundua kwamba ni pesa bandia; inaweza kusababisha mwananchi yule kupigwa na kujeruhija wakati pengine kosa hili si lake. Kwa hiyo, kwa upande wa Serikali, naishauri iendeleze elimu juu ya utambuzi wa hizi pesa za bandia, lakini vilevile wananchi wajitokeze waweze kutoa taarifa kuhusiana na wale wanaofanya biashara hii ya pesa za bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kwa leo ulikuwa huo, napenda kuunga mkono hoja na kuendelea tena kuipongeza Serikali. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana na kama nilivyosema mwanzo, kwa kuwa Mheshimiwa Nimrodi Mkono, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Nakei hawapo, kwa hiyo, mchangiaji aliyebakia kwa jioni hii ya leo ni mmoja tu, naye ni

Senator Wilson Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini. Kwa maana hiyo, yeye ndiye atakayefunga pazia la uchangiaji katika hoja iliyo mbele yetu. (*Makofi*)

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninakushukuru kwa maneno mazuri uliyoyasema juu yangu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyetujalia afya nzuri sote humu ndani, tukaweza kushiriki mjadala huu mzuri. (*Makofi*)

Pili, kwa heshima kubwa na unyenyekevu, natoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wote wa Bunge wa Serikali, Mkuu wetu wa Wilaya, Viongozi wa Wilaya ya Muleba na Wananchi wote wa Muleba Kusini, kwa kutufariji mimi na familia yangu, tulipoondokewa na mpendwa wetu, baba mkwe, Marehemu Mzee Edward Ngaiza Ndibalema. Nawashukuru sana kwa ushirikiano mlilotupatia, mambo ya msiba yaliisha vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Lollesia Bukwimba, Mbunge mpya wa Busanda, kwa ushindi wa kishindo, uliowadhihirishia watani zetu kwamba, wananchi wanajua kupima. Tulifuatilia mjadala na kampeni, uchaguzi huo ulikuwa ni kipimo kama Serikali ya CCM inastahili kuendelea au isiendelee, wananchi wanasema tuendelee. Nilikuwa nawasikia watani zetu hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye hoja; nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, Manaibu wote wawili, Makatibu Wakuu, Watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kulitumikia Taifa tangu mwaka huu wa fedha ulipoanza, mwezi Julai hadi sasa tunauhitimisha mwezi huu. Nimevutiwa zaidi na taarifa kwamba, fedha ya kigeni hamjaimaliza bado ipo, inayotosha kuagiza bidhaa nje kwa miezi minne na nukta tatu hivi, karibu bilioni mbili, milioni 735.7, si mafanikio madogo. Aidha, nimevutiwa na uwezo wenu wa kudhibiti mfumko wa bei, hadi Aprili ni asilimia 12; nchi jirani wengine wamekwenda mpaka 30%, si kazi ndogo.

Nilichogundua na amekieleza bayana ni kwamba, mfumko wa bei ungekuwa chini zaidi kama tungekuwa na chakula cha kutosha. Kwa sababu mfumko wa bei unaotokana na chakula kuwa bei ghali ambayo imekadirisha kuwa ni 18.6%, ndio umetufanya tuwe katika hali mbaya hii. Ule mfumko wa bei ambao hautokani na bei za vyakula 2.9%, si kazi ndogo.

Kwa hiyo, kaulimbiu ya Kilimo Kwanza ni sahihi na hii nimefurahi kwamba ni kaulimbiu ya mwaka huu wa fedha tunaouanza Julai mwaka huu. Vipaumbele mlivyovipanga kama tulivyokubaliana Februari, kuanza na elimu yakafuatia mambo ya afya, maji, miundombinu na kadhalika; ni sahihi kabisa, mimi nawaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetofautiana na mtoa hoja katika maeneo matatu; eneo la kwanza na hali sio nzuri hata kidogo ni hili la kutaka kuondoa kodi kwa Mashirika ya Dini na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali; jambo ambalo lingeleta madhara makubwa katika nchi yetu na hususan Wilaya ya Muleba na Jimbo la Muleba

Kusini. Sisi tunategemea sana michango ya Madhehebu ya Dini na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali, lakini kazi nzuri ambayo imefanywa na Mheshimiwa Rais na Serikali yake, kukubali michango mizuri ya Wabunge walionitangulia na hususan wa Chama cha Mapinduzi na inastahili pongezi; ninazo taarifa, Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongea na waandishi wa habari saa 10.30 kwamba, pendekezo hili la kuondoa misamaha ya Kodi ya VAT kwa Mashirika haya, Serikali imekubali ushauri wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Ahsante Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imesikiliza jambo zito na ninaamini hata Wabunge, watani zetu, bila shaka wanakubaliana na busara nzuri ya Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningesema nilikuwa natofautiana na Serikali na ninaamini wataendelea kulitafakari kwa sababu Wabunge wengi wamelizungumzia ni mapendekezo ambayo hayasaidii viwanda nya ndani. Mimi sikusomea uchumi, lakini wachangiaji walionitangulia wamelizungumzia vizuri sana. Ukiweka kodi kwa bidhaa kutoka nje, ambayo itaathiri ushindani wa mazao yanayozalishwa na viwanda nya ndani si jambo zuri na ninaamini Serikali itaendelea kulitafakari hilo, kwa sababu Wabunge wengi wamelizungumzia kwa nguvu sana na kwa ufasaha kabisa. Eneo la tatu, ambalo nilikuwa natofautiana na mtoa hoja ingawa naunga mkono hoja yake ni la kuzungumzia kuimarisha usimamizi au mfumo wa usimamizi wa fedha na ufuatiliaji wa miradi katika utekelezaji wake ili kupata ufanisi katika matumizi ya fedha au rasilimali fedha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, tatizo sio mfumo, mfumo ukiimarishwa bila watu kuuhestimu haisadii. Kwa hivi sasa, mfumo uliopo ungeheshimika, fedha nyingi na hususan inayopelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya, ingeweza kuwafikia walengwa na kukidhi matarajio ya Serikali. Serikali inatoa fedha nyingi sana, kwa ajili ya miradi mikubwa na hata Serikali za Mitaa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, lakini fedha nyingi zinaibiwa na nyingine zinafujwa. Kwa hiyo, ningependelea kwamba, mkakati uwe ni kuwawajibisha ambao wanatumia ovyo fedha hizi za Serikali na sio kuimarisha mifumo. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake, huu mkakati wa kusaidia mabenki na baadhi ya wafanyabiashara, kwa sasa hivi ambapo kuna mtikisiko wa uchumi wa dunia; ni jambo la msingi sana. Tukilipuuza, uchumi wetu utaanguka na itabidi tuanze upya. Kwa hiyo, tuwaunge mkono Wabunge kwenye hili ili ushauri ambao wameutoa wa kuangalia namna bora ya kutumia fedha hizi za walipa kodi katika kufanikisha azma nzuri ambayo Mheshimiwa Rais aliifafanua vizuri kabisa, utekelezwe ipasavyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo kwangu naona ni zito sana ni la Muleba Kusini. Umaskini wa kipato Muleba Kusini ni jambo zito sana. Ninamwomba Waziri wa Fedha na Uchumi, ambaye anahuksika na mipango, Muleba pia tunahitaji wataalamu wa kutosha, mahususi wa kufanya utafiti na kutusaidia. Kuna umaskini wa kipato ambao hauonekani, watu wanavaa suti kama mimi na tai, hawana hela mfukoni. Siwatani, nawaambia ukweli; mkitutembelea watu wanavaa vizuri lakini ukimwambia mtu changa shilingi 5000, uadui unaanza hapo hapo. Tunawasifu Wananchi wa Muleba Kusini, kwa sababu wanajilisha muda wote, hawaombi chakula,lakini mvua ikikatika twafa. Tusaidieni kilimo cha umwagiliaji, hizi mvua za kila mwaka zikikatika kidogo tu,

maana yake hatuna mahindi. Mahindi tukichanganya na migomba ni ya kuchoma, maharage tunachanganya humo humo, hayatoshi kula mwaka mzima.

Kwa hiyo, tukipata majanga huwa hata mahindi hatupewi, wanasema tunaona migomba ya kijani; hatuli majani tunakula matunda; ile ndizi. Kwa hiyo, napenda mtuelewe; mkiona ile *green* sio chakula, tuko kwenye msitu. Ukiangalia Kaya kwa Kaya kuna njaa, tusaidieni mpango maalumu na msaidieni Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Angelina Mabula, ambaye ameingia kwa watu wenye umaskini wa kipato. Huyu mama ametuvutia sana, ana mtazamo wa kutuelewa wa kutufahamu ili tushirikiane kuleta mambo, msaidieni ili msije kusema kwamba, ameshindwa kazi kwa kumwambia atuchangishe wakati hatuna cha kuchanga. Tusaidieni msaada maalumu wa kujenga madarasa, tujengeeni madarasa hatutawaomba mahindi. Mkitusaka na kamba na fimbo, watu watakimbia na mengine yanaweza yakatuletea aibu. Hilo niliona niliseme kwa uchungu kabisa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, anastahili pongezi; ukikiangalia Chuo Kikuu cha Dodoma, mimi nakwenda mara kwa mara kukiangalia tu; ukitokea angani ukaangalia Chuo Kikuu cha Dodoma utashangaa; na hiyo imetokana na ujasiri wa uamuzi wa Mheshimiwa Rais kwamba, tuwe na Chuo Kikuu cha Dodoma. Wanafunzi 40,000 si jambo dogo. Mimi niliwahi kuja na wageni kwenye ndege nikiwaleta kwa Mheshimiwa Rais, wakati ule nikiwa kwenye kazi hizo, tulipotua Uwanja wa Dodoma, wageni waliniuliza kwa Kingereza ni umbali gani kutoka hapa kwenda kwenye Mji Mkuu wa Nchi yenu? Tulipotua waliniuliza ni umbali gani, maana waliangalia angani hawakuona mji, tumetua sasa ni umbali gani *tuta-drive* kwenda kwa Mheshimiwa Rais?

Nikasema tumeshafika; lakini naamini wageni wale wale wakija tena, kwa *route* ile ile, watasema kumbe Mji Mkuu wa Tanzania ni pale. Chuo Kikuu cha Dodoma ni kizuri, kikubwa; na ujasiri wa aina hiyo ni wa kuigwa katika sekta zote. Bunge limsaidie Mheshimiwa Rais na namna ya kumsaidia ni Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia Vyuo Vikuu, wanasema kuna pengo la shilingi milioni 80, alipokuwa anachangia hapa nilisikitika kweli; Serikali tafuteni pesa watoto hawa wakopeshwe wasome, mengine yasimame. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mifano ya kwetu; kwetu wazee walikuwa wanauzu mashamba kusomesha watoto na hawa watoto baada ya kusoma wakapata kazi, wameyakomboa mashamba hayo. Sasa sisi tumsaidie Mheshimiwa Kikwete, kwa kuidhinisha pesa za kutosha kwa mikopo ya wanafunzi na kuangalia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kama kweli chumba kimoja wanalala watoto 10 kama alivyosema Mheshimiwa Susan hapa, kama kweli ni aibu. Wanalala Hall 2 na Hall 5, wahandisi wako pale; hivi yale maghorofa yanaweza yakabeba watu mara 10 zile?

Chumba tulikuwa tunalala wawili, vingine mmoja mmoja, sasa 10 wanalala wapi? Fuatilieni haya mambo ya ushauri wa Wabunge, hii imenitisha sana na vyuo vingine kama Sokoine, tuwasaidieni watoto wetu maana sisi uhai wetu umekwisha ili tuweze kundelea vizuri sana. Ahsante kwa uwanja wa ndege wa Bukoba na wameuunganisha na wa Mpanda nikafurahi. Mheshimiwa Pinda, ataanza na wakwetu kabla ya wa Mpanda,

maana kiongozi si unakula wa mwisho? Kwa hiyo, imenivutia zaidi ya kuunganisha, ufanuzi mtafanya baadae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Muleba - Kagomba - Rusahunga imenivutia, shilingi bilioni 19. Serikali imeni-*brief*, *ADB* karibu wanatoa maelezo ya mwisho, kazi yenu ni nzuri sana. Unajua kuna maeneo mengine unatofautiana, lakini mengine unasifu, mambo ni mazuri kwa ujumla. Hongera sana Serikali. Ahsanteni kwa kunisikiliza. Ningefurahi kuzungumza nusu saa nzima kwa sababu ni wa mwisho, lakini kanuni haziruhusu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunivumilia, Mungu awalinde, chapa kazi Serikali tusonge mbele. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Wilson Masilingi, Seneta, kwa maneno yako na hasa kuhusu Chuo Kikuu cha Dodoma, ikitiliwa maanani kwamba, mimi ndio Mwakilishi wa Bunge hili kwenye *University Council* ya Chuo Kikuu cha Dodoma na *University Senate*, inaelekea kazi ninayofanya ni nzuri. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, nilipokea *note* kutoka kwa Mheshimiwa Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, akisema kwamba, juzi alipokuwa akichangia hapa ndani alitereza ulimi kidogo kwa kutaja neno Tandahimba, badala ya neno Namtumbo. Jambo hili limemkwaza kidogo Mheshimiwa Njwayo, Mbunge wa Tandahimba na wapiga kura wake. Anachukua nafasi hii, kuwaomba radhi, lakini pia anasisitiza kwamba, maneno haya hayamaanishi kufuta kauli yake juu ya hali ya shule za msingi. Kwa hiyo, nitawaomba watu wa *Hansard* waangalie jambo hili walirekebishe vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika, ameshatangaza leo asubuhi kwamba, kesho na hasa jioni, kutakuwa na shughuli maalum humu ndani. Labda nianze kwa kusema kwamba, hoja ambayo tumekuwa nayo toka Alhamisi wiki iliyopita, ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, ni hoja ya Serikali ambayo inaliomba Bunge kwamba, likubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha ujao (2009/2010) na kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka uliopita (2008/2009) na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

Sasa hii ndiyo kazi ambayo tumeifanya tangu Jumatatu, toka Mchangiaji wa kwanza mpaka leo alipomalizia Mheshimiwa Masilingi, tumekuwa tukifanya majadiliano kuhusu jambo hilo la msingi.

Sasa hili jambo lina maelekezo yake na ninaomba nichukue fursa hii, kulifafanua kidogo kwa sababu nimesikia baadhi ya Wabunge wakisema hawaungi mkono hoja hii, wengine wakisema watakamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri.

Nianze na wale ambao wana nia na mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nataka kuwaambia tu kwamba, katika taratibu za Bunge, ipo siku ambayo imepangwa kwa ajili ya Wizara ya Fedha na Uchumi na siku hiyo ni tarehe 29 Julai, 2009.

Siku hiyo, italetwa hapa Bajeti ya Wizara hiyo na kufuatana na ratiba yetu, itaambatana na *Appropriation Bill*; kwa maana hiyo, yule ambaye ana nia na mshahara wa Waziri, inabidi asubiri tarehe hiyo; kesho kutakuwa hakuna mshahara wa Waziri hapa. (*Kicheko*)

Kwa wale ambao wana nia ya kutokuunga mkono hoja, niwakumbushe kidogo Kanuni za Bunge zinasema nini; kwa wale wenye Kanuni ni Kanuni za 98(1) na 98(2). 98(1) inasema: “*Mjadala juu ya Hotuba ya Bajeti utakapomalizika na utamalizika kesho rasmi; Spika atalihoji Bunge litoe uamuza wake wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya ibara ya 90(2)(b) ya Katiba.*”

Utaratibu atakaoutumia uko kwenye Kanuni ya 98(2): “*Uamuza wake wa kupitisha au kutokupitisha Bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja.*”

Kwa maana hiyo, Mheshimiwa Spika, ameshatoa wito na mimi nakumbusha umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kuwepo kesho kwenye *session* ya jioni; kwa sababu kwa matakwa hayo ya Katiba na Kanuni, itatakiwa Mbunge mmoja mmoja kwa jina, aseme kama anakubali kupitisha au kutokupitisha Bajeti hii.

Sasa katika taratibu za Bunge, kuna kitu kinaitwa *three lines whip*; tuna *Chief Whips* hapa wanafahamu; hili si jambo la mchezo mchezo hivi; sasa katika kupitisha ama kutokupitisha Katiba inasema nini?

Ibara ya 90(2) inasema, kuna sababu kama tano za kuweza kuvunja Bunge. Mimi sitapitia zile nne, nitazungumzia moja ya sababu ambazo zinaweza zikapelekea Bunge kuvunjwa nayo ni ibara ya 90(2) nasoma Katiba inasema: “*Rais hatakuwa na uwezo wa kulivunja Bunge wakati wowote isipokuwa tu:- (a) kama Bunge limekataa kupitisha Bajeti iliyopendekezwa na Serikali.*”

Baada ya maneno haya, Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizoko Mezani hapa zimeisha na kwa kuwa shughuli zote zimeisha, basi naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. (*Kicheko*)

(*Saa 1.34 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Terehe 18 Juni, 2009 Saa Tatu Asubuhi*)